



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

**HOTUBA YA MHESHIMIWA PROFESA JOYCE LAZARO NDALICHAKO (MB),  
WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA AKIWASILISHA BUNGENI  
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA  
MWAKA 2020/2021**





Maktaba ya Tehama Chuo cha Ualimu Korogwe



Jengo Jipya lenye vyumba vya mihadhara na Ofisi Chuo Kikuu  
Mzumbe Kampasi ya Mbeya





**Mhe. Profesa Joyce Lazaro Ndalichako (Mb.)**  
Waziri



**Mhe. William Tate Ole Nasha (Mb.)**  
Naibu Waziri



**Dkt. Leonard Douglas Akwilapo**  
Katibu Mkuu



**Profesa. James Epiphan Mdoe**  
Naibu Katibu Mkuu



**Dkt. Ave Maria Semakafu**  
Naibu Katibu Mkuu



**HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
MHESHIMIWA PROF. JOYCE LAZARO NDALICHAKO (MB)  
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA  
FEDHA KWA MWAKA 2020/21**

**DODOMA**

**APRILI, 2020**

# YALIYOMO

<b>VIFUPISHO</b> .....	VI
<b>DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA</b> .....	VIII
<i>Dira</i> .....	viii
<i>Dhima</i> .....	viii
<i>Majukumu ya Wizara</i> .....	viii
<b>A. UTANGULIZI</b> .....	1
<b>B. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2019/20</b> .....	4
TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI .....	4
UKUSANYAJI WA MADUHILI.....	5
MATUMIZI YA KAWAIDA .....	5
MIRADI YA MAENDELEO .....	6
TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU.....	6
UONGEZAJI FURSA ZA UPATIKANAJI ELIMU YA MSINGI, SEKONDARI NA VYUO VYA UALIMU .....	6
<i>Ithibati na Usajili wa Shule na Vyuo vya Ualimu</i> .....	7
<i>Utoaji wa Miongozo ya Uratibu wa Elimu ya Msingi, Sekondari na Mafunzo ya Ualimu</i> .....	8
<i>Kusimamia Utoaji wa Elimu Maalum</i> .....	8
<i>Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu</i> .....	9
<i>Kusimamia Ubora wa Elimu katika Shule na Vyuo vya Ualimu</i> .....	11
<i>Kusimamia Ubora wa Elimu Nje ya Mfumo Rasmi</i> .....	12
USIMAMIZI NA UENDELEZAJI WA ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI .....	13
USIMAMIZI NA UENDELEZAJI WA ELIMU YA JUU.....	14
USIMAMIZI NA UENDELEZAJI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UBUNIFU .....	15
<b>SHUGHULI ZILIZOFANYWA NA TAASISI, MAMLAKA NA WAKALA ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20</b> .....	16
<i>Chuo Kikuu cha Dar es Salaam</i> .....	17
<i>Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo</i> .....	19
<i>Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili</i> .....	23
<i>Chuo Kikuu cha Ardhi</i> .....	24
<i>Chuo Kikuu Mzumbe</i> .....	25
<i>Chuo Kikuu cha Dodoma</i> .....	26
<i>Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi</i> .....	27
<i>Chuo Kikuu Huria cha Tanzania</i> .....	28
<i>Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Sayansi ya Kilimo na Teknolojia</i> .....	30

<i>Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam</i> .....	30
<i>Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa</i> .....	31
<i>Chuo cha Ufundi Arusha (ATC)</i> .....	32
<i>Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere</i> .....	34
<i>Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA)</i> .....	35
<i>Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)</i> .....	36
<i>Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya</i> .....	38
<i>Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam</i> .....	39
<i>Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha (NM-AIST)</i> .....	43
TATHMINI YA UTOAJI WA ELIMU NA MAFUNZO .....	44
<i>Baraza la Mitihani la Tanzania - NECTA</i> .....	44
<i>Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania - TCU</i> .....	45
<i>Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE)</i> .....	47
UWEZESHAJI WA UTOAJI WA ELIMU NA MAFUNZO .....	49
<i>Taasisi ya Elimu Tanzania (TET)</i> .....	49
<i>Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)</i> .....	53
<i>Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM)</i> .....	54
<i>Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu</i> .....	56
<i>Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (BOHUMATA)</i> .....	58
UENDELEZAJI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UBUNIFU.....	58
<i>Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)</i> .....	58
<i>Tume ya Nguvu za Atomiki (TAEC)</i> .....	61
<b>C. MPANGO NA BAJETI YA FUNGU 46 KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21</b> .....	<b>64</b>
<i>Ithibati na Usajili wa Shule na Vyuo vya Ualimu</i> .....	64
<i>Usimamizi wa Elimumsingi na Sekondari</i> .....	65
<i>Usimamizi wa Elimu Maalum</i> .....	66
<i>Usimamizi wa Elimu ya Ualimu</i> .....	67
<i>Uthibiti Ubora wa Shule na Vyuo vya Ualimu</i> .....	68
<i>Baraza la Mitihani la Tanzania</i> .....	68
<i>Taasisi ya Elimu Tanzania</i> .....	69
<i>Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu-ADEM</i> .....	71
<i>Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima</i> .....	72
<i>Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (BOHUMATA)</i> .....	73
<i>Mamlaka ya Elimu Tanzania</i> .....	73
<i>Kituo cha Maendeleo Dakawa</i> .....	74
<i>Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu ya Juu</i> .....	82

<i>Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania</i> .....	83
<i>Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu</i> .....	84
<i>Chuo Kikuu cha Dar es Salaam</i> .....	85
<i>Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam</i> .....	86
<i>Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa</i> .....	88
<i>Chuo Kikuu Mzumbe</i> .....	89
<i>Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA)</i> .....	90
<i>Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili</i> .....	92
<i>Chuo Kikuu cha Dodoma</i> .....	93
<i>Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi</i> .....	96
<i>Chuo Kikuu Huria cha Tanzania</i> .....	97
<i>Chuo Kikuu cha Ardhi</i> .....	98
<i>Sayansi, Teknolojia na Ubunifu</i> .....	99
<i>Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia – COSTECH</i> .....	100
<i>Tume ya Nguvu za Atomiki</i> .....	102
<i>Taasisi Teknolojia Dar es Salaam (DIT)</i> .....	106
<i>Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya</i> .....	108
<i>Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha (NM-AIST)</i> .....	109
<i>Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimaliwatu</i> .....	110
<i>Usimamizi wa Rasilimali za Wizara</i> .....	111
<i>Uendelezaji na Uboreshaji wa Sera, Sheria na Miongozo ya Elimu</i> .....	111

**USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYO CHINI YA WIZARA .....112**

<i>Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (Education Programme for Results – EP4R)</i> .....	112
<i>Mradi wa Elimu na Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi (Education and Skills for Productive Jobs - ESPJ)</i> .....	113
<i>Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Ufundi, Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu</i> .....	114
<i>Mradi wa Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MEM) – Kuimarisha Mafunzo ya Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu - KKK</i> .....	114
<i>Mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu (TESP)</i> .....	116
<i>Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu (UTC)</i> .....	117
<i>Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni</i> .....	117
<i>Mradi wa Kuimarisha Ubora Elimu ya Sekondari - SEQUIP</i> .....	118
<i>Mradi wa Kujenga Ujuzi Afrika Mashariki - East Africa for Transformation and Regional Integration Project (EASTRIP)</i> .....	119



<b>D. SHUKRANI .....</b>	<b>120</b>
<b>E. MAOMBI YA FEDHA WA MWAKA 2020/21 .....</b>	<b>122</b>

## VIFUPISHO

<b>ACE</b>	African Centre of Excellence
<b>ACSEE</b>	Advance Certificate of Secondary Education Examination
<b>ADEM</b>	Agency for the Development of Educational Management
<b>AHEAD</b>	African Higher Education Leadership in Advocacy
<b>ANC</b>	African National Congress
<b>ATC</b>	Arusha Technical College
<b>AVN</b>	Award Verification Number
<b>BAKITA</b>	Baraza la Kiswahili Tanzania
<b>CBC</b>	Competence Based Curriculum
<b>CBET</b>	Competence Based Education and Training
<b>CDK</b>	Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
<b>CELMA</b>	Certificate of Education in Leadership and Management
<b>CKD</b>	Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
<b>COSTECH</b>	Commision for Science and Technology
<b>CSEE</b>	Certificate of Secondary Education Examination
<b>DEMA</b>	Diploma in Education Management and Administration
<b>DfID</b>	Department for International Development
<b>DIT</b>	Dar es Salaam Institute of Technology
<b>DPTE</b>	Diploma in Primary Teacher Education
<b>DSI</b>	Diploma in School Inspection
<b>EASTRIP</b>	East Africa Skills for Transformation and Regional Integration Project
<b>EP4R</b>	Education Program for Results
<b>ESDP</b>	Education Sector Development Plan
<b>ESMIS</b>	Education Sector Management Information System
<b>ESPJ</b>	Education and Skills for Productive Job
<b>FDCs</b>	Folk Development Colleges
<b>GPE</b>	Global Partinership in Education Fund
<b>HEET</b>	Higher Education for Economic Transformation

<b>HESLB</b>	Higher Education Students Loan Board
<b>IAEA</b>	International Atomic Energy Agency
<b>IPOSA</b>	Intergrated Programme for Out of School Adolescents
<b>KKK</b>	Kusoma, Kuandika na Kuhesabu
<b>LANES</b>	Literacy and Numerancy Education Supports
<b>MAKISATU</b>	Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu
<b>MEMKWA</b>	Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Watoto Walioikosa
<b>MMEM</b>	Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi
<b>MVTTC</b>	Morogoro Vocational Techer Training Centre
<b>NACTE</b>	National Council for Technical Education
<b>NALMES</b>	National Literacy and Mass Education Strategy
<b>OPRAS</b>	Open Performance Review and Appraisal System
<b>PSLE</b>	Primary School Leaving Examination
<b>QT</b>	Qualifying Test
<b>SADC</b>	Southern African Development Countries
<b>SAIS</b>	South African Innovation Support
<b>SDF</b>	Skills Development Fund
<b>SEQUIP</b>	Secondary Education Quality Improvement Program
<b>SIPA</b>	Students Individual Permament Account
<b>SP</b>	Strategic Plan
<b>STVET-TE</b>	Support Technical Vocational Education Training and Teacher Education
<b>TCU</b>	Tanzania Education for Universities
<b>TEA</b>	Tanzania Education Authority
<b>TEHAMA</b>	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
<b>TEP</b>	Teachers' Educators Programme
<b>TESP</b>	Teachers Education Support Programme
<b>UMISAVUTA</b>	Umoja wa Michezo na Sanaa kwa Vyuo vya Ualimu Tanzania
<b>UNESCO</b>	United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization
<b>VETA</b>	Vocational Education Training Authority

## **DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA**

### **Dira**

*Dira ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni kuwa na Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi, umahiri, uwezo na mtazamo chanya katika kuchangia Maendeleo ya Taifa.*

### **Dhima**

*Dhima ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni kuinua ubora wa elimu na mafunzo na kuweka mifumo na taratibu zitakazoweza kupata Watanzania walioelimika na wanaopenda kujielimisha zaidi ili waweze kuchangia katika kuleta maendeleo ya Taifa letu.*

### **Majukumu ya Wizara**

*Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ina jukumu la kusimamia na kuratibu utoaji wa elimu nchini kwa kuandaa Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali kutoka ngazi ya Elimu ya Awali hadi Elimu ya Juu. Aidha, Wizara ina jukumu la kusimamia na kuratibu maendeleo ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, pamoja na matumizi yake katika nyanja mbalimbali ikiwemo Biashara, Viwanda, Kilimo na maisha ya kila siku kwa ujumla. Wizara inawajibika pia na uendeshaji wa Elimu ya Ualimu, Elimu ya Juu, Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.*

*Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yameainishwa katika Hati Idhini iliyotolewa tarehe 22 Aprili 2016, ambapo imeelekezwa kuwa Wizara itatekeleza majukumu yafuatayo:*

- (i) kutunga na kutekeleza Sera za Elimu, Utafiti, Huduma za Maktaba, Sayansi, Teknolojia, Ubunifu na Uendelezaji wa Mafunzo ya Ufundi;*
- (ii) kuendeleza Elimumsingi kwa kutoa ithibati ya Mafunzo ya Ualimu na Maendeleo ya Kitaalamu ya Walimu;*
- (iii) kusimamia uendelezaji wa mafunzo katika Vyuo vya Maendeleo ya*

*Wananchi;*

- (iv) kusimamia mfumo wa Tuzo wa Taifa;*
  - (v) kuainisha mahitaji ya nchi katika ujuzi na kuuendeleza;*
  - (vi) kuweka viwango vya taaluma ya Ualimu;*
  - (vii) kusimamia Ithibati na Uthibiti Ubora wa Shule;*
  - (viii) kusimamia huduma za machapisho ya kielimu;*
  - (ix) kutegemeza/kuimarisha utumiaji wa Sayansi, Uhandisi, Teknolojia na Hisabati;*
  - (x) kuendeleza wataalamu wa ndani katika Sayansi, Teknolojia na Ubunifu;*
  - (xi) kuratibu na kusimamia Tafiti na Bunifu katika fani za Sayansi, Hisabati na Teknolojia;*
  - (xii) uendelezaji wa rasilimali watu na uongezaji tija ya watumishi walio chini ya Wizara; na*
  - (xiii) kuratibu shughuli za Idara, Mashirika, Wakala, Programu na miradi iliyo chini*
- ya* *Wizara*

## **A. UTANGULIZI**

- 1. *Mheshimiwa Spika***, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, iliyochambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu, likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2019/20. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/21.
  
- 2. *Mheshimiwa Spika***, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuendelea kutimiza majukumu yetu hasa katika kipindi hiki ambacho Taifa letu na Dunia kwa ujumla inakabiliwa na janga la ugonjwa wa Homa kali ya Mapafu inayotokana na virusi vya Corona (COVID-19). Aidha, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwa namna ya pekee na kwa unyenyekevu mkubwa, natoa shukrani za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuendelea kuniamini katika dhamana hii aliyonipa ya kusimamia Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa moyo wa dhati, kwa umakini na uadilifu wa hali ya juu huku nikimtanguliza Mwenyezi Mungu.
  
- 3. *Mheshimiwa Spika***, sina budi kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** kwa uongozi wake thabiti na kwa uzalendo alionao



katika kulinda na kusimamia rasilimali za nchi yetu. Watanzania wanashuhudia miradi mikubwa ya maendeleo ikitekelezwa katika sekta zote muhimu. Tuendeele kumuunga mkono ili aendelee kufanikisha azma yake ya kuleta maendeleo ya kweli katika nchi yetu.

4. **Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) kwa uongozi wao makini, miongozo wanayotoa na ufuatiliaji wanaofanya katika kuhakikisha kuwa malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano yanatekelezwa kwa ufanisi mkubwa. Pia napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake uliotukuka.
5. **Mheshimiwa Spika**, naomba nikupongeze kwa dhati wewe Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai na Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu kwa kuliongoza Bunge kwa umahiri wa hali ya juu. Nawapongeza pia Wenyekiti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuongoza kwa ufanisi mijadala ndani ya Bunge letu Tukufu.
6. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuungana na Wabunge wenzangu waliotangulia kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kumpoteza Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatara, Mbunge wa Viti Maalum, aliyefariki tarehe 20 Aprili, 2020. Marehemu Rwakatara alikuwa ni mmiliki wa Shule za St. Mary's ambazo zinatoa elimu kuanzia ngazi ya Awali mpaka Elimu ya Sekondari. Pia alikuwa ni mmiliki wa Chuo cha Ualimu cha St. Mary's kilichopo Tabata ambacho kinafundisha walimu wa shule za Awali na Msingi. Ni dhahiri kuwa, Wizara imepoteza

mdau muhimu sana katika Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mchango wake katika kutoa elimu tutaendelea kuuthamini na kuenzi. Pia natoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kumpoteza Mheshimiwa Rashidi Ajali Akbar, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini, aliyefariki tarehe 15 Januari, 2020. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

7. **Mheshimiwa Spika**, sote tunatambua kuwa shule pamoja na vyuo vimefungwa ikiwa ni hatua muhimu ambayo Serikali imechukua kuzuia kuenea kwa ugonjwa wa Corona. Wizara yangu imeanzisha vipindi maalum vya Redio na Televisheni ili wanafunzi waendeleo kupata elimu katika kipindi ambacho wapo nyumbani. Hivyo, natoa wito kwa Wazazi na Walezi kuendelea kuwasimamia Watoto wetu ili kuhakikisha wanaendelea kujisomea na kwamba hawatoki nyumbani bila kuwa na sababu za msingi. Aidha, napenda kuwasihi wanafunzi, walimu na wadau wote wa elimu kwa ujumla, kuendelea kuzingatia maelekezo yanayotolewa na Wataalam wa Afya ili kuepuka maambukizi ya ugonjwa wa Corona.
8. **Mheshimiwa Spika**, naomba kuwapongeza Mawaziri walioteuliwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mbunge wa Kibakwe) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mbunge wa Ilala) kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na Mazingira.
9. **Mheshimiwa Spika**, Naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba (Mb), Makamu Mwenyekiti,

Mheshimiwa Juma Nkamia (Mb), na Wajumbe wote wa Kamati kwa maoni na mapendekezo yao, ambayo yamechangia kuongeza tija katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri mlionipa kwa kipindi chote cha uhai wa Bunge hili. Mwenyezi Mungu awabariki sana.

- 10. *Mheshimiwa Spika***, naishukuru kwa dhati familia yangu kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu ya kitaifa na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa utulivu.
- 11. *Mheshimiwa Spika***, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/20 na Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/21.

**B. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2019/20**

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI**

- 12. *Mheshimiwa Spika*** katika mwaka wa fedha 2019/20 Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha **Shilingi 1,386,508,723,272.00** kwa ajili ya Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambapo **Shilingi 523,788,923,012.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 862,719,800,260.00** zilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO - Fungu 18 Bunge liliidhinisha kiasi cha **Shilingi 2,156,017,000.00** ambapo **Shilingi 1,532,293,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 623,724,000.00** kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Tume.

## **Ukusanyaji wa Maduhuli**

- 13. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Wizara kupitia Fungu 46 ilitarajia kukusanya maduhuli yenye thamani ya **Shilingi 553,739,899,119.13** ambapo kiasi cha **Shilingi 13,942,894,000.00** kilipangwa kukusanywa na Idara na Vitengo, na **Shilingi 539,797,005,119.13** zilipangwa kukusanywa na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2020, Wizara ilikuwa imekusanya **Shilingi 335,148,981,970.31** sawa na asilimia **60.5** ya Makadirio.
  
- 14. Mheshimiwa Spika,** kupitia Fungu 18 – Tume ya Taifa ya UNESCO, Wizara ilipanga kukusanya maduhuli yenye thamani ya **Shilingi 27,000,000.00** kutokana na malipo ya mrabaha kutoka katika uchapishaji wa Jarida la Tume. Hadi kufikia mwezi Machi 2020, kiasi cha **Shilingi milioni 8.5** sawa na asilimia **31.48** ya lengo kilikuwa kimekusanywa.

## **Matumizi ya Kawaida**

- 15. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2020 Wizara ilikuwa imepokea Jumla **Shilingi 396,788,907,260.36** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kupitia Fungu 46, ambazo ni sawa na asilimia **75.8** ya fedha za Matumizi ya Kawaida zilizoidhinishwa. Aidha, kupitia Tume ya UNESCO – Fungu 18, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 1,176,454,000** sawa na asilimia **54.56** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

## **Miradi ya Maendeleo**

- 16. *Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Machi 30, 2020 Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi 734,890,659,288.20** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambayo ni sawa na asilimia **85.20** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo **Shilingi 459,937,828,356.68** ni fedha za ndani na **Shilingi 274,952,830,931.51** ni fedha za nje.

## **TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU**

- 17. *Mheshimiwa Spika***, sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2019/20.

## **Uongezaji Fursa za Upatikanaji Elimu ya Msingi, Sekondari na Vyuvo vya Ualimu**

- 18. *Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ina wajibu wa kuhakikisha Elimu ya Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu inaendelea kutolewa kwa ubora kwa kuzingatia fursa sawa kwa wote ili kuwawezesha wahitimu kukabiliana na mazingira pamoja na kuwa na utayari wa kuendelea na ngazi za elimu zinazofuata. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali imetekeleza yafuatayo:

- (i) imewezesha ujenzi wa matundu ya vyoo 9,712 (Wasichana - 5,539, Wavulana - 3,645 na Walimu - 528) miundombinu ya maji, matanki ya maji 911 pamoja na miundombinu ya kunawia mikono katika shule za Msingi 602 kupitia **Mradi wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni;**
- (ii) imekamilisha taratibu za ununuzi wa mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari inayojengwa eneo la Iyumbu – Dodoma

kupitia **Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo – EP4R;**

- (iii) imeendelea na ujenzi wa Chuo cha Ualimu Kabanga ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2020 kupitia **Mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu;**
- (iv) imeendelea kuboresha miundombinu na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kukarabati Vyuo vya Ualimu 9 kupitia Mradi wa Lipa kulingana na Matokeo. Vyuo hivyo ni: Singachini, Monduli, Mamire, Bustani, Bunda, Katoke, Vikindu, Mtwara Kawaida na Mtwara Ufundi
- (v) imeendelea na Ujenzi na ukarabati wa Vyuo vya Ualimu Mpuguso, Ndala, Kitangali, na Shinyanga kupitia **Mradi wa Uboreshaji Vyuo vya Ualimu – UTC.**

### ***Ithibati na Usajili wa Shule na Vyuo vya Ualimu***

**19. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza jukumu la upatikanaji wa fursa ya Elimu na Mafunzo, Serikali imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) imesajili jumla ya shule 395 zilizokidhi vigezo kati ya 407 zilizoomba kwa mchanganuo ufuatao: Awali Pekee 15 (Zisizo za Serikali), Awali na Msingi 265, (Serikali 144, Zisizo za Serikali 121) na Sekondari 115 (Serikali 87 na Zisizo za Serikali 28);
- (ii) imeendelea kutengeneza mfumo wa Kielektroniki wa Usajili wa Shule za Awali na Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ualimu na Vituo Nje ya Mfumo Rasmi ili kuwezesha usajili wa shule kufanyika kwa uwazi na kwa wakati; na
- (iii) imetoa jumla ya leseni 253 za kufundishia zikiwemo 240 kwa walimu wa kigeni na 13 kwa wataalam raia wasio walimu.



***Utoaji wa Miongozo ya Uratibu wa Elimu ya Msingi, Sekondari na Mafunzo ya Ualimu***

- 20. *Mheshimiwa Spika***, katika kusimamia na kuratibu utoaji wa Elimu ya Msingi, Sekondari na Mafunzo ya Ualimu, katika mwaka wa fedha 2019/20 Serikali imetekeleza kazi zifuatazo:
- (i) imehuisha Mwongozo wa Mafunzo ya Malezi, Unasihi na Ulinzi wa Mtoto kwa Walimu wa Shule za Msingi, Sekondari na Wakufunzi wa Vyu vya Ualimu;
  - (ii) imehuisha Mwongozo wa utoaji wa Huduma za Elimu kwa Wanafunzi wenye Ualbino ili kuongeza uelewa wa wadau kuhusu wajibu wao na mahitaji ya kielimu kwa wanafunzi hao; na
  - (iii) imeandaa Kiunzi cha Mafunzo Endelevu Kazini kwa Walimu (*Teachers' Continuous Professional Development Framework*) ambacho kitakuwa nyenzo ya kuwaendeleza walimu kitaaluma na kitalaamu ili kuongeza ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji.

**Kusimamia Utoaji wa Elimu Maalum**

- 21. *Mheshimiwa Spika***, pamoja na kuendelea kuimarisha utekelezaji wa afua zenye kuhakikisha elimu yetu inakuwa jumuishi, Serikali imetekeleza yafuatayo;
- (i) imenunua na kusambaza vifaa maalum vya kielimu katika shule maalum na vitengo 424 ili kuboresha ujifunzaji na ufundishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum;
  - (i) imetoa mafunzo kazini kwa walimu 269 kutoka shule 23 za sekondari nchini kuhusu matumizi ya Lugha ya Alama na mbinu za kufundishia. Aidha, imetoa mafunzo kazini ya Lugha ya Alama kwa walimu 183 wanaofundisha shule zenye wanafunzi Viziwi; na

- (ii) imenunua na kusambaza Vifaa vya Wanafunzi na Wakufunzi wenye mahitaji maalum katika vyuo vya Ualimu Patandi, Mpwapwa na Mtwara Kawaida ili kuwawezesha kufundisha na kujifunza kikamilifu.

### ***Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu***

**22. *Mheshimiwa Spika***, Serikali inatambua umuhimu wa walimu katika kuinua ubora wa elimu nchini. Katika kipindi cha mwaka 2019/20, Serikali imeendelea kuhakikisha inaimarisha elimu ya ualimu na kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu ambapo yafuatayo yametokelezwa:

- (i) kugharamia chakula na malazi kwa wanachuo wote katika vyuo vyote 35 vya Serikali;
- (ii) kuimarisha elimu ya michezo ikiwa ni pamoja na kuendesha mashindano ya michezo na sanaa katika Vyuo vya Ualimu (UMISAVUTA). Mashindano hayo yamefanyika kuanzia ngazi ya Vyuo, Kanda na Taifa na kuhusisha michezo ya riadha, mpira wa miguu, mpira wa pete, mpira wa kikapu na mpira wa wavu. Vilevile, mashindano ya sanaa za maonesho (nyimbo, michezo ya kuigiza na ngoma), uchoraji na utengenezaji wa zana za kufundishia na kujifunzia yalifanyika.
- (iii) kununua magari 39 kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo – EP4R, ambapo magari 35 yamegawiwa katika Vyuo vyote vya Ualimu vya Serikali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi katika vyuo hivyo na magari 4 ni kwa ajili ya kuimarisha ufuatiliaji na tathmini;

**23. *Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu imetokeleza yafuatayo:

- (i) imenunua na kusambaza katika vyuo vya Ualimu vya Serikali aina 449 za vitabu zenye jumla ya nakala 25,709 kwa ajili ya masomo yote yanayofundishwa vyuoni;
- (ii) imeendelea kuimarisha mafunzo kwa njia ya TEHAMA katika vyuo vyote vya ualimu vya Serikali ikiwa ni pamoja na kununua *Servers* mbili kwa ajili ya kuweka mfumo wa ufundishaji na ujifunzaji (Learning Management System).
- (iii) imenunua na kusambaza katika Vyuo vya Ualimu, kompyuta 480, *UPS* 480, *Photocopy Machines* 35, kompyuta mpakato 43 ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa njia ya TEHAMA;
- (iv) imetoa mafunzo kazini ya TEHAMA kwa wakufunzi 530 wa kutoka katika vyuo 17 vya Ualimu (Butimba, Murutunguru, Bunda, Tarime, Katoke, Ndala, Tabora, Kasulu, Shinyanga, Kabanga, Mamire, Monduli, Patandi, Singachini, Marangu, Mandaka na Korogwe) ili kuwajengea uwezo wa kutumia TEHAMA kama nyenzo ya ufundishaji na ujifunzaji;
- (v) inaendelea na uunganishaji wa Vyuo vyote 35 katika Mkongo wa Taifa kwa lengo la kuimarisha mifumo na matumizi ya TEHAMA katika Vyuo vya Ualimu;
- (vi) imetoa mafunzo kazini ya TEHAMA na Teknolojia saidizi kwa Walimu 125 na Wakufunzi 9 wenye mahitaji maalum ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kutumia TEHAMA;
- (vii) imetoa mafunzo kazini kwa walimu 771 (Msingi 451 na Sekondari 320) katika Halmashauri 20 zenye ufaulu wa chini katika somo la Hisabati kwenye mitihani ya Kitaifa kwa lengo la kuwapa Walimu mbinu na njia fanisi zaidi kufundishia na kujifunzia somo hilo. Halmashauri zilizopewa mafunzo hayo ni: Korogwe, Chemba, Gairo, Momba, Nyasa, Madaba, Rufiji,

Ruangwa, Nanyamba, Butiama, Nachingwea, na Tandahimba kwa shule za sekondari na Mkalama, Simanjiro, Meatu, Chemba, Ukerewe, Kilindi, Musoma na Lushoto kwa shule za Msingi;

- (viii) imeandaa miongozo ya mafunzo ya TEHAMA na Teknolojia saidizi kwa Wakufunzi na Walimu wenye mahitaji maalumu ili waweze kufundisha na kujifunza kwa urahisi zaidi;
- (ix) imeandaa miongozo ya mafunzo kazini kwa wakufunzi wa Vyuo vya Ualimu kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji; na
- (x) imefanya ufuatiliaji kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari waliopata Mafunzo ya ufundishaji wa Hisabati ili kutathmini tija ya mafunzo waliyopata.

### ***Kusimamia Ubora wa Elimu katika Shule na Vyuo vya Ualimu***

**24. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa taasisi zilizopata Ithibati na Usajili zinatoa elimu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu. Kutokana na azma hiyo, katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali imetekeleza yafuatayo:

- (i) imefanya tathmini ya mazingira ya utoaji wa elimu katika asasi 4,102 zikiwemo Shule za Msingi 3,251, Sekondari 837 na Vyuo 14 vya Ualimu na kutoa ushauri wa kitaalam na kitaaluma kwa ajili ya kuboresha utoaji wa elimu;
- (ii) imefanya ufuatiliaji katika asasi 516 zikiwemo Shule 428 za Msingi, Sekondari 76 na Vyuo vya Ualimu 12. Ufuatiliaji huo ulilenga kufanya tathmini ya jumla ya shule ili kubaini kama wamiliki wa asasi hizo wametekeleza ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Wathibiti Ubora wa Shule;

- (iii) imefanya ukaguzi maalum katika asasi 548 zikiwemo shule 363 za Msingi na 185 za Sekondari kwa ajili ya kupewa kibali cha Usajili, ambapo shule 395 zikiwemo za Msingi 280 na za Sekondari 115 zilikidhi vigezo na kupatiwa usajili;
- (iv) imeongeza Wathibiti Ubora wapya 400 wa Shule katika ofisi za Kanda na Wilaya;
- (v) imenunua kompyuta na *printer* 153 na kuzisambaza katika Ofisi mbalimbali za Uthibiti Ubora ili kurahisisha utendaji kazi kwa Wathibiti Ubora wa Shule;
- (vi) imekamilisha ujenzi wa ofisi mpya 100 za Uthibiti Ubora wa Shule za Wilaya na inaendelea na ujenzi wa ofisi nyingine mpya 55 ili kuongeza ufanisi wa utendaji wa Wathibiti Ubora; na
- (vii) inaendelea na utaratibu wa ununuzi wa magari 65 ya Uthibiti Ubora wa Shule ili kuimarisha ufuatiliaji.

***Kusimamia Ubora wa Elimu Nje ya Mfumo Rasmi***

**25. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi inatolewa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu na kuwafikia walengwa kwa ufanisi. Ili kufikia azma hiyo yafuatayo yamefanyika:

- (i) kufanya ufuatiliaji wa programu za Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ikiwemo programu ya Elimu Changamani kwa vijana walio nje ya mfumo rasmi (Intergrated Programme for Out of School Adolescents - IPOSA); na
- (ii) kutoa elimu ya katika Vituo vya Elimu Nje ya Mfumo Rasmi kwa vijana 13,036 (Wanawake 7,625 na wanaume 5,411).

## **Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi**

**26. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali imetekeleza yafuatayo:

- (i) imewezesha ununuzi wa vifaa vya ufundi vya kufundishia na kujifunzia (Technical Equipments) katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54 ili kuboresha utoaji wa mafunzo katika vyuo hivi; na
- (ii) imewezesha ujenzi wa mabweni mawili (2) katika Chuo cha Walimu wa Ufundi Stadi cha Morogoro (MVTTC) ili kuongeza upatikanaji wa fursa za elimu kwa wakufunzi wa vyuo vya ufundi stadi;
- (iii) imegharamia chakula cha Wanachuo 5,520 katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54;
- (iv) imewezesha mafunzo ya muda mrefu ya Ufundi Stadi na Elimu ya Wananchi (*Folk Education*) kwa washiriki 7,079 katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54 ili kuwapa ujuzi unaohitajika kwenye soko la ajira;
- (v) imetoa mafunzo ya muda mfupi ya Ufundi Stadi na Elimu ya Wananchi (*Folk Education*) kwa washiriki 1,079 katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54 ili kuwaongezea ufanisi katika shughuli mbalimbali za uzalishaji katika maeneo wanayoishi;
- (vi) imeratibu uanzishwaji wa vituo vinne (4) vya umahiri kwenye nyanja za TEHAMA, Usafiri wa anga, Nishati jadidifu na Mazao ya ngozi katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Chuo cha Usafirishaji cha Taifa na Chuo cha Ufundi Arusha kupitia mradi wa *East Africa Skills for Transformation and Regional Integration Project (EASTRIP)*;
- (vii) imewezesha ushiriki wa wabunifu katika Mashindano ya Ubunifu –



*African Challenge Tech Awards* yaliyofanyika Kenya - Nairobi na kuhusisha nchi 8 ambapo Timu ya Tanzania iliibuka mshindi wa pili na kupata zawadi ya \$100,000, pamoja na ufadhili wa kusoma nchini China;

- (viii) imeendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa nne (4) kwa ajili ya madarasa, maabara na ofisi za walimu kwa lengo la kuimarisha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika Chuo cha Ufundi Arusha;
- (ix) imeendelea kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu ya ufundi stadi na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kutekeleza awamu ya pili ya ukarabati na upanuzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 20 (FDCs); na
- (x) imewezesha vijana 2,534 kupata mafunzo ya uanagenzi.

### **Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu ya Juu**

**27. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali inatambua umuhimu wa Elimu ya Juu katika juhudi za kuifikisha nchi yetu katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali imetekeleza yafuatayo:

- (i) imeendelea kugharamia wanataaluma 620 katika ngazi za Shahada ya Umahiri 196 na Uzamivu 424 kutoka Vyuo Vikuu vya Serikali kwa lengo la kuboresha Elimu ya Juu kwa kuwa na wahadhiri waliobobea katika fani zao;
- (ii) imeratibu ufadhili nje ya nchi wa wanafunzi 115 wa Kitanzania (China 61, Hungary 29, Uingereza 7 na Algeria 18);
- (iii) imeratibu uchambuzi wa wanafunzi watakaonufaika na ufadhili kwa mwaka wa masomo 2020/21 kutoka Jumuiya ya Madola -

Uingereza, China, Hungary, Malaysia na Venezuela;

- (iv) imefadhili wanafunzi 10 raia wa China kusoma Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa mujibu wa mkataba uliopo na kwa lengo la kukuza Lugha yetu adhimu ya Kiswahili; na
- (v) imefadhili wanafunzi 207 (Umahiri 107 na Uzamivu 100) kupitia Mradi wa Vituo vya Umahiri vya Africa (African Centres for Excellence ACE II) katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha (NM-AIST).

### **Usimamizi na Uendelezaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**

**28. *Mheshimiwa Spika***, katika kuratibu na kusimamia uendelezaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu nchini, Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/20 imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) imetambua na kuhakiki teknolojia 231 zilizozalishwa nchini kwa lengo la kuwa na kanzidata ya kitaifa itakayorahisisha upatikanaji wa taarifa kuhusu teknolojia hizo.
- (ii) imeendelea kuandaa mahitaji ya mfumo wa kanzidata ya teknolojia zinazozalishwa nchini kwa kushirikiana na Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Kumbukumbu (NIDC)
- (iii) imefanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi saba (7) ya utafiti inayofadhiliwa na Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA) katika Sekta za Maji, Afya, Kilimo na Mifugo na kubaini kuwa utekelezaji wa miradi hiyo unafanyika kulingana na makubaliano; na
- (iv) imeshiriki Mkutano Mkuu wa 63 wa Shirika la Nguvu za Atomiki

Duniani (IAEA) uliofanyika Vienna, Austria Septemba, 2019 ambapo miradi mipya mitano (5) ya utafiti katika Sekta za Maji, Afya, Kilimo na Mifugo imepata ufadhili wenye jumla ya **Euro 965,220** sawa na **Shilingi 2,414,045,190.13**.

- 29. Mheshimiwa Spika,** katika kuwajengea uwezo wabunifu kuhusu kulinda na kuendeleza ubunifu kuwa fursa za kiuchumi, Serikali imewaendeleza wabunifu 60 waliopatikana katika Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) ya mwaka 2019. Aidha, bunifu za wabunifu 12 zipo katika hatua ya kutengeneza bidhaa za mfano (prototypes) tayari kwa kuingia sokoni.
- 30. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeratibu mashindano ya MAKISATU kwa lengo la kuibua, kutambua na kuendeleza wabunifu na wagunduzi nchini. Mashindano yalikusisha wabunifu kutoka Makundi 7 ya wabunifu ambayo ni: Wanafunzi wa Shule za Msingi; Shule za Sekondari; Vyu vya Ufundi Stadi; Vyu vya Ufundi wa Kati; Mfumo usio Rasmi; Vyu Vikuu; na Taasisi za Utafiti na Maendeleo. Jumla ya wabunifu 621 walijitokeza kushiriki mashindano ambapo wabunifu mahiri 70 (10 kutoka katika kila kundi) walipatikana na kushiriki kilele cha mashindano hayo. Wabunifu watatu mahiri kwa kila kundi walipewa tuzo mbalimbali na ubunifu wao utaendelezwa ili kufikia hatua ya kuwa bidhaa na kubiasharishwa.

## **SHUGHULI ZILIZOFANYWA NA TAASISI, MAMLAKA NA WAKALA ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20**

- 31. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu majukumu ya Taasisi, Mamlaka na Wakala zilizo chini yake ili kuhakikisha nchi

inazalisha rasilimaliwatu yenye weledi kwa kuzingatia mahitaji ya Mipango ya ndani ya nchi, Soko la Kikanda na Kimataifa. Shughuli zilizofanyika kwa kila Taasisi ni kama ifuatavyo:

### **Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

**32. *Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam imetekeleza yafuatayo:

- (i) imedahili jumla ya wanafunzi 28,511 wakiwemo Astashahada 483, Stashahada 802, Shahada 24,368, Stashahada ya Uzamili 191, Shahada ya Umahiri 2,300, Shahada ya Uzamivu 320 na kozi za muda mfupi wanafunzi 47 katika Kampasi Kuu ya Mwl. J.K. Nyerere;
- (ii) imeongeza idadi ya miradi ya utafiti ili kutatua changamoto mbalimbali katika jamii kutoka tafiti 135 hadi 173;
- (iii) imeongeza idadi ya machapisho katika majarida ya Kitaifa na Kimataifa kutoka machapisho 735 hadi 1,048 (Kitaifa) na 11 hadi 13 (Kimataifa) kwa lengo la kutatua changamoto za kijamii, kuelimisha na kujitangaza kimataifa;
- (iv) inaendelea na mradi wa ufungaji gesi asilia kwenye nyumba 35 za wafanyakazi na Kafeteria zote za chuo, Kampasi ya Mwalimu Nyerere ili kuhakikisha mazingira ya chuo yanahifadhiwa; na
- (v) imegharamia masomo ya uzamili kwa wanataaluma 35 (31 – Uzamivu na 4 Umahiri) ili kupunguza changamoto ya upungufu wa Wahadhiri.

**33. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha mazingira ya ustawi wa wanafunzi na wafanyakazi, Serikali imetekeleza yafuatayo;

- (i) imekarabati Bweni Na. 1 Kitalu G linalotumiwa na wanafunzi wenye mahitaji maalum lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 63. Aidha, inaendelea na ukarabati wa majengo ya Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia;
- (ii) imeendelea na ukarabati mkubwa wa mabweni Namba 2 na 5 yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 788 kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo. Kukamilika kwa mradi huu kutakiwezesha chuo kufikia jumla ya wanafunzi 11,103 wanaopata malazi katika Kampasi ya Mwl. J. K. Nyerere;
- (iii) imekamilisha ukarabati mkubwa wa nyumba 5 za watumishi kwa lengo la kuboresha mazingira ya makazi;
- (iv) imeendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa tano la kituo cha wanafunzi kwa lengo la kutoa huduma mbalimbali ikiwemo huduma za kujisomea, kupumzika, kufanya michezo ya ndani, migahawa, benki, maduka ya vitabu na ofisi za Serikali ya wanafunzi na Mshauri wa wanafunzi;
- (v) imeendelea na ujenzi wa mfumo mpya wa maji katika Kampasi ya Mwl. J. K. Nyerere ambapo inahusisha kuweka upya mabomba makubwa mapya na kujenga tenki la maji lenye mita za ujazo 500,000, mashine kubwa nne (4) za kusukuma maji na ulazaji wa bomba jipya la inchi 16 lenye uwezo wa kusafirisha maji kiasi cha lita 360,000 kwa saa; na
- (vi) imeendelea na ujenzi wa Jengo la huduma katika Hosteli za Dkt. J. P. Magufuli ambapo jengo hilo linahusisha maduka, *ATM, Hair Salons, Dry cleaner, Dispensary, Mgahawa na Supermarket.*

## **Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo**

**34. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, imetekeleza yafuatayo:

- (i) imedahili jumla ya wanafunzi wapya 4,873 kati yao Shahada za awali 4,208 (Wanawake 1,361 na Wanaume 2,847) na Shahada za Umahiri wanafunzi 194 (Wanawake 79 na Wanaume 115) na masomo yasiyo ya Shahada (*Non-degree Programme*) wanafunzi 471 (Wanawake 192 na Wanaume 279);
- (ii) imeanzisha kampasi mpya iliyopewa jina la Waziri Mkuu mstaafu Mhe. Mizengo Peter Kayanza Pinda katika Mkoa wa Katavi ambayo itatoa masomo ya Stashahada, Astashahada na Shahada katika nyanja za Kilimo na Mifugo. Uanzishwaji wa Kampasi hiyo unalenga kutekeleza malengo ya Serikali ya awamu ya tano ya kuwa na Tanzania ya viwanda. Kampasi hii itasogeza huduma za kitaalamu kwa wananchi wa Mkoa wa Katavi na Mikoa ya jirani;
- (iii) imeendelea kuviongezea uwezo vitengo vyake vya uzalishaji vikiwemo: Vitengo vya kuzalisha mikate, maziwa na mbogamboga; na
- (iv) imeimarisha Hospitali ya Taifa ya Rufaa ya Wanyama, Taasisi ya Elimu ya Kujiendeleza, kumbi za mikutano na Idara ya Huduma za Afya kwa lengo la kuongeza mapato ya ndani ya chuo na kupunguza utegemezi kwa Serikali.

**35. *Mheshimiwa Spika***, katika eneo la Tafiti na Ushauri elekezi, Serikali kupitia Chuo imetekeleza yafuatayo:

- (i) imeendelea na miradi mipya 13 ya utafiti yenye lengo la kuboresha uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo, misitu na uvuvi

ili kuwezesha wananchi kuzalisha mali na malighafi za mazao ya kilimo kwa ajili ya viwanda;

- (ii) imetoa huduma ya elimu ya ushauri wa kitaalamu kwa wakulima 9,500 kwa kutumia vituo atamizi, mashamba darasa, semina, kozi fupi, runinga na redio kwa lengo la kuongeza uzalishaji wenye tija na kupunguza umaskini kwa wananchi. Mafunzo hayo yametolewa kwa wakulima katika mikoa ya Mwanza, Dar es Salaam, Iringa, Dodoma, Tabora, Tanga, Pwani na Morogoro;
- (iii) imeandaa na kushiriki katika maonesho mbalimbali ya kitaifa ya: kilimo *Nane Nane* yaliyofanyika kitaifa Mkoani Simiyu na kuwafikia takribani wadau 8,000; Kamisheni ya Tume ya Vyuu Vikuu; Kumbukizi ya Hayati Edward Moringe Sokoine na Maonesho ya zana za Kilimo kwa lengo la kutoa elimu kuhusu kilimo na ufugaji; na
- (iv) imepima jumla ya sampuli 1,553 zikiwemo sampuli za udongo 1,180, za mimea 297, za mbolea za viwandani 20, za samadi tisa (9) na sampuli za maji 47 kutoka kwa watafiti, Mashirika ya kilimo, Viwanda na Taasisi mbalimbali pamoja na wakulima binafsi kupitia maabara yake ya udongo iliyopo Idara ya Sayansi ya Udongo na Jiolojia.

**36. *Mheshimiwa Spika***, ili kujenga uwezo wa wafanyakazi na wanafunzi katika kufanya tafiti za kisayansi na kilimo kwa lengo la kuongeza uzalishaji wenye tija katika shughuli mbalimbali za maendeleo kwa wananchi, Serikali imeingia mikataba mipya 13 ya mahusiano na Taasisi nyingine za ndani na nje ya nchi. Taasisi hizo ni pamoja na: Chuo Kikuu cha Sophia kilichopo Japan; *National Institute of Health - Korea*; *Foundation Pierre Fabre - France*; *Kunming Institute of Zoology*,

*Chinese Academy of Science; Silverlands Tanzania Limited - Iringa, Tanzania; College of Animal Science and Technology Nanjing Agricultural University - China; Agronomos Sin Fronteras Foundation (ASFF ) - Iringa Tanzania; University of Leeds – UK; na Wuhan University (WHU) – China.*

**37. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia Serikali imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) imejenga jengo lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,400 kwa wakati mmoja litakalokuwa na maabara nane (8) zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 100 kila moja na madarasa nane (8) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200 kila moja kwa gharama ya **shilingi bilioni 11.5**. Kukamilika kwa jengo hilo kutapunguza changamoto ya ufinyu wa nafasi za kufundishia na kujifunzia uliopo chuoni;
- (ii) imenunua vifaa mbalimbali vya maabara, kemikali za kufundishia na samani za ofisi;
- (iii) imekamilisha ujenzi wa jengo la utafiti wa wanyama na wadudu - *Animal House* kwa ufadhili wa mradi wa *Eastern and Southern Africa Centers of Excellence for Innovative Rodent Pest Management and Biosensor Technology Development (ACE II, IRPM and BTD)*;
- (iv) imeendelea na ukarabati wa madarasa likiwemo jengo la *Hay Building* kwa lengo la kuongeza nafasi za kufundishia na kujifunzia;
- (v) imeendelea na ukarabati wa karakana za uhandisi kilimo ambao umelenga kuboresha karakana za uhandisi kilimo hivyo kukamilika kwake kutawapa fursa wanafunzi kufanya mafunzo



kwa vitendo kwa kutumia vifaa vya kisasa; na

- (vi) imeboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kufunga mfumo wa mawasiliano - *wireless point* kwenye kumbi za mikutano na maeneo yanayozunguka chuo. Aidha, chuo kinaendelea kuboresha mifumo ya kurusha matangazo kwa njia ya runinga na redio ili "SUA *media*" iweze kuwafikia wananchi wengi.

**38. *Mheshimiwa Spika***, Serikali imeboresha shamba kwa kupanda mazao ya Taifa ya kimkakati kwa kuandaa eneo lenye ukubwa wa hekari 200 kwa ajili ya kupanda zao la katani ambapo hekari 80 zimepandwa na zoezi la upandaji linaendelea. Uboreshaji wa shamba hilo umechochewa na matrekta yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Aidha, chuo kimeboresha shamba darasa kwa kufunga vifaa vya kisasa vya kilimo na kupanda mazao ya kitaifa ya kimkakati kama vile zabibu, pamba, katani, kakao, kahawa, mananasi, migomba na mazao ya mbogamboga.

**39. *Mheshimiwa Spika***, ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira, Serikali imeanzisha Programu zifuatazo;

- (i) Shahada za Umahiri tisa (9) ambazo ni: *MSc. Seed Technology and Business; MSc. Horticulture; MSc. Environmental Sciences, Management and Technology; MSc. Hydrogeology and Water Resources Management; MSc. Public Health Pest Management; MA. Development Planning and Policy Analysis; MSc. Acquacture; PhD. Agribusiness na PhD. Agro-ecology;*
- (ii) Shahada za kwanza mpya nne (4) ambazo ni: *Bachelor of Agricultural Investment and Banking; BA Human Resources,*

*Management and Labour relations; BA in Development planning and Management na BSc in Bee Resources management; na*

- (iii) Programu zisizo za Shahada katika fani mbili (2) ambazo ni *Certificate in Tour Guiding and Hunting Operations* na *Diploma in Crop Production and Management*.

### **Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili**

**40. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili imetekeleza yafuatayo:

- (i) imedahili jumla ya wanafunzi 1,329 wa Shahada na Stashahada na kuongeza fursa za elimu kwa wanafunzi;
- (ii) imeongeza idadi ya moduli kutoka 40 hadi kufikia 155 zinazotolewa kwa kutumia jukwaa la TEHAMA. Vilevile, imeongeza usajili wa wanaotumia jukwaa la TEHAMA kutoka wanafunzi 715 hadi kufikia wanafunzi 2,597 kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa elimu;
- (iii) inaendelea na ujenzi wa kituo cha Umahiri wa magonjwa ya moyo na mishipa ya damu - *Center of Excellence in Cardiovascular Sciences* ambapo kazi ya kimuundo, *skimming* ya jengo na uwekaji wa dari katika chumba cha mikutano umekamilika na uwekaji wa umeme na mifumo ya mtandao unaendelea;
- (iv) inaendelea kutekeleza tafiti 102 ambapo 31 ni mpya na zimepata ufadhili. Tafiti hizi zimejikita katika maeneo mbalimbali ya magonjwa ambukizi, yasiyoambukiza na magonjwa yasiyopewa kipaumbele; na

- (v) imefanya maboresho katika “Shule ya Tiba Meno” ikiwemo kufanya ukarabati wa chumba kwa ajili ya kutolea huduma binafsi na mchakato wa kupatikana kwa vifaa tiba unaendelea.

### **Chuo Kikuu cha Ardhi**

**41. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Ardhi imetekeleza yafuatayo:

- (i) imedahili jumla ya wanafunzi 4,393 kwa lengo la kutoa fursa ya elimu ambapo wanafunzi wa Shahada ya kwanza 4,127, Shahada ya Umahiri 200 na Shahada ya Uzamivu 66;
- (ii) imeendelea kufanya miradi ya tafiti 43 yenye lengo la kutatua changamoto katika jamii ili kuboresha maisha yao kwa ujumla;
- (iii) imeandaa jumla ya machapisho 37 ya tafiti zilizokamilika kwa ajili ya kuongeza maarifa katika jamii kuhusu kutatua changamoto katika maeneo ya usimamizi wa ardhi na mazingira, uboreshaji wa makazi na usanifu wa majengo;
- (iv) imetoa mafunzo kwa jamii kuhusu usimamizi bora wa Ardhi na Sheria za Ardhi kwa wakazi wa Wilaya za Mkuranga, Kisarawe na Nachingwea yaliyolenga kupunguza migogoro ya ardhi. Aidha, imetoa mafunzo kuhusu utengenezaji wa mkaa mbadala kwa kutumia mabaki ya mazao ya kilimo kwa wakazi wa kata za Igawa, Mabadaga, Uburaku, Igurusi, Ruiwa, Utengule, Rujewa, Mswiswi na Madibira katika Wilaya ya Mbarali;
- (v) imeendelea kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu kuhusu usanifu majengo, utayarishaji wa mipango ya kuendeleza miji na uthamini ikiwemo ujenzi wa Shule ya Mfano Dodoma na jengo la ofisi za Uhamiaji Dodoma, jengo la Mahakama ya Wilaya ya

Chato na kuandaa *Master Plan* ya Mji wa Mafinga;

- (vi) inaendelea na ujenzi wa bweni lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 592 ili kuongeza sehemu za malazi; na
- (vii) imewezesha wafanyakazi 48 kwenda masomoni wakiwemo wanataaluma 37 (Uzamivu 25 na Umahiri 12) na wafanyakazi waendeshaji 11.

### **Chuo Kikuu Mzumbe**

**42. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Mzumbe imetekeleza yafuatayo:

- (i) imesajili jumla ya wanafunzi 11,967 na kati ya hao, wanafunzi 5,310 ni wanafunzi wa mwaka wa kwanza (Astashahada 411, Stashahada 598, Shahada ya Kwanza 3,587; Shahada ya Uzamivu 14);
- (ii) imegharamia masomo kwa watumishi 103 wakiwemo wa Shahada ya Uzamivu 67, Shahada ya Umahiri 27 na Shahada ya Kwanza 9;
- (iii) imeandaa na kuchapisha Makala 104 katika majarida mbalimbali ya ndani na nje ya nchi; sura za vitabu ("book chapters") 10, pamoja na kitabu kimoja kwa lengo la kusambaza matokeo ya tafiti na kazi mbalimbali za kitaaluma ili kutoa maarifa yanayolenga kutatua changamoto katika jamii. Aidha, utekelezaji wa miradi 26 ya utafiti katika maeneo mbalimbali ikiwemo uchumi wa viwanda unaendelea; na
- (iv) imeendelea na ujenzi wa madarasa na kumbi za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 na ofisi zenye uwezo wa kuchukua wafanyakazi 50 katika Kampasi Kuu; ukarabati na

uwekaji wa samani katika majengo ya Tegeta, Kampasi ya Dar es Salaam yenye uwezo wa kuchukua takribani wanafunzi 1,500 pamoja na maktaba, maabara ya kompyuta na ofisi za wafanyakazi. Aidha, imekamilisha ukarabati wa hosteli mbili (2) katika Kampasi ya Mbeya, pamoja na hosteli tatu (3) na nyumba saba (7) za watumishi katika Kampasi Kuu.

### **Chuo Kikuu cha Dodoma**

**43. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Dodoma imetekeleza yafuatayo:

- (i) imedahili jumla ya wanafunzi 27,133 wakiwemo wapya 10,447 na 16,686 wanaoendelea na masomo;
- (ii) imejengea uwezo wafanyakazi 441 ambapo wafanyakazi 234 walipata mafunzo ya muda mfupi na 207 mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za Astashahada (10), Stashahada (22), Shahada ya kwanza (11), Shahada ya Umahiri (77) na Shahada ya Uzamivu (87);
- (iii) imeajiri wafanyakazi 61 wa kada tofauti ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi;
- (iv) inaendelea na ujenzi wa jengo la kitengo cha huduma za mionzi katika hospitali ya chuo kwa lengo la kuongeza wigo wa utoaji huduma za mionzi kwa wanafunzi, wafanyakazi na jamii; na
- (v) imeendelea na ukarabati wa majengo ya ofisi, makazi, mabweni, madarasa, miundombinu ya barabara pamoja na viwanja vya michezo ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

- 44. *Mheshimiwa Spika***, katika eneo la Tafiti na Ushauri Elekezi, Serikali kupitia Chuo imefanya jumla ya tafiti 11 katika maeneo ya Elimu, Mazingira na TEHAMA. Vilevile, imetoa huduma za ushauri nne (4) katika nyanja za TEHAMA na elimu ili kuongeza ufanisi wa huduma mbalimbali zinazotolewa katika jamii. Aidha, imejenga mahusiano na taasisi nyingine 49 katika nyanja za ubunifu, Afya na Elimu.

### **Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi**

- 45. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi imetekeleza yafuatayo:
- (i) imedahili jumla ya wanafunzi 7,231 wakiwemo Astashahada 1,363, Stashahada 1,148, Shahada ya kwanza 4,448 na Shahada za uzamili 272. Aidha, imepata ithibati ya programu mbili (2) za Shahada ya Umahiri;
  - (ii) imetoa mafunzo kwa wafanyakazi 64 (wahadhiri 55 na wafanyakazi waendeshaji 9) ambapo Shahada ya Uzamivu ni 42, Shahada ya umahiri 20, Shahada ya Kwanza mmoja (1) na Stashahada mmoja (1);
  - (iii) imetekeleza mradi wa kutoa mafunzo ya kilimo, biashara na ujasiliamali (Skills Development Fund) kwa wanafunzi wa mwaka wa pili na wa tatu wa shahada za kwanza ili kuwajengea uwezo wa kujiajiri pindi watakapomaliza masomo;
  - (iv) imeandaa machapisho manne (4) ya utafiti yanayohusu ushirika na biashara, sayansi jamii, sheria na mazingira kwa lengo la kusambaza matokeo ya utafiti kwa wadau mbalimbali; na
  - (v) imetoa mafunzo kwa vyama 101 vya ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) katika wilaya 61 za Tanzania Bara

yaliyofadhiliwa na “*Market Infrastructure, Value Addition and Rural Finance (MIVARF)*”. Mafunzo hayo yalilenga kuvijengea uwezo Vyama vya Ushirika katika usimamizi na uendeshaji.

**46. *Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi imetekeleza yafuatayo:

- (i) imefanya ukarabati na upanuzi wa mabweni tisa (9) ambapo mabweni sita (6) yapo katika Kampasi Kuu ya Moshi na matatu (3) katika kituo cha Kufundishia Kizumbi kilichopo Shinyanga. Ukarabati huo umewezesha upatikanaji wa nafasi mpya 460, matundu ya vyoo 40 na mabafu 38 na kufanya mabweni hayo kuwa na jumla ya nafasi 962, matundu ya vyoo 68 na mabafu 66; na
- (ii) imekamilisha ujenzi wa kafteria yenye uwezo wa kuchukua watu 100 kwa wakati mmoja kwa lengo la kuongeza maeneo ya utoaji wa huduma ya chakula kwa wanafunzi na wafanyakazi pamoja na ukuta wenye urefu wa mita 200 kwa lengo kuimarisha usalama wa wanafunzi na mali za chuo.

### **Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**

**47. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania imetekeleza yafuatayo:

- (i) imedahili jumla ya wanafunzi 4,198 wakiwemo wanafunzi wa mafunzo ya awali 1,009, Astashahada 517, Stashahada 175, Shahada ya kwanza 1,532, Shahada ya Umahiri 903 na Shahada ya Uzamivu 62 kwa lengo la kuongeza fursa za elimu;

- (ii) imekamilisha uwekaji wa kompyuta 20 katika maabara ya kituo cha mkoa wa Geita na kompyuta mpakato 20 katika Mkoa wa Mara na kufunga mfumo wa mawasiliano kwa lengo la kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji kwa njia ya TEHAMA;
- (iii) imeimarisha mtandao wa kujifunzia kwa njia ya masafa kwa kutengeneza programu mpya 35 ambapo kati ya hizo 30 zilipitishwa na Tume ya Vyuho Vikuu;
- (iv) imefanya ukarabati wa ukumbi wa Mitihani katika Kituo cha Mkoa wa Mwanza na kuendelea na miradi ya ujenzi katika vituo vya mikoa ya Manyara na Geita;
- (v) imeendesha mafunzo ya wiki mbili kwa walimu 837 wa Shule za Msingi wanaosomea Stashahada ya Ualimu wa Shule za Msingi '*Diploma in Primary Teachers Education – DPTE*' kwa mwaka wa kwanza na wa pili katika vituo vifuatavyo: Chato (237), Korogwe (145), Mtwara (85), Njombe (130) na Singida (240) ili kuwaongezea ujuzi wa utendaji kazi;
- (vi) imeunganisha mfumo wa kujifunzia (OUTLeMS) na mfumo wa rejesta ya wanafunzi (SARIS) ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia ambapo kwa sasa mifumo hii inafanya kazi pamoja; na
- (vii) imeimarisha mafunzo kwa vitendo kwa kuzindua maabara tatu (3) za Sayansi katika masomo ya Kemia, Fizikia na Bailojia zilizopo katika kituo cha Kinondoni.



## **Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Sayansi ya Kilimo na Teknolojia**

**48. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Sayansi ya Kilimo na Teknolojia imetekeleza yafuatayo:

- (i) imeandaa mitaala 35 ikiwemo Shahada za Sayansi 26 na Astashahada za taaluma za Sayansi za kilimo tisa (9);
- (ii) imeajiri watumishi 82 kati yao wahadhiri ni 42 na waendeshaji ni 40; na
- (iii) imeendelea na jitihada za upatikanaji wa hatimiliki katika maeneo ya chuo kama ifuatavyo:
  - (a) imepata hatimiliki ya ekari 231 zikiwemo ekari 95 katika kampasi ya Kinesi Halmashauri ya Rorya na ekari 136 kampasi ya Kisangura Wilaya ya Serengeti;
  - (b) inaendelea kukamilisha taratibu za kupata umiliki wa ekari 61 kutoka eneo la Oswald Mang'ombe ambapo awali lilikuwa ni shule ya sekondari;
  - (c) inaendelea kukamilisha umiliki wa eneo la BAIC lenye ukubwa wa ekari 1,512 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Butiama ambalo litakuwa makao makuu ya chuo; na
  - (d) inaendelea na majadiliano ili kupata eneo katika Hospitali kuu ya Rufaa Mkoa wa Mara na eneo la Kwangwa kwa ajili ya Stadi za Afya na Sayansi shirikishi.

## **Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam**

**49. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam imetekeleza yafuatayo:

- (i) imedahili jumla ya wanafunzi 1,943 kati ya hao Shahada ya kwanza ni 1,878 na Stashahada ya Uzamili 65;
- (ii) imenunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji;
- (iii) imefanya jumla ya Tafiti 14 za sayansi na teknolojia zenye lengo la kutatua changamoto za kijamii; na
- (iv) imeendelea na ujenzi wa jengo la utawala awamu ya pili kwa lengo la kuboresha mazingira ya utendaji kazi.

### **Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa**

**50. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa imetekeleza yafuatayo:

- (i) imedahili jumla ya wanafunzi 6,315 (Wanaume 3,535 na Wanawake 2,780) ili kuongeza fursa za elimu;
- (ii) imetoa mafunzo kwa wahadhiri kuhusu namna ya kuandaa mihtasari ya sera - *Policy brief writing*, usimamizi wa wanafunzi wa shahada za juu - *Postgraduate supervision* na namna bora ya kubadilisha maudhui ya kwenye Tasnifu (*Dissertation*) kuwa Machapisho (*Journal Paper*) katika majarida ya kitaifa na kimataifa ili kuongeza maarifa, weledi na ufanisi katika utendaji kazi;
- (iii) imeendelea kutekeleza miradi mitano (5) ya utafiti na imeanza utekelezaji wa miradi saba (7) mipya katika nyanja za kilimo, afya, na mabadiliko ya tabia nchi. Tafiti hizo zinalenga kutafuta njia salama za kukabiliana na wadudu waharibifu wa mazao;

- (iv) imetoa jumla ya machapisho 24 katika nyanja mbalimbali za kitaaluma zenye lengo la kuongeza maarifa, weledi na ufanisi katika utendaji kazi; na
- (v) imewezesha jumla ya wafanyakazi 75 kwenda masomoni wakiwemo wanataaluma 71 (Wanaume 46 na Wanawake 25) na waendeshaji wanne (4) kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi.

### **Chuo cha Ufundi Arusha (ATC)**

**51. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali imeendelea kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ufundi, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo cha Ufundi Arusha imetekeleza yafuatayo:

- (i) imedahili jumla ya wanafunzi 1,129 wa mwaka wa kwanza ambapo ngazi ya Astashahada na Stashahada ni 911 na Shahada 218 (NTA Level 4-8);
- (ii) imeendelea na ukarabati wa nyumba 68 za watumishi zilizojengwa mwaka 1975 wakati chuo kinaanzishwa pamoja na ukarabati wa mabweni matatu yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800 kwa wakati mmoja ili kuboresha mazingira wanayoishi wafanyakazi na wanafunzi;
- (iii) imekamilisha ujenzi wa jengo la kufundishia matumizi ya nishati jadidifu ya umeme wa jua lenye uwezo wa kuchukua washiriki 20 na ufungaji wa mtambo wa uzalishaji wa Umeme wa jua wa kilowati moja, ambapo vijana 98 wameshapatiwa mafunzo juu ya matumizi ya nishati hiyo;
- (iv) imekamilisha ujenzi wa tanki kubwa la kuhifadhia maji lenye uwezo wa mita za ujazo 675 pamoja na nyumba ya pampu na mifereji ya umwagiliaji. Kukamilika kwa miundombinu hiyo

itaongeza ufanisi katika utoaji wa mafunzo kwa vitendo inayohusisha teknolojia za umwagiliaji na hivyo kuzalisha wataalamu wa umwagiliaji wenye uzoefu;

- (v) imekamilisha ujenzi wa miundombinu katika Kituo cha Mafunzo ya Nishati Jadidifu (*Renewable Energy*) cha Kikuletwa kwa asilimia 40. Mradi ukikamilika utaweza kuzalisha umeme wa kW 70 na utachangia katika uzalishaji wa wataalam wa umeme utokanao na nguvu za maji (Hydropower) wanaohitajika katika miradi ya uzalishaji umeme wa nguvu ya maji. Kazi zilizokamilika ni pamoja na:
  - (a) ujenzi wa barabara (access roads) zenye jumla ya urefu wa kilometa 4.3 kwa kiwango cha changarawe (gravel standards) na kuwezesha kituo kufikika kwa urahisi;
  - (b) ujenzi wa nyumba mbili (2) za kisasa zenye uwezo wa kuchukua familia nne (4) zitakazotumiwa na wataalam watakaokuwa wanafanya tafiti mbalimbali kuhusiana na nishati jadidifu; na
- (vi) imesanifu na kutekeleza mradi wa kufunga taa za kuongozea magari barabarani katika Jiji la Arusha kwa kushirikiana na ofisi ya TANROADS kwa lengo la kuongeza usalama kwa watumiaji wa barabara katika jiji hilo.

**52. *Mheshimiwa Spika*,** Chuo kimeendelea kutoa Ushauri wa Kitaalamu katika miradi ifuatayo:

- (i) usanifu na usimamizi wa miradi ya ujenzi katika Vyuo vya VETA (Kasulu, Ruangwa, Kongwa na Nyasa); Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ishirini (20) na Vyuo vya Ualimu tisa (9);
- (ii) upimaji wa udongo katika miradi ya Upanuzi wa Maji Safi na

Taka katika Jiji la Arusha; Upanuzi wa uwanja wa ndege wa Arusha, ujenzi wa ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, upanuzi wa Hospitali ya Wilaya ya Babati na ujenzi wa Bwawa la umwagiliaji Kivingo – Lushoto, Tanga; na

- (iii) upimaji lami katika miradi ya ukarabati wa barabara Bariadi – Slama A, Lamadi – Wigelekelo na Bariadi – Kisesa na upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Arusha.

### **Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**

**53. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere imetekeleza yafuatayo:

- (i) imedahili jumla ya wanafunzi 4,142 wakiwemo Astashahada 368, Stashahada 719 na Shahada 3,055;
- (ii) imefunga viti 326 visivyohamishika katika jengo jipya la mihadhara hivyo kuimarisha na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;
- (iii) imegharamia mafunzo kwa watumishi 10 wakiwemo Shahada ya Uzamivu saba (7) na Umahiri watatu (3) katika vyuo vya ndani; na
- (iv) imeendelea na ujenzi wa bweni la wanafunzi katika kampasi ya Zanzibar lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja kwa lengo la kuongeza udahili na kuboresha malazi kwa wanafunzi.

## **Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA)**

**54. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Serikali imetekeleza yafuatayo:

- (i) imedahili wanafunzi 302,626 katika kozi ndefu na fupi kwenye Mafunzo ya Ufundi Stadi. Kati yao wanafunzi wa kike ni 112,453 sawa na asilimia 37;
- (ii) imefanya upanuzi na ukarabati wa Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi 11 katika mikoa ya Pwani, Manyara, Lindi, Singida, Arusha, Mbeya, Mara, Mwanza pamoja na Halmashauri ya Karagwe, Makete na Kituo cha Dakawa;
- (iii) imefunga vifaa na mitambo ya kisasa kwenye karakana za Mtwara, *Morogoro Vocational Teacher Training Center (MVTTC)*, Kihonda, na Arusha kwa lengo la kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu na mafunzo ya Ufundi Stadi na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;
- (iv) imeendelea kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi kwa kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi 42 ambavyo vinajumuisha: Vyuo vipya vitatu (3) vya Mikoa ya Kagera, Geita, Rukwa; na kufanya upanuzi na ukarabati wa vyuo vya ufundi stadi kumi (10) ambavyo ni; Kitangali, Ileje, Nkasi, Ndolage, Kanadi, Samunge, Nyamidaho, Mabalanga, Gorowa, Simanjiro; pamoja na ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi vipya 29 vya Wilaya za Kongwa, Kasulu, Ruangwa, Nyasa, Chunya, Kilindi, Korogwe, Ukerewe, Butiama, Igunga, Pangani, Kishapu, Rufiji, Uyui, Kwimba, Bahi, Mafia, Longido, Nkinga, Uvinza, Ikungi, Isimani, Lushoto, Mbalali, Monduli, Buhigwe, Ulanga, Masasi na Butiama kwa utaratibu wa *Force Account*;

- (v) imeboresha karakana na kuweka zana za kisasa za kilimo katika Chuo cha Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) cha Arusha kwa lengo la kuimarisha mafunzo kwa vitendo na hivyo kuwaongezea wanafunzi stadi na uwezo wa kiutendaji;
- (vi) imeendelea kuongeza fursa kwa watoto wa kike kujiunga na mafunzo ya ufundi stadi kwa kujenga bweni la wasichana na nyumba ya mtumishi katika chuo cha Wilaya ya Makete;
- (vii) imeendelea kuongeza fursa za mafunzo ya ufundi stadi kwa kujenga Karakana za ufundi magari, bomba na uashi katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Lindi;
- (viii) imeboresha utoaji mafunzo kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa kuunganisha Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi 27 katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; na
- (ix) imefanikiwa kupata Hati Miliki za maeneo ya Vyuo vya Wilaya vya Ufundi Stadi vya Ukerewe, Ulanga, Chunya, Babati na Kwimba kwa lengo la kulinda maeneo hayo yasivamiwe na jamii inayozunguka.

### **Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**

**55. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi ili kuhakikisha kuwa vijana wengi wanapata Stadi, Ujuzi na Maarifa stahiki. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima imetekeleza yafuatayo:

- (i) imesajili jumla ya wanafunzi 3,062 (Wanaume 1,184 na Wanawake 1,878) wa Astashahada 99 (wanaume 22 na wanawake 77), Stashahada 2,867 (wanaume 1,121 na

Wanawake 1,746) na Shahada 96 (Wanaume 41 na wanawake 55);

- (ii) imesajili wanafunzi 13,036 wa sekondari wanaosoma Nje ya Mfumo Rasmi wakiwemo Wanaume 5,411 na Wanawake 7, 625;
- (iii) imeendelea kusimamia ubora katika uendeshaji wa Programu ya Elimu ya Sekondari Nje ya Mfumo Rasmi ambapo mitihani ya utamilifu ilifanyika katika mikoa 21 ya Tanzania Bara;
- (iv) imefanya mapitio ya mitaala ya programu tatu (3) za Usimamizi wa Elimu Masafa (*Management of Distance Education*) NTA level 4 - 8; Elimu ya Watu Wazima na Maendeleo ya Jamii (Adult Education and Community Development NTA level 4 - 8) na Usimamizi na Utawala wa Elimu ya Watu Wazima (Adult Education Management and Administration NTA level 4 - 8); na
- (v) imeboresha Mkakati wa Kuendeleza Kisomo na Elimu kwa Umma (National Literacy and Mass Education Strategy - NALMES) ili uendane na mahitaji ya sasa.

**56. *Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, Serikali kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima imekarabati madarasa mawili (2) na kuweka viti 173 katika kituo cha Luchelele Mwanza ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, imenunua vifaa kwa ajili ya kufanya mafunzo ya uongezaji thamani mazao ya samaki katika kituo cha Luchelele Mwanza.



## **Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya**

**57. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) imedahili jumla ya wanafunzi 5,738 (Wanawake: 1,182 na Wanaume: 4,556) kati ya wanafunzi hao Stashahada 2,680, Shahada 3,043, Shahada ya Umahiri ya Uhandisi Ujenzi 6, Stashahada ya Juu ya Elimu ya Ufundi 2 na Shahada ya Uzamivu ya Uhandisi Ujenzi 6;
- (ii) imeendelea na tafiti na bunifu zilizofadhiliwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) zinazohusu kutengeneza ndege inayoendeshwa bila rubani (*Drone*), 3D Printa pamoja na programu ya simu inayoonesha na kutoa maelezo ya maeneo na mitaa ambayo huduma za kijamii na kiuchumi zinatolewa;
- (iii) imeendelea na ujenzi wa maktaba itakayogharimu kiasi cha **Shilingi 5,523,685,496.00** yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja ambapo awamu ya kwanza ya ujenzi imekamilika na jengo limeanza kutumika hivyo kupunguza changamoto ya nafasi ya maktaba katika chuo;
- (iv) imefunga jumla ya taa 20 za kisasa zinazotumia nishati ya jua kuzunguka eneo la chuo, kampasi ya Mbeya na hivyo kuimarisha ulinzi na usalama pamoja na kupunguza gharama za nishati;
- (v) imetathmini eneo lenye hekta 511 kupitia Mamlaka ya Ardhi, Nyumba na Makazi ikishirikiana na ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya ikiwa ni hatua za kupanua eneo la chuo;
- (vi) imetathmini hekta 500 kuzunguka Kampasi ya Rukwa kupitia Mamlaka ya Ardhi, Nyumba na Makazi ikishirikiana na ofisi ya

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Sumbawanga kwa lengo la kuongeza ukubwa wa eneo la kampasi ya Rukwa;

- (vii) imekamilisha ujenzi wa madarasa mawili (2) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800 kwa wakati mmoja na hivyo kupunguza changamoto ya madarasa inayotokana na ongezeko la wanafunzi;
- (viii) imekamilisha michoro kwa ajili ya ujenzi wa jengo la vyumba viwili (2) vya mihadhara na vyumba vya madarasa vitatu (3) litakalokuwa na uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 800; na
- (ix) imekarabati ofisi 80 zilizo chini ya majengo ya chuo (basements offices) ili kuongeza nafasi za ofisi kwa wafanyakazi 320 pamoja na kufunga viti visivyohamishika katika madarasa matano (5) ili kuboresha mazingira ya kusomea kwa wanafunzi.

### **Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam**

**58. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam imetekeleza yafuatayo:

- (i) imedahili jumla ya wanafunzi 2,025 wakiwemo Stashahada 956, Shahada ya Kwanza 1,027 na Shahada ya Umahiri 42. Aidha, imeendelea kuhudumia wanafunzi 2,309 wanaondelea na masomo na kufanya Taasisi kuwa na jumla ya wanafunzi 4,334; na
- (ii) imefanya mashindano ndani ya Taasisi ya kuwatambua wanafunzi wabunifu 26 na kuwazawadia wanafunzi bora zaidi katika ubunifu. Aidha, bunifu zilizofikia hatua ya kuendelezwa kwa lengo la kubiasharishwa ni pamoja na uundaji wa gari aina ya "buggy" (Manufacturing of a buggy vehicle), teknolojia ya

ufuatiliaji wa ndege angani (Aircraft Tracking System) na mashine ya kutengenezea vitofali vya vitalu (Manufacture of a Concrete Paver Making Machine).

**59. *Mheshimiwa Spika*,** katika kutatua changamoto mbalimbali Taasisi imeendelea kutekeleza miradi saba (7) ya tafiti za kijamii ambayo ni:

- (i) kutengeneza mtambo maalumu wa kuwezesha mazingira rafiki ya kilimo mjini;
- (ii) kukamilisha utengenezaji wa mfumo wa kilimo cha umwagiliaji unaotumia nguvu za jua kwa kutumia maji ya kisima;
- (iii) kutengeneza mfumo wa kuhifadhi, kusambaza na kuchakata taarifa za bioanwai nchini;
- (iv) kuboresha teknolojia ya mfumo wa usimamizi wa hospitali na vituo vya afya ambao kwa sasa unatumika katika hospitali ya Amana kwa majaribio;
- (v) kutengeneza mfumo wa Mawasiliano yasiyotumia nyaya kwenye magari yasiyo na dereva;
- (vi) kukamilisha kusanifu na kutengeneza mashine ya kuchakata kahawa kwa kigezo cha rangi utakaosaidia wakulima wa kahawa kuongeza mnyororo wa thamani; na
- (vii) kutengeneza injini itakayotumia mfumo wa gesi asilia.

**60. *Mheshimiwa Spika*,** Taasisi imeendelea kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu kwa jamii ili kutatua changamoto za kijamii kwa kukamilisha miradi 12 na kuendeleza miradi 38. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:

- (i) kufanya upembuzi yakinifu na usimamizi wa ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu mbalimbali katika Vyuo 12 vya

Maendeleo ya Wananchi (FDCs) katika mikoa ya Morogoro, Mtwara, Lindi, Pwani, na Rufiji;

- (ii) kutoa ushauri wa kitaalamu wa kuandaa mkakati wa kuboresha mawasiliano wa kitaifa (National Broadband Strategy) chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano;
- (iii) kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa jengo la kufanyia matengenezo ya ndege katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius K. Nyerere; na
- (iv) kupima ubora wa vifaa vya ujenzi katika miradi miwili mikubwa ya kimkakati ambayo ni mradi wa kufua umeme wa maji (Julius Nyerere Hydropower Project) na mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (Standard Gauge Railway).

**61. *Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, Taasisi imejenga, imekarabati na kufanya upanuzi wa majengo katika kampasi zake tatu kama ifuatavyo:

- (i) upanuzi wa jengo la maktaba (Vertical Extension of DIT Library) pamoja na kuweka samani na miundombinu ya TEHAMA katika Kampasi Kuu ya Dar es Salaam na hivyo kuongeza uwezo wa matumizi ya Maktaba kutoka wanafunzi 150 hadi 450 kwa wakati mmoja;
- (ii) ukarabati wa miundombinu ya Kampasi ya Mwanza ikiwemo maabara na ununuzi wa mashine ya kuchakata na kutengeneza bidhaa za ngozi kupitia mradi wa "Skills Development Fund (SDF)" kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA);
- (iii) ujenzi wa jengo la maabara ya Kompyuta, darasa na bwalo la chakula katika Kampasi ya Myunga iliyopo mkoani Songwe;

- (iv) imeendelea kupitia na kuboresha Mitaala 14 kwa ngazi za Stashahada, Shahada na Shahada ya Umahiri ambapo mitaala nane (8) ni maalumu kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la ajira Kitaifa na kikanda katika fani ya TEHAMA na teknolojia za ngozi;
- (v) imepata ithibati ya mtaala wa Shahada ya Kwanza ya Uhandisi Madini na ya Umahiri wa Uhandisi katika Nishati Endelevu ambapo wanafunzi 59 wa Shahada ya Kwanza ya Uhandisi Madini na wanafunzi 9 wa Shahada ya Umahiri wa Nishati Endelevu wamedahiliwa; na
- (vi) imeanza utekelezaji wa mradi wa maendeleo wa miaka mitano ujulikanao kama "*East Africa for Transformation and Regional Integration Project – EASTRIP*". Mradi huu una lengo la kuanzisha vituo vya umahiri vya kikanda katika fani za TEHAMA na teknolojia ya uzalishaji wa bidhaa za ngozi kwa ufadhili wa Benki ya Dunia ambao ulitekeleza kazi zifuatavyo:
  - (a) kuwajengea uwezo wasimamizi na watekelezaji wa mradi;
  - (b) kuratibu ujenzi wa mabweni manne (4) ya wanafunzi na majengo mawili (2) ya vituo vya umahiri katika kampasi za Mwanza na Dar es Salaam;
  - (c) kuandaa miongozo ya utekelezaji wa mradi; na
  - (d) kuratibu ununuzi wa magari manne (4) ya mradi.

**62. *Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imeendelea kutekeleza miradi mikubwa mitatu (3) ya kubiasharisha bunifu ambayo ni: ufungaji wa taa za barabarani katika eneo la daraja la Ruvu mkoani Pwani; ufungaji wa taa za kuvukia waenda kwa miguu mkoani Manyara na kuhuisha mfumo wa miito ya huduma kwa wateja (call center) wa TANESCO. Aidha, imeandaa maandiko manne (4) ya miradi ya utafiti kwa ajili ya kupata

fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi. Miradi hiyo ni pamoja na:

- (i) Elimu ya Nishati Jadidifu (Education for Renewable Energy Technology Center);
- (ii) Uendelezaji vipaji vya uvumbuzi katika mafunzo ya uhandisi (Leading Invention in Engineering Education);
- (iii) Uboreshwaji wa uongozi wa elimu ya juu katika Bara la Afrika (African Higher Education Leadership in Advocacy (AHEAD)); na
- (iv) Uandaaji wa Kanzidata ya vifaa vya utafiti katika taasisi za elimu ya juu na utafiti (Development of Equipment catalogue of higher learning and Research and Development institutions).

### **Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha (NM-AIST)**

**63. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha imetekeleza yafuatayo:

- (i) Imeongeza udahili kutoka wanafunzi 116 hadi 602 sawa na ongezeko la asilimia 24;
- (ii) imeandaa sera mbalimbali za chuo ikiwa ni pamoja na Sera ya Utafutaji Rasilimali na Uwekezaji, Sera ya Utafiti na Ubunifu na Sera ya Hatimiliki kwa lengo la kuboresha utendaji wa Taasisi na ukusanyaji maduhuli; na
- (iii) imeendelea na utekelezaji wa miradi ya utafiti katika kilimo, maji, TEHAMA na usalama wa chakula kama vile uzalishaji wa miche bora ya ndizi inayohimili magonjwa ya kitropiki na kuondoa sumu kuvu katika nafaka na kudhibiti maambukizi ya ugonjwa wa kimeta kwa wanyama pori na wanaofugwa.

**64. *Mheshimiwa Spika*,** Taasisi imetekeleza tafiti na bunifu mbalimbali ambapo baadhi ya tafiti zimeonesha matokeo chanya kwa kuja na teknolojia mbalimbali zinazoweza kutumika katika maendeleo ya viwanda nchini ambazo ni:

- (i) kanuni ya madawa asilia yatokanayo na magome ya miti yanayoweza kutumika katika uchakataji wa ngozi ili kuengeneza bidhaa mbalimbali (kama vile viatu, mikamba na mikoba);
- (ii) kiuatilifu cha kumdhibiti mdudu maarufu kwa jina la kanitangaze '*Tuta absoluta*' ambaye hushambulia nyanya na mahindi shambani; na
- (iii) kanuni ya utengenezaji wa unga lishe '*Nutritional formulation*' ili kutatua changamoto za utapiamlo kwa mama na mtoto.

### **Tathmini ya Utoaji wa Elimu na Mafunzo**

**65. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuhakikisha elimu yetu inaendana na mahitaji ya mipango ya nchi yetu na soko la ndani, kikanda na kimataifa, Serikali imeendelea kuziwezesha taasisi zetu zenye majukumu ya kutathmini ubora na utoaji wa elimu kama ifuatavyo.

### **Baraza la Mitihani la Tanzania - NECTA**

**66. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Baraza la Mitihani la Tanzania imetekeleza yafuatayo:

- (i) imekamilisha Uchapaji, Usafirishaji na Usahihishaji wa mitihani ya Kitaifa ya Darasa la Nne ambapo jumla ya watahiniwa 1,667,552 walifanya upimaji kati ya watahiniwa 1,787,034 waliokuwa

wamesajiliwa; Kidato cha Pili ulijumuisha Watahiniwa 571,670 kati ya 609,386 waliokuwa wamesajiliwa na Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) ulikuwa na jumla ya Watahiniwa 933,369 kati ya 947,077 waliokuwa wamesajiliwa. Aidha, Mitihani ya Kidato cha Nne (CSEE) na Maarifa (QT) ilifanyika ambapo jumla ya Watahiniwa 473,724 wa Kidato cha Nne walifanya mtihani kati ya 485,737 waliokuwa wamesajiliwa na jumla ya Watahiniwa 11,985 walifanya Mtihani wa Maarifa (QT) kati ya 12,985 waliokuwa wamesajiliwa;

- (ii) imekamilisha Usajili wa Watahiniwa wa Kidato cha Sita (ACSEE) 2020 ambapo jumla ya Watahiniwa 85,525 wamesajiliwa;
- (iii) imekamilisha usajili wa Watahiniwa wa Mtihani wa Ualimu kwa mwaka 2020 ambapo jumla ya Watahiniwa 8,574 wamesajiliwa kufanya Mtihani huo; na
- (iv) imekamilisha Upimaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa Sampuli ya wanafunzi 33,313 wa Darasa la Pili (2019) uliofanyika tarehe 28 hadi 29 Januari, 2020.

### **Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania - TCU**

**67. *Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Tume ya Vyuo Vikuu imetekeleza yafuatayo:

- (i) imeratibu maombi 99,014 (Wanaume 57,328 na Wanawake 41,686) ya wanafunzi walioomba kujiunga na masomo ya Shahada ya kwanza kwa mwaka wa masomo 2019/20. Kati ya maombi hayo, waombaji 87,813 wamedahiliwa katika vyuo mbalimbali vya Elimu ya Juu hapa nchini;
- (ii) imepokea maombi 457 ya waombaji wanaotaka kwenda kusoma



nje ya nchi ambapo maombi 393 yaliidhinishwa na maombi 64 yalikataliwa kwa kutokidhi vigezo;

- (iii) imeandaa Mwongozo wa waombaji wanaotaka kwenda kusoma nje ya nchi ili kuhakikisha wanafunzi kutoka Tanzania wanaenda kusoma vyuo vinavyotambulika. Aidha, imefanya ukaguzi wa Taasisi saba (7) zinazoshughulikia usajili na upelekaji wanafunzi kusoma nje ya nchi kwa lengo la kuzisajili;
- (iv) imeratibu programu mbalimbali za kuwajengea uelewa wanaotaka kujiunga na Elimu ya Juu nchini kupitia vyombo vya habari na kambi za Jeshi la Kujenga Taifa Tanzania Bara na Visiwani ambapo jumla ya Vijana 19,196 walifikiwa;
- (v) imetoa ithibati ya Chuo cha Tumaini Ndaki ya Dar es Salaam (TUDARCo) na ithibati 170 za Programu kati ya hizo 93 ni mpya na 77 zilipitiwa upya na kuridhiwa;
- (vi) imetathmini na kutambua tuzo 1,502 zilizotolewa katika Vyuo vya Elimu ya Juu nje ya nchi;
- (vii) imefanya ufuatiliaji wa masuala ya ubora katika vyuo vikuu nane (8) ili kijiridhisha kama vinafuata miongozo ya Tume;
- (viii) imeratibu mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi watatu (3) wanaoendelea na masomo ya Shahada za Umahiri na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 26 kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa watumishi;
- (ix) imeratibu mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 604 wa taasisi nufaika wa mradi wa Kukuza Ujuzi na Stadi za Kazi (ESPJ) kwa ajili ya kuwaongezea ujuzi wa uzalishaji kwenye sekta sita za kipaumbele (Kilimo Biashara, Utalii na Ukarimu, Ujenzi, Uchukuzi, Nishati na TEHAMA). Aidha, mafunzo haya yalihusu Usimamizi wa Programu mbalimbali katika Taasisi, Utunzaji Kumbukumbu,

Mfumo wa Bajeti na Masuala yahasuyo Ukaguzi kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa watumishi;

- (x) imechapisha kitabu kinachoeleza "Hali ya Elimu ya Juu nchini, 2018" ili kutoa taarifa mbalimbali kuhusu vyuo, wanafunzi na watumishi wa vyuo vya Elimu ya Juu;
- (xi) imeendelea kufanya maboresho ya mfumo wa kukusanya taarifa uitwao *University Information Management System - UIMS* ambapo Bodi za Mikopo za Wanafunzi wa Elimu ya Juu Tanzania Bara na Visiwani ziliunganishwa ili kurahisisha utoaji wa taarifa mbalimbali za Taasisi za Elimu ya Juu nchini;
- (xii) imeratibu maonesho ya 14 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ili kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu mambo mbalimbali yahasuyo elimu ya juu ambapo jumla ya taasisi 84 za ndani na nje ya nchi zilishiriki; na
- (xiii) imeshiriki kwenye mikutano kuhusu masuala ya uthibiti ubora katika Elimu ya Juu iliyoratibiwa na Umoja wa Afrika na IUCEA.

### **Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE)**

**68. *Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha usimamizi wa elimu ya ufundi, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi kwa mwaka wa fedha 2019/20 imetekeleza yafuatayo:

- (i) imefanya ufuatiliaji na tathmini ya ubora wa elimu na mafunzo yanayotolewa katika vyuo vya ufundi 109 ambapo vyuo 103 vilipatiwa ushauri kuhusu namna ya kuboresha utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo, Vyuo viwili (2) vilifutiwa usajili, na vyuo vinne (4) vilizuiliwa kudahili wanafunzi ili kuvipa nafasi ya kurekebisha mapungufu yaliyobainika;

- (ii) imesajili vyo 24 katika bodi za masomo katika fani zifuatazo:- Afya na Sayansi Shirikishi - 12, Biashara, Utalii na Mipango - 9, Sayansi na Teknolojia Shirikishi - 2 na Elimu na Uwezeshaji wa Kujifunza – 1;
- (iii) imehakiki Mitaala 65 iliyokuzwa na vyo vya ufundi, imeidhinisha programu 7 na kukagua vyo 17 ili kuhakikisha elimu na mafunzo yanayotolewa yanalingana na vigezo vilivyowekwa na Baraza;
- (iv) imeratibu na kuhakiki udahili wa Wanafunzi 151,969 (Wanaume 81,523 na Wanawake 70,446) katika ngazi ya Astashahada ya Awali, Astashahada na Stashahada katika fani za Sayansi na Teknolojia Shirikishi; Afya na Sayansi Shirikishi; Biashara, Utalii na Mipango; na Uwezeshaji wa Ufundishaji na Kujifunza;
- (v) imefanya tathmini ya vyeti vya wahitimu 16,549 vilivyopokelewa kwa ajili ya kutoa namba ya uthibitisho (*Award Verification Number - AVN*) ili kudhibiti uendeshaji wa mafunzo bila kufuata kanuni na sheria zilizowekwa na Baraza. Aidha, utoaji wa AVN umesaidia kuepusha udanganyifu wa wahitimu wanaoendelea na elimu ya juu;
- (vi) imetoa mafunzo kuhusu Mitaala inayozingatia Umahiri kwa wakufunzi 608 wa Vyo vya Elimu ya Ufundi yatakayosaidia wahitimu kuwa mahiri katika ujuzi uliokusudiwa;
- (vii) imetoa ithibati kwa vyo 19 katika bodi za masomo zifuatazo: Afya na Sayansi Shirikishi vyo 11, Biashara, Utalii na Mipango vyo vinne (4) na Sayansi na Teknolojia Shirikishi vyo vinne (4);
- (viii) imefanya utafiti katika sekta 6 ambazo ni *Construction, Agribusiness and Agroprocessing, Energy, Tourism and Hospitality, Transport and Logistics* na *ICT* kwa lengo la kubaini

pengo la ujuzi lililopo ili kuviwezesha vyuo na taasisi kutoa elimu na mafunzo yanayoendana na mahitaji ya soko la ajira; na

- (ix) imeunganisha mifumo ya udahili na mitihani ili kuwezesha kuwasiliana na mifumo ya vyuo 32 vya elimu ya ufundi iliyotengenezwa kwa lugha mbalimbali (Coding Language) ambayo itarahisisha mawasiliano kati ya Baraza na vyuo.

### **Uwezeshaji wa Utoaji wa Elimu na Mafunzo**

- 69. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuhakikisha elimu yetu inatolewa kwa ufanisi na tija, Serikali imeendelea kuwezesha Taasisi zenye majukumu ya kuwezesha mifumo ya elimu na ujifunzaji kuhakikisha unafanyika katika mazingira yenye kuleta tija na ufanisi na kuhakikisha na vitabu vyenye kufaa katika shule zetu. Taasisi hizo zimetetekeleza yafuatayo.

### **Taasisi ya Elimu Tanzania (TET)**

- 70. *Mheshimiwa Spika*,** kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Taasisi ya Elimu Tanzania imetekeleza yafuatayo:
  - (i) imekamilisha kazi ya uandishi, kuchapa na kusambaza aina nane (8) za vitabu vya kiada vya Darasa la VI kwa masomo ya Kiswahili, Hisabati, English, Uraia na Maadili, Maarifa ya Jamii, Stadi za Kazi, Sayansi na Teknolojia na Kifaransa kwa kuzingatia mtaala wa mwaka 2015 unaolenga umahiri. Jumla ya nakala 2,962,155 zimesambazwa katika Halmashauri za Mikoa 26 ya Tanzania Bara kwa uwiano wa 1:3;
  - (ii) imeandaa na kusambaza nakala 272,000 za Kiongozi cha Mwalimu kwa masomo yote nane (8) kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ufundishaji wa masomo husika;
  - (iii) imechapa na kusambaza nakala za vitabu 1,359,350 vya masomo

yote kwa ngazi ya Elimu ya Awali na Msingi Darasa la I-V kwa matumizi ya shule zinazotumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia yaani *English Medium Schools* na hivyo kuondoa changamoto ya upatikanaji wa vitabu kwa shule zinazotumia lugha ya Kiingereza;

- (iv) imekamilisha uandishi wa vitabu vya kiada kwa Darasa la VI kwa shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia. Vitabu hivyo vinapatikana katika maktaba mtandao na nakala ngumu ipo katika hatua ya uchapaji;
- (v) imechapa na kusambaza katika Halmashauri zote nakala 440,000 za kitabu cha kiongozi cha mwalimu kwa Darasa la I na II nchini ili kumwezesha Mwalimu kuutekeleza mtaala wa Darasa la I na II kwa ufanisi zaidi;
- (vi) imechapa na kusambaza nakala 719,905 za vitabu vya kiada vya Elimu ya Awali na kufikia uwiano wa 1:3 pamoja na nakala 41,642 za Mwongozo wa Mwalimu wa kufundishia Elimu ya awali;
- (vii) imekamilisha kazi ya uandishi, kuchapa na kusambaza aina 15 ya vitabu vya kiada kwa masomo ya Historia na Jiografia ngazi ya Sekondari (O-level), pamoja na masomo ya Sayansi (Biology, Chemistry, Physics na Basic Mathematics) na Kiswahili kidato cha 5 na 6 ili kurahisisha upatikanaji wa vitabu. Jumla ya nakala 1,567,537 zimesambazwa kwa (uwiano wa 1:3) katika Halmashauri za Mikoa 26 ya Tanzania Bara;
- (viii) imechapa na kusambaza vitabu vya kiada vya maandishi yaliyokuzwa kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu. Jumla ya nakala 8,750 za vitabu hivi zimegawanywa katika Halmashauri zote zenye wanafunzi wenye uoni hafifu kwa uwiano wa 1:1;

- (ix) imeandika, kuchapa na kusambaza vitabu vya kiada vya nukta nundu (Braille) aina 18 kwa Darasa la I, II, na V kwa ajili ya wanafunzi wasioona. Jumla ya nakala 11,402 za vitabu vya nukta nundu (braille) na Mchoro mguso (embossed drawing) vimesambazwa kwa uwiano 1:1 katika shule zote zenye wanafunzi wasioona Tanzania Bara;
- (x) imechapa katika maandishi ya nukta nundu (braille) na kusambaza nakala 200 za Mtaala wa Darasa la I – VII katika shule zote zenye wanafunzi wasioona Tanzania Bara;
- (xi) imefanya tathmini ya machapisho 80 ya kielekroniki yaliyopokelewa ambapo machapisho 11 yalipewa ithibati yakiwa na maboresho madogo, 38 yalikuwa na maboresho makubwa na machapisho 31 yalikataliwa;
- (xii) imeandaa na kusambaza aina 47 za vitabu vya ziada vya nukta nundu kwa ajili ya masomo ya sekondari kwa kushirikiana na Shirika la *Siloam International for Blind*. Jumla ya nakala 5,100 zimesambazwa katika shule zote zenye wanafunzi wasioona Tanzania Bara na Visiwani;
- (xiii) inaendelea kufanya mapitio ya Mtaala wa Elimu ya Ualimu kupitia **Mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu** ili uendane na mtaala wa Elimu ya msingi na mahitaji ya sasa;
- (xiv) inaendelea kuimarisha upatikanaji wa vitabu kupitia huduma ya maktaba mtandao (TIE- online library) ambapo wanafunzi wanapata vitabu vya kiada, ziada, na machapisho mengine ya TET kwa ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na vyuo vya Ualimu. Maktaba hii inawawezesha wanafunzi kujisomea na hivyo kuimarisha utamaduni wa kujisomea.

**71. *Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania imeendelea kuandaa na kusambaza miongozo na mihtasari mbalimbali yenye lengo la kuimarisha ufundishaji wa wanafunzi kwa kuzingatia vitabu vinavyotolewa na taasisi kama yafuatayo:

- (i) imeandaa Mwongozo wa Mwalimu Mshauri wa Darasa la Elimu ya Awali, Darasa la I na II ambao utatumika kutoa mafunzo kwa walimu kazini
- (ii) imeandaa miongozo mitano (5) ya kufundishia na kujifunzia kwa kutumia mbinu ya michezo kwa Darasa I – IV itakayosaidia kuboresha ufundishaji na ujifunzaji na kuibua udadisi wa wanafunzi;
- (iii) imeandaa mwongozo wa kutekeleza mtaala wa Elimu ya Sekondari unaozingatia mahitaji ya wanafunzi viziwi na kusanifisha Lugha ya Alama nchini ili kuboresha ufundishaji kwa wanafunzi hao;
- (iv) imeandaa mwongozo wa mafunzo ya Lugha ya Alama ili kuwawezesha wakufunzi kutekeleza Mtaala wa Astashahada ya Ualimu wa Elimu Maalum; na
- (v) imetafsiri mtaala na mihtasari ya Astashahada ya Ualimu kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza ili kuwezesha vyuo vya Serikali na vyuo binafsi kuandaa walimu wa ngazi ya Astashahada wenye uwezo wa kufundisha shule za msingi kwa kutumia lugha ya Kiingereza.

**72. *Mheshimiwa Spika***, uboreshaji wa mitaala ni moja ya majukumu ya Taasisi ya Elimu Tanzania wenye lengo la kuhakikisha nchi inakuwa na mitaala yenye kuwanda vijana wetu kuendana na mahitaji ya mipango ya nchi, kikanda na kimataifa. Utekelezaji wa jukumu hili unahusisha

pia uelimishaji wa watumiaji wa mitaala husika ili waweze kuzingatia maboresho wakati wa utoaji wa elimu. Katika kufikia azma hiyo, Serikali kupitia Taasisi imetekeleza yafuatayo:

- (i) imeendesha mafunzo kwa wathibiti ubora, Maafisa Elimu na Maafisa Elimu Kata kuhusu mtaala ili kuwawezesha kufuatilia utekelezaji wa mtaala shuleni na vyuoni;
- (ii) imetoa mafunzo kabilishi kwa walimu 592 wa Shule Zisizo za Serikali, kwa ngazi ya Elimu ya Awali na Msingi yaliyolenga kuwawezesha kutekeleza kwa ufanisi mtaala ulioboreshwa; na
- (iii) imetoa mafunzo kwa walimu 431 wa Shule Zisizo za Serikali kwa ngazi ya Elimu ya Sekondari ambayo yatawawezesha walimu kutekeleza mtaala unaozingatia ujenzi wa umahiri kwa ufanisi.

### **Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)**

**73. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania imetekeleza Miradi ifuatayo:

- (i) inaendelea na ujenzi wa vyumba vya madarasa 81 (madarasa matatu (3) kwa kila shule) katika shule za msingi 22 na shule za sekondari tano (5) zenye uhitaji mkubwa. Aidha, inajenga mabweni 16 ya wasichana katika shule 16 za sekondari (kidato cha 5 na 6) zilizo katika mazingira hatarishi;
- (ii) inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba 40 za walimu; (Nyumba 4 kwa kila shule) katika shule za sekondari 10;
- (iii) inajenga mabweni matatu (3) katika shule 3 za msingi na ujenzi wa vyumba viwili (2) vya madarasa, chumba maalum (Audiology room); na
- (iv) inaendelea na ujenzi wa matundu ya vyoo 528 (matundu 24 kwa



kila shule) katika shule za msingi 18 na shule za sekondari nne (4) zenye uhitaji mkubwa.

### **Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM)**

**74. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa Taasisi za Elimu nchini, Serikali kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu imetekeleza yafuatayo:

- (i) imesajili walimu 2,806 kati ya walimu 2,521 waliopangwa kusajiliwa, sawa na ongezeko la asilimia 11, katika kozi za Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu (DEMA), Stashahada ya Uthibiti Ubora wa Shule (DSI), na Astashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu (CELMA). Lengo ni kuwajengea uwezo wa kuthibiti utoaji wa elimu bora shuleni, kuongoza na kusimamia rasilimali katika taasisi za elimu, hususan shule za msingi na sekondari;
- (ii) imetoa Mafunzo kwa Wakuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54 yaliyolenga kuboresha utendaji katika kuongoza, kusimamia na kuendesha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi;
- (iii) imetoa mafunzo ya Uongozi na Usimamizi wa Taaluma (Pedagogical Leadership) **kupitia mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu** kwa wajumbe 245 wa Menejimenti za Vyuo kutoka vyuo vya Ualimu 35 kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuongoza na kusimamia utoaji wa elimu bora kwa Wanachuo tarajali;
- (iv) imetoa mafunzo kwa Maafisa Elimu ngazi ya Mkoa na Wilaya (Sekondari na Msingi) 383 ambayo yalilenga kuwapatia uwezo wa kuongoza, kupanga, kusimamia na kufanya tathmini ya

shughuli za elimu katika maeneo yao ya kazi;

- (v) imetoa mafunzo kwa Wakuu wa Shule za Sekondari pamoja na Maafisa Elimu Kata 985 kutoka Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Mwanza, Geita na Kilimanjaro kwa lengo la kuwapatia uwezo wa kuongoza, kupanga, kusimamia na kufanya tathmini ya shughuli za elimu katika maeneo yao ya kazi;
- (vi) imetoa mafunzo ya Uongozi na Usimamizi wa Shule kwa Wakuu Shule 89 za Sekondari zilizo chini ya madhehebu ya Kikristo (CSSC) kutoka mkoa wa Arusha, Kilimanjaro na Manyara pamoja na Wakuu wa Shule 20 kutoka shule zinazomilikiwa na BAKWATA kwa lengo la kuwapatia uwezo wa kuongoza, kusimamia na kufanya ufuatiliaji wa shughuli za utoaji elimu katika ngazi ya shule;
- (vii) imetoa mafunzo kwa wawezeshaji wa kitaifa 74 (Trainer of Trainers) kwa lengo la kuwapatia uwezo wa kuwezesha Wajumbe wa Kamati za Shule za Msingi katika mikoa minne (4) ya Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe kwa ajili ya kusimamia utoaji wa elimu kwa shule za msingi;
- (viii) imetoa mafunzo kuhusu Kupambana na Rushwa, Kujikinga na Maambukizi ya UKIMWI na elimu kuhusu kuzuia Majanga kwa watumishi 67 na Wanachuo 2,324 katika Kampasi za Bagamoyo, Mbeya na Mwanza;
- (ix) imeandaa moduli ya uendeshaji mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati za Shule za Msingi pamoja na Mpango wa Jumla wa Maendeleo ya Shule kwa lengo la kutoa mwongozo wa utoaji wa elimu bora ngazi ya shule; na
- (x) imeimarisha mazingira ya kufundishia, kujifunzia na mazingira ya

utendaji kazi kwa watumishi katika Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu - ADEM kwa kukarabati nyumba nne (4) za watumishi, ofisi tatu (3) na madarasa manne (4).

### **Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

**75. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imetekeleza yafuatayo:

- (i) imetoa mikopo kwa wanafunzi 132,119 hadi kufikia Machi, 2020 wakiwemo 49,799 wa mwaka wa kwanza na 82,320 wanaoendelea na masomo ili kutoa fursa ya wahitaji wa Elimu ya Juu;
- (ii) imefanya ukaguzi kwa waajiri 2,406 nchi nzima na kutambua wanufaika wapya 14,731 wenye mikopo iliyoiva yenye thamani ya Shilingi Bilioni 100.7 ambapo kati yao wanufaika 13,969 (94%) wameanza kulipa. Aidha, hadi kufikia Disemba, 2019 idadi ya wanufaika wanaorejesha mikopo ilikuwa imefikia 176,952 kati ya 184,166 waliotarajiwa sawa na asilimia 96 ya lengo;
- (iii) imetoa jumla ya mikopo yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 449.99** kwa wanafunzi 132,119 kati ya **Shilingi bilioni 450** iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2019/20 sawa na asilimia **99**.
- (iv) imeendelea na ukusanyaji wa mikopo iliyoiva ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 144.3** kati ya **Shilingi bilioni 166.1** zilizolengwa katika kipindi cha mwezi Juni 2019 hadi Machi 2020 sawa na asilimia 86.9 zimekusanywa. Lengo la makusanyo kwa mwaka ni **Shilingi bilioni 221.5**;

- (v) imefungua ofisi ya Kanda katika Mkoa wa Mtwara na kufikisha jumla ya ofisi sita (6) za Kanda ambazo ziko katika mikoa ya Dodoma, Mwanza, Arusha, Mtwara, Mbeya na Zanzibar ili kusogeza huduma za mikopo ya Elimu ya Juu karibu na wananchi pamoja na kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mikopo iliyoiva;
- (vi) imeendelea kuboresha mifumo ya uendeshaji ili kuongeza uwazi na ufanisi wa utoaji huduma katika upangaji, utoaji na ukusanyaji wa mikopo iliyoiva. Aidha, mifumo imeboreshwa na kumuwezesha mwanafunzi kupata taarifa za mkopo wake kupitia simu ya mkononi au mtandaoni (Student's Individual Permanent Account – SIPA) na kuondoa usumbufu wa wanafunzi kufuatilia taarifa hizo kwenye ofisi za Bodi; na
- (vii) imebuni mfumo unaoviwezesha vyo kuambatisha nyaraka muhimu kama vile matokeo ya mitihani kupitia mtandao badala ya kutuma nakala ngumu. Vilevile, uboreshaji wa mifumo umehusisha uunganishaji wa mifumo ya TEHAMA ya Bodi ya Mikopo na ya Tume ya Vyuo Vikuu ambapo taarifa za udahili za waombaji wa mikopo zinapatikana kwa urahisi na kwa wakati.

**76. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuiwezesha jamii kupata taarifa za huduma zinazotolewa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Serikali imeendelea na kampeni za uelimishaji kuhusu mikopo kama ifuatavyo:

- (i) imeendesha programu za elimu katika shule na kambi 17 za Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu sifa, vigezo na taratibu za uombaji wa mikopo kwa wanafunzi waliomaliza masomo ya kidato cha sita (6) na kujiandaa kujiunga na taasisi za Elimu ya Juu; na
- (ii) imeandaa na kuendesha vipindi 30 vya Redio na Televisheni kuhusu umuhimu wa kurejesha mkopo wa Elimu ya Juu ambapo

waajiri, wanufaika na wanafunzi walipata fursa ya kuuliza maswali na kujibiwa.

### **Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (BOHUMATA)**

**77. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba imetekeleza yafuatayo:

- (i) imedahili jumla ya wanafunzi 551 katika Chuo cha Ukutubi, Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu (*School of Library Achieves and Documentation Studies - SLADS*) ili kuongeza upatikanaji wa wataalamu Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka nchini; na
- (ii) imewezesha upatikanaji wa jumla ya vitabu 310,490 ambapo vitabu 1,673 vilipatikana kwa mujibu wa sheria, vitabu 308,801 vilipatikana kwa msaada na vitabu 16 kwa fedha za Matumizi Mengineyo. Aidha, jumla ya magazeti na majarida 4,906 yalipatikana (magazeti 4,788 na majarida 118). Upatikanaji wa vitabu, magazeti na majarida hayo vimeongeza fursa kwa wasomaji katika maktaba za Mikoa 22, Wilaya 19 na Tarafa 2.

### **Uendelezaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**

#### **Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)**

**78. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia imetekeleza yafuatayo:

- (i) imebaini mahitaji ya ubunifu na namna ya kujenga uwezo kwa wabunifu 60 wa MAKISATU na kuwapatia mafunzo katika nyanja

za ulinzi miliki bunifu, ujasiriamali, ubiasharishaji na usimamizi wa mikataba;

- (ii) imeandaa siku maalum ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ambapo watafiti, wabunifu, wawekezaji, watunga sera na wananchi 207 walikutanishwa na kujadili namna ya ukuzaji na uendelezaji wa bidhaa za wabunifu kibiashara;
- (iii) imeendesha kongamano la ubunifu lijulikanalo kama *AfricaLICS* lililofanyika Novemba, 2019 ambapo washiriki 300 kutoka nchi mbalimbali ulimwenguni walihudhuria. Kongamano hilo lililenga kutoa elimu kuhusu masuala ya ubunifu;
- (iv) imeshiriki katika maonesho na mikutano mbalimbali ambapo kazi za wabunifu na watafiti zilioneshwa na kusambazwa kama ifuatavyo:
  - (a) Watafiti na wabunifu 26 walionesha kazi zao na wananchi 576 walitembelea banda katika viwanja vya maonesho ya Sabasaba - Dar es Salaam;
  - (b) imetoa elimu kuhusu *biotechnology and biosafety* na kupokea maoni kutoka kwa washiriki 800 wakijumuisha Wakulima, Watafiti, NGOs na Wananchi katika maonesho ya Nanenane katika mikoa ya Dodoma, Simiyu na Morogoro;
  - (c) imetoa elimu kuhusu majukumu ya Tume kwa wageni 456 waliotembelea banda la Tume katika maonesho ya vyuo vikuu (Wageni 300) na maonesho ya nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (Wageni 156); na
  - (d) imetoa mafunzo kwa Washiriki 230 kutoka nchi 29 ulimwenguni kuhusu masuala ya utafiti na matumizi ya ushahidi wa kisayansi katika kutunga sera na kutoa maamuzi kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.

Mafunzo hayo yalitolewa katika mkutano wa Mabaraza uliofanyika Novemba, 2019 uliokuwa na kaulimbiu "Sayansi Wazi na Shirikishi katika Utafiti na Ubunifu kwa Maendeleo."

- (v) imeelimisha na kuhamasisha matumizi ya tafiti, sayansi, teknolojia na bunifu kwa umma wa watanzania kwa kuandaa na kusambaza machapisho ya tafiti na bunifu yakiwemo *promotional materials* 2,000, mabango 8, vijitabu 500 na vipeperushi maalum 1,000. Aidha, ilifadhili makala za magazeti 212, vipindi 211 vya redio na runinga, Makala maalum (*documentary*) tatu (3) na vipindi mubashara vinne (4) vya runinga na redio kwa lengo la kuelimisha jamii kuhusu matumizi ya tafiti, sayansi, teknolojia na ubunifu;
- (vi) imeendelea kugharamia uanzishaji wa Kituo cha Teknolojia cha mfano *pilot technology station* kwa ajili ya uhawilishaji wa teknolojia kupitia uwekezaji wa nje;
- (vii) imeratibu na kufadhili zoezi la kuwapata na kuwawezesha wabunifu wawili (2) kushiriki katika mashindano ya kimataifa ya ubunifu (SLUSH 2019) yaliyofanyika nchini Finland;
- (viii) imeboresha mfumo wa udhibiti na utoaji vibali vya utafiti nchini na kuwezesha kusajili na kutoa jumla ya vibali vya utafiti 449 kati ya maombi 580 ikilinganishwa na vibali 406 vilivyotolewa mwaka wa fedha 2018/2019;
- (ix) imetathmini na kufanya ufuatiliaji wa miradi 12 ya utafiti na ubunifu (kutoka watafiti wa nje wakishirikiana na watafiti wazawa) iliyopewa vibali vya utafiti kutoka COSTECH ili kujiridhisha na utekelezaji wa taratibu za vibali na misingi ya ushirikiano wa utafiti kwa maendeleo na kuainisha mapungufu

yaliyoshughulikiwa; na

- (x) imeendesha Mikutano minne (4) na wadau muhimu wa utafiti nchini ambao ni Vyuho Vikuu, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Taasisi za utafiti na OR - TAMISEMI na kuweka mikakati ya pamoja ya utaratibu wa kieletroniki inayounganisha taasisi za utafiti na waratibu wa tafiti nchini.

### **Tume ya Nguvu za Atomiki (TAEC)**

**79. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2019/20, Serikali kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki imetekeleza yafuatayo:

- (i) imepokea na kutathmini maombi 469 ya leseni za kutumia, kumiliki, kusafirisha na kuingiza nchini vyanzo vya mionzi ambapo leseni 447 sawa na asilimia 95 zimetolewa. Aidha, maombi 22 hayakukidhi vigezo;
- (ii) imekagua migodi mitano (5) ambayo ni Buzwagi Gold Mine, North Mara Gold Mine, Bulyankulu Gold Mine, Mkuju River Project na Oceanic na kubaini kuwa haina madhara ya mionzi kwa mazingira na wafanyakazi;
- (iii) imekagua na kuhakiki vituo 384 vya vyanzo vya mionzi nchi nzima ambapo ukaguzi huo ulibaini kuwa vituo 369 vilikuwa vinaendeshwa kwa kufuata taratibu husika na vituo 15 vilikuwa vinatumia vyanzo vya mionzi bila kufuata utaratibu wa kiusalama. Aidha, vituo vitano (5) vilitimiza masharti na hivyo vimeruhusiwa kuendelea na kazi zake;
- (iv) imesajili vituo vipya 58 kwa ajili ya kuanza kutumia vyanzo vya mionzi na hivyo kufikia jumla ya vituo 985 vilivyosajiliwa;
- (v) imewapima wafanyakazi 1,743 kwenye vituo 400 sehemu



mbalimbali nchini. Upimaji huo ulibaini kuwa katika vituo vyote viwango vya mionzi vilikuwa kati ya 0.1mSv hadi 4.5mSv ambavyo ni salama kwa binadamu;

- (vi) ilisafirisha vyanzo vya mionzi 14 vilivyokwisha muda wa matumizi kutoka Wakala wa Barabara Tabora na Taasisi ya Saratani ya Ocean Road kwa lengo la kuzuia madhara yanayoweza kutokea kutokana na vyanzo hivyo vikiachwa kuhifadhiwa bila utaratibu;
- (vii) ilipima sampuli 19,462 na kutoa vibali 29,613 vilivyojumuisha sampuli za vyakula 16,563, mbolea 363, na sigara pamoja na matumizi mengine kama chakula cha mifugo zilikuwa sampuli 2,536. Sampuli zote zilizopimwa hazikuwa na mionzi hatarishi;
- (viii) imeendelea kuratibu miradi mitano (5) ya kitaifa na kushiriki katika miradi 45 ya kikanda ambayo inatekelezwa kwa ushirikiano na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomu. Miradi hii inanufaisha sekta mbalimbali ikiwemo Afya, Kilimo, Maji, Elimu na Mifugo;
- (ix) ilinunua vifaa viwili (2) vya kupima mionzi (Sodium Iodide Detector) kwa ajili ya ofisi mbili (2) za kanda na vifaa vingine mbalimbali vya maabara kwa ajili ofisi 18 za mipakani vyenye thamani ya Shilingi 227,949,660.00. Vifaa hivi vimesaidia kuongeza kasi ya utoaji wa vibali ndani ya siku moja ili kulinda usalama wa wananchi, mazingira na kulinda masoko ya bidhaa zetu nje ya nchi;
- (x) imeendelea na ujenzi wa maabara changamano awamu ya pili ambayo itaboresha utoaji huduma na ufanisi katika utendaji wa kazi za Tume. Vilevile, Tume imepata mshauri elekezi kwa ajili ya michoro ya maabara za kanda zilizopo Dodoma, Zanzibar na Mwanza;

- (xi) imeendelea na upimaji wa mionzi kwenye mazingira katika vituo 14 ambavyo vimekuwa vikiendeshwa kwa ushirikiano na Taasisi nyingine. Pia, imepima usalama wa mionzi kwenye ofisi za wizara zote na makazi ya viongozi pamoja na maeneo yatakayokuwa na miradi mikubwa ya maendeleo kama vile maeneo ya ujenzi wa uwanja wa ndege jijini Dodoma;
- (xii) imeendelea kuendesha kituo cha kupima mionzi katika hewa ya anga (Radionuclide Monitoring Station-TZPRN64) kilichopo kampasi kuu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam chini ya mkataba wa kimataifa wa *Comprehensive Nuclear Test-Ban Treaty (CTBT) for Non-Proliferation Test (NPT) of Nuclear Weapons*. Upimaji wa usalama wa mionzi kwenye anga ni muhimu kwa kuendelea kulinda usalama wa mazingira yetu dhidi ya uchafuzi wa mionzi;
- (xiii) imekagua vituo 41 vinavyotoa mionzi isiyoayonishwa (Non-Ionizing Radiation) kama vile minara ya simu, redio, runinga, na vifaa vingine vya mionzi ili kubaini usalama wa wakazi wa maeneo husika;
- (xiv) imeendelea kujitangaza kwa kutumia maonesho ya Sabasaba, Nanenane, sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar na vipindi vya Televisheni na Redio pamoja na mitandao ya jamii. Vilevile, Tume ilishiriki katika maonesho matano (5) pamoja na vipindi 24 vya redio na 26 vya runinga. Aidha, vipeperushi na vijarida 3,000 vilisambazwa kwa lengo la kuelimisha wananchi na kuongeza uelewa kuhusu kazi za Tume, usalama wao na faida za matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia; na
- (xv) ilitoa mafunzo kwa maafisa 137 wa vyombo vya ulinzi na usalama na kuendesha mafunzo 14 ya muda mfupi ya kinga na udhibiti wa mionzi kwa taasisi na vituo mbalimbali vinavyotumia

vyanzo vya mionzi ambapo wafanyakazi 270 walipatiwa mafunzo.

### **C. MPANGO NA BAJETI YA FUNGU 46 KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21**

- 80. Mheshimiwa Spika,** Mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21 itatekelezwa kupitia Idara, Vitengo na Taasisi kama ilivyofafanuliwa katika majukumu ya Wizara. Malengo yatakayotekelezwa ni kama ifuatavyo:

#### **Ithibati na Usajili wa Shule na Vyuo vya Ualimu**

- 81. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza jukumu la kusimamia Sera na kuongeza upatikanaji wa fursa za Elimu na Mafunzo, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali itatekeleza yafuatayo:

- (i) itafanya ufuatiliaji na tathmini kwa shule 200 zilizopatiwa usajili ili kuhakiki uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za usajili wa shule;
- (ii) itafanya ufuatiliaji na tathmini kwa shule 100 zilizosajiliwa kwa masharti ili kuona kama zimekamilisha miundombinu iliyokuwa haijakamilika;
- (iii) itafanya ufuatiliaji na tathmini kwa shule 200 ili kuhakiki kama walimu wa kigeni wanafundisha kwa mujibu wa leseni zao;
- (iv) itaandaa "Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Ujenzi na Ukarabati wa Shule" ili kuwezesha wadau wote wa shule kufuatilia na kutathmini maendeleo ya ujenzi; na
- (v) itakamilisha uandaaji wa mfumo wa Kieletroniki wa usajili wa shule za Awali na Msingi, Vyuo vya Ualimu na Vituo Nje ya Mfumo Rasmi ili kuhakikisha usajili wa shule unafanyika kwa uwazi na wakati.

## **Usimamizi wa Elimumsingi na Sekondari**

**82. *Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha Elimumsingi na Sekondari, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itafanya ufuatiliaji na tathmini ya uendeshaji na usimamizi wa vituo Shikizi vya shule katika mikoa 15 ili kupima matokeo ya ufundishaji na ujifunzaji na kuchukua hatua stahiki;
- (ii) itafanya ufuatiliaji na tathmini katika shule za Ufundi, Kilimo na shule za Michezo ili kutathmini hali ya miundombinu ya ufundishaji na ujifunzaji;
- (iii) itaratibu mashindano ya insha ya nchi za Afrika Mashariki na Jumuiya ya nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara (SADC) kuwajengea wanafunzi uwezo wa kufikiri, kuandika na kujieleza;
- (iv) itatoa mafunzo ya malezi, unasihi na ulinzi wa mtoto shuleni kwa walimu 200 wa shule za sekondari ili kuwajengea uwezo na kuimarisha stadi za utoaji wa huduma za malezi shuleni;
- (v) itasambaza Mwongozo wa "Malezi, Unasihi na Ulinzi wa Mtoto Shuleni katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuvo vya Ualimu" ili kuimarisha utoaji wa huduma za malezi shuleni;
- (vi) itahuisha Miongozo na Nyaraka ya utekelezaji wa Programu ya MEMKWA Kudirika la II ili kuongeza fursa za elimu na mafunzo kwa vijana ambao hawakumaliza elimu ya msingi wenye umri kati ya miaka 14-18;
- (vii) itachapisha na kusambaza Miongozo na Vitabu vya MEMKWA Kudirika la I ili kuimarisha/kuinua ubora wa elimu na mafunzo kwa wanafunzi nje ya mfumo rasmi (MEMKWA Kudirika la I) ili kuendana na mabadiliko ya Mtaala mpya wa mfumo rasmi wa shule darasa la I – IV;

- (viii) itawezesha Vituo vya Walimu kutekeleza Mpango wa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini kwa kuandaa mwongozo kwa ajili ya Waratibu wa Vituo vya Walimu ili kuendana na Mpango wa mafunzo endelevu kazini;
- (ix) itaandaa moduli za mafunzo endelevu kazini kwa walimu wa shule za msingi kuhusu mtaala mpya, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na upimaji endelevu;
- (x) itawajengea uwezo Waratibu wa Vituo vya Ualimu na Maafisa Elimu Kata 966 kuhusiana na Mpango wa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini kwa kuzingatia Kiunzi cha Mafunzo Endelevu Kazini kwa Walimu (Teachers' Continuous Professional Development Framework);
- (xi) itaandaa moduli za mafunzo endelevu kazini kwa wawezeshaji wa MEMKWA kuhusu mtaala mpya, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na upimaji endelevu;
- (xii) itawajengea uwezo wawezeshaji wa MEMKWA na mahitaji maalum ngazi ya Mikoa na Halmashauri; na
- (xiii) itawajengea uwezo Maafisa Elimu Mikoa, Halmashauri, Kata na Walimu Wakuu kuhusu miongozo mipya ya usimamizi wa shule katika utekelezaji wa Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule.

### **Usimamizi wa Elimu Maalum**

**83. *Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa Elimu maalum, Serikali katika mwaka wa fedha 2020/21 imepanga kutekeleza yafuatayo:

- (i) itaendesha Mafunzo kazini kwa walimu wenye taaluma ya elimu maalum 350 wa shule za msingi na 150 wa shule za sekondari

- kuhusu Lugha ya Alama, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, na TEHAMA ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji shuleni;
- (ii) itafanya ufuatiliaji na tathmini katika shule za Sekondari 26, Msingi 52, Vyu vya Kati vitatu (3) na Vyu vya Vikuu saba (7) vinavyopokea wanafunzi wenye ulemavu ili kupima matokeo ya ufundishaji na ujifunzaji na kutoa ushauri wa kitaalamu;
  - (iii) itawezesha ununuzi wa vifaa maalum vya kielimu na saidizi katika shule za Msingi, Sekondari na Vyu vya Ualimu ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum; na
  - (iv) itahamasisha jamii kupitia vyombo vya habari, matukio ya kitaifa, na vikao maalum kuhusu utambuzi wa mapema, uandikishaji katika shule na utoaji wa huduma za kielimu kwa wanafunzi wenye ulemavu katika ngazi zote za elimu.

### **Usimamizi wa Elimu ya Ualimu**

**84. *Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha mafunzo ya Elimu ya Ualimu, Serikali katika mwaka wa fedha 2020/21 itatekeleza yafuatayo:

- (i) itafanya ufuatiliaji na tathmini kuhusu zoezi la udahili, ufundishaji na ujifunzaji wa walimu tarajali pamoja na uendeshaji wa Vyu vya Ualimu vya Serikali na visivyo vya Serikali ili kubaini upungufu na kufanya maboresho; na
- (ii) itaratibu na kusimamia mashindano ya michezo na Sanaa katika Vyu vya Ualimu vya Serikali na visivyo vya Serikali (UMISAVUTA) ili kuimarisha elimu ya michezo na sanaa vyuoni.

## **Uthibiti Ubora wa Shule na Vyuo vya Ualimu**

**85. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule na Vyuo vya Ualimu itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itafanya tathmini ya jumla katika asasi 6,020 zikiwemo shule za Msingi 4,700, Sekondari 1,200 na Vyuo vya Ualimu 120 pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na kitaaluma kwa walimu;
- (ii) itawajengea uwezo wathibiti ubora wa shule wapya 200 watakaoteuliwa kujiunga na idara ya uthibiti ubora wa shule katika ngazi ya kanda na wilaya; na
- (iii) itafanya tafiti tatu (3) za kielimu katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu ili kubaini mafanikio na changamoto za utoaji wa elimu nchini na kutoa mapendekezo stahiki.

## **Baraza la Mitihani la Tanzania**

**86. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Baraza la Mitihani la Tanzania litatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kuendesha Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa watahiniwa 1,825,387;
- (ii) kuendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa watahiniwa 1,009,938;
- (iii) kuendesha Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili kwa watahiniwa 612,745;
- (iv) kuendesha Mtihani wa Kidato cha Nne kwa watahiniwa 495,207 na Mtihani wa Maarifa kwa watahiniwa 15,044;

- (v) kuendesha Mtihani wa Kidato cha Sita kwa watahiniwa 90,182;
- (vi) kuendesha Mitihani ya Ualimu katika ngazi ya Astashahada na Stashahada kwa watahiniwa 8,135; na
- (vii) kuendesha Upimaji wa Kitaifa wa Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu - KKK kwa sampuli ya watahiniwa 33,350 wa Darasa la Pili mwezi Januari, 2021.

### **Taasisi ya Elimu Tanzania**

**87. *Mheshimiwa Spika***, katika kufanikisha upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa mwaka wa fedha 2020/21, Taasisi itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kuandaa aina nane (8) za vitabu (book titles) vya kiada Darasa la VII pamoja na viongozi vya mwalimu ili kutatua changamoto ya uwepo wa vitabu hivyo vinavyoendana na mtaala ulioboreshwa;
- (ii) kutafsiri aina tano (5) za vitabu vya kiada Darasa la VII kwa ajili ya matumizi ya shule zinazotumia lugha ya kiingereza;
- (iii) kuandaa vitabu vya kiada Darasa la VI na VII kwa matumizi ya wanafunzi wenye uoni hafifu na wasioona ili kuwawezesha katika ufundishaji na ujifunzaji;
- (iv) kuandika aina 40 za vitabu vya kiada ngazi ya sekondari ili kukidhi mahitaji ya mtaala;
- (v) kuandaa vitabu vya kiada aina 40 kwa matumizi ya wanafunzi wenye uoni hafifu na wasioona kwa ngazi ya sekondari ili kuhakikisha kuwa wanafunzi hao wanajifunza kwa ufanisi;
- (vi) kuandika miongozo 12 ya ufundishaji kwa njia ya vitendo



(*practical manuals*) kwa kidato cha kwanza mpaka cha sita;

- (vii) kutathmini vitabu vya ziada na maudhui ya kielektroniki yanayoandaliwa na wadau ili kuhakikisha kama vinakidhi mahitaji ya mtaala;
- (viii) kuandaa maudhui ya kielektroniki kwa ngazi ya Elimu ya Msingi ili kurahisisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji; na
- (ix) kuboresha mitaala ya Elimu ya Ualimu ngazi ya Astashahada na Stashahada na elimu ya sekondari ili kukidhi mahitaji ya sasa.

**88. *Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji, Serikali itatekeleza yafuatayo:

- (i) itaandaa mfumo wa mafunzo ya walimu kazini kwa njia ya mtandao ili kukuza stadi na mbinu za ufundishaji na ujifunzaji;
- (ii) itaendelea kutoa mafunzo kazini kwa walimu, wakufunzi na wathibiti ubora wa shule kuhusu mtaala ulioboreshwa ili kukuza stadi na mbinu za ufundishaji;
- (iii) itafanya ufuatiliaji wa matumizi ya vifaa vya utekelezaji wa mtaala kama vile vitabu, mihtasari na viongozi vya mwalimu ili kubaini mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji mtaala;
- (iv) itafanya tafiti za utekelezaji wa mtaala zitakazosaidia kuboresha ufundishaji na ujifunzaji; na
- (v) itaandaa matini ya kidigitali na kurekodi vipindi vya redio na television ili kuboresha ujifunzaji na ufundishaji.

## **Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu-ADEM**

**89. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala utatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kudahili walimu 2,483 watakaosoma kozi za Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu na Uthibiti Ubora wa Shule ili kuwapa ujuzi na maarifa katika utoaji na Usimamizi wa Elimu;
- (ii) kujenga jengo la utawala, madarasa, maktaba na kompyuta katika Kampasi ya ADEM-Mbeya ili kuwezesha kuhudumia wanachuo 421 na kukarabati jengo la Kihistoria la zamani la ADEM pamoja na nyumba nne (4) za wafanyakazi kampasi ya Bagamoyo;
- (iii) kutoa mafunzo kwa ngazi ya Astashahada ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu (CELMA) kwa Wakuu wa Shule za Msingi 32 ili kuwajengea uwezo wa kuongoza na kusimamia Shule zao kwa ufanisi;
- (iv) kuratibu mafunzo ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu kwa washiriki 250 ambao ni Wakuu wa Vyuo vya Ufundi Stadi (VET) na Wasaidizi wao, na Wakuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDC) kwa lengo la kuimarisha uongozi na usimamizi wa taasisi zao;
- (v) kuratibu mafunzo ya muda mfupi ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu kwa viongozi 4,548 wakiwemo Wakuu wa Shule za Sekondari, Maafisa Elimu katika ngazi ya kata hadi Mkoa ili kuimarisha mbinu bora za uongozi na usimamizi wa Elimu;
- (vi) kufanya tafiti tatu (3) kuhusu Uongozi na Usimamizi wa Elimu katika maeneo yenye changamoto na kutoa ushauri; na
- (vii) kufadhili watumishi sita (6) katika mafunzo ya muda mrefu katika

maeneo ya taaluma na 20 katika mafunzo ya muda mfupi.

### **Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima**

**90. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kisomo na Elimu kwa Umma (NALMES) ili kupunguza kiwango cha watu wasiojua kusoma na kuandika kwa kuwajengea uwezo maafisa na wataalamu wa kisomo;
- (ii) itaboresha miundombinu ya ufundishaji na ujifunzaji katika Elimu ya Sekondari Nje ya Mfumo Rasmi kwa mikoa 24 na kuongeza udahili kutoka wanafunzi 13,036 hadi 14,930;
- (iii) itafanya utafiti wa kitaifa juu ya hali ya kisomo na elimu kwa umma utakaoboresha utekelezaji wa Mkakati wa Kisomo na Elimu kwa Umma;
- (iv) itatekeleza miradi ya Elimu ya Watu Wazima ikiwemo: Mradi wa Elimu ya Sekondari kwa Wanafunzi walio Nje ya Mfumo Rasmi, Mpango wa Elimu changamani kwa vijana walio Nje ya Mfumo Rasmi (IPOSA) na Mradi wa kuwawezesha vijana na watu wazima kielimu;
- (v) itaongeza udahili wa wanafunzi wa Astashahada, Stashahada na Shahada kutoka 3,062 hadi kufikia 3,200; na
- (vi) itajenga na kukarabati miundombinu ya ufundishaji na ujifunzaji katika vituo vilivyoko katika mikoa minne (4) ya Dar es Salaam, Dodoma, Morogoro - WAMO na Mwanza.

## **Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (BOHUMATA)**

**91. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania itatekeleza yafuatayo:

- (i) itaongeza vitabu 40,000 na vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya watu wazima na watoto ili kuongeza ari ya usomaji katika jamii;
- (ii) itaendelea kutoa ushauri wa Kitaalam juu ya uanzishaji na uendeshaji wa Maktaba za Shule, Vyuo na Halmashauri za Miji na Wilaya nchini;
- (iii) itatoa mafunzo ya Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka katika ngazi ya Cheti cha Msingi (NTA 4) wanafunzi 400, Cheti (NTA 5) wanafunzi 300 na Stashahada (NTA 6) wanafunzi 300;
- (iv) itaanza taratibu za ujenzi wa maktaba katika Mikoa ya Singida, Shinyanga, Simiyu na Dodoma pamoja na Wilaya ya Chato, na Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka – Bagamoyo na;
- (v) itakarabati majengo ya Maktaba za Mikoa ya Ruvuma, Songwe, Kilimanjaro, Morogoro, Kigoma, Rukwa, Kagera, Iringa na Tabora.

## **Mamlaka ya Elimu Tanzania**

**92. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Mamlaka itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itawezesha ujenzi wa madarasa 180 katika shule za Msingi 50 na Sekondari 10 zenye uhaba wa vyumba vya madarasa ili kuboresha mazingira ya utoaji elimu;
- (ii) itawezesha ujenzi wa nyumba 100 za walimu katika Shule za Sekondari 25 zilizopo katika maeneo yenye mazingira magumu ili kuongeza ufanisi kwa walimu;
- (iii) itawezesha ujenzi wa mabweni 15 ya wanafunzi wa kike katika

shule 15 za sekondari zenye mazingira magumu. Kukamilika kwa mradi huu kutanufaisha wanafunzi wa kike 1,200;

- (iv) itawezesha ujenzi wa matundu ya vyoo 432 katika shule za msingi 13 na sekondari tano (5) zenye upungufu ili kuboresha mazingira kwa wanafunzi na kupunguza magonjwa ya mlipuko;
- (v) itawezesha awamu ya kwanza ya ujenzi wa shule ya msingi ya kisasa inayotumia Kiingereza kufundishia katika jiji la Dodoma;
- (vi) itawezesha ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na uboreshaji wa miundombinu katika Chuo Kikuu kimoja kutoka Zanzibar ili kuboresha upatikanaji wa Elimu ya Juu; na
- (vii) itawezesha ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia na ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule za Msingi nne (4) na Sekondari nne (4).

### **Kituo cha Maendeleo Dakawa**

**93. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/21, Serikali kupitia Kituo cha Maendeleo Dakawa, itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kupanda miti ya mbao aina ya mitiki 9,240 kuzunguka eneo lenye ukubwa wa ekari 140 ili kuhifadhi mazingira ya kituo;
- (ii) kukarabati nyumba tano (5) za watumishi (2 in 1) zenye uwezo wa kubeba familia 10 na kuendeleza ujenzi wa nyumba mbili (2) ili kuboresha mazingira ya makazi kwa watumishi;
- (iii) kuendeleza, kuhifadhi na kutunza kumbukumbu adhimu za nyaraka, majengo na makaburi ya makumbusho ya wapigania uhuru wa ANC; na
- (iv) kupima eneo la kituo lenye ukubwa wa ekari 7,500 kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa na kulipatia hati.

## **Uimarishaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi**

**94. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itatoa mafunzo ya muda mrefu ya Ufundi Stadi na Elimu ya Wananchi (Folk Education) kwa washiriki wapatao 10,000 katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54 ili kuongeza ujuzi utakaowawezesha wahitimu kujajiri na kuajiriwa;
- (ii) itawezesha mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 24,000 katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili kuwaongezea uwezo wa kutekeleza miradi na shughuli katika maeneo wanayoishi;
- (iii) itawajengea uwezo wakufunzi 670 kutoka katika Taasisi za Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ili kuwaongezea uwezo wa ufundishaji wa mitaala inayoendana na soko la ajira;
- (iv) itaendelea kuratibu uhamasishaji kwa wanafunzi wa kike kujiunga na masomo ya Sayansi kwa lengo la kuwaongezea sifa za kujiunga na Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi;
- (v) itaendelea kuratibu upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54 ili kuhakikisha elimu itolewayo inaendana na soko la ajira;
- (vi) itawezesha maafisa 7 kushiriki mikutano ya ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa kwenye maeneo ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi nje ya Nchi ili kuwajengea uwezo wa kuratibu na kusimamia Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini;
- (vii) itawezesha mkutano wa kimkakati wa Taasisi nne (4) ambazo ni Mamlaka ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), *Tanzania Private Sector Foundation (TPSF)* na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE)

- ili kuwajengea uwezo wa kusimamia na kuratibu mafunzo na uandaaji wa Mitaala ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi;
- (viii) itagharamia upimaji na upatikanaji wa hati miliki ya maeneo ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kote nchini kwa lengo la kuhakikisha kuwa maeneo hayo hayavamiwi na wananchi wanaozunguka vyuo hivyo;
  - (ix) itaendelea kugharimia chakula katika vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54;
  - (x) itaendelea kuratibu ujenzi wa Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi 25 vya Wilaya (DRVTSC) kwa lengo la kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ya Ufundi; na
  - (xi) itaendelea kuratibu uanzishwaji wa vituo vinne (4) vya umahiri kwenye nyanja za TEHAMA, Usafiri wa anga, Nishati jadidifu na Mazao ya ngozi katika Taasisi za DIT, NIT na ATC kupitia mradi wa *East Africa Skills for Transformation and Regional Integration Project* (EASTRIP) kwa lengo la kuviongezea vyuo hivyo uwezo wa kutoa mafunzo kwa vitendo yanayoendana na soko la ajira.

### **Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA)**

**95. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, mamlaka itatekeleza yafuatayo:

- (i) itadahili jumla ya wanafunzi 2,800 wakiwemo wanafunzi 400 wenye mahitaji maalum na vijana 2,400 kutoka kwenye mazingira magumu ifikapo Juni, 2021;
- (ii) itaongeza udahili wa wanafunzi kutoka 370,000 hadi 700,000 ifikapo Juni, 2021 ikiwemo ongezeko la wanafunzi wa kike kutoka

asilimia 35 hadi asilimia 45;

- (iii) itatoa mafunzo kwa wajasiriamali 3,000 wa Sekta isiyo rasmi kupitia programu ya *INTEP* (Intergrated Training for Entrepreneurship Promotion) kwa lengo la kuwaongezea uwezo wa uendeshaji wa shughuli zao za kiuzalishaji; na
- (iv) itaendelea kutoa mafunzo kwa walimu wa Elimu ya Ufundi Stadi wa vyuo vya VETA na FDC kwa lengo la kuwaongezea uwezo wa kufundisha kwa kupitia mradi wa SET (Skills for Employment Tanzania) unaofadhiliwa na Serikali ya Uswisi.

**96. *Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha utawala na usimamizi wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Mamlaka itatekeleza yafuatayo:

- (i) itaboresha utendaji kazi kwa kutekeleza Muundo wa Mamlaka na *Scheme of Service* mpya na kuajiri watumishi wapya ili kuziba nafasi zilizo wazi;
- (ii) itawajengea uwezo watumishi katika taaluma zao;
- (iii) itaendelea kutangaza shughuli za Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini kwa lengo la kutoa elimu kwa jamii kuhusu huduma zinazotolewa na mamlaka; na
- (iv) itajenga nyumba 23 za watumishi kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwenye Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi kama ifuatavyo: Makete (6); Ulyankulu (10); Busokelo (2) na Namtumbo (5) pamoja na kukarabati nyumba saba (7) za watumishi wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi zilizopo Tabata Dar es Salaam.



**97. *Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Mamlaka ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi itaendelea kuimarisha Ubora wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, kwa kutekeleza yafuatayo:

- (i) kuimarisha mfumo wa utafiti pamoja na kufanya utafiti wa soko la ajira kwenye sekta tatu (3) za uchapishaji vitabu, biashara na sekta ya umeme;
- (ii) kuanzisha kitengo cha unenepeshaji Ng'ombe kwenye Kituo cha Mafunzo na Kiwanda cha Nyama katika Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Dodoma pamoja na kukamilisha uanzishwaji wa Kituo cha Uchapaji kwenye Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi Chang'ombe, Dar es Salaam;
- (iii) kutoa elimu kwa wadau kuhusu matumizi ya taarifa za soko la ajira na kuratibu ukusanyaji wa taarifa za Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini; na
- (iv) kuratibu utekelezaji wa mpango wa kukuza ujuzi viwandani - *Skills Enhancement Programme* (SEP) katika makampuni 60 ambao utawajengea uwezo wafanyakazi na kuwapelekea teknolojia mpya bila kulazimika kuhudhuria mafunzo vyuoni.

**98. *Mheshimiwa Spika***, Serikali itaendelea na ujenzi wa vyuo vya Ufundi Stadi na Huduma vya mikoa ya Kagera, Geita, na Rukwa. Vilevile, itaendelea na ujenzi wa vyuo 30 vya Mafunzo ya Ufundi Stadi vya Wilaya za Monduli, Buhigwe, Butiama, Chemba, Chunya, Ikungi, Igunga, Kishapu, Kwimba, Chato, Mbarali, Mafia, Pangani, Ulanga, Uvinza, Kilindi, Korogwe, Longido, Masasi, Mkinga, Ukerewe, Uyui, Bahi, Iringa, Lushoto, Kongwa, Ruangwa, Nyasa, Kasulu na Rufiji ili kutoa fursa za mafunzo kwa jamii.

- 99. *Mheshimiwa Spika***, Serikali itajenga mabweni sita (6) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 64 kila moja, katika Vyuo mbalimbali vya Ufundi Stadi kama ifuatavyo: Namtumbo (2), Mbeya (1), Mara (1), Dakawa (1), na Makete (1) ili kutatua changamoto ya malazi. Vilevile, itaendelea na ujenzi wa madarasa sita (6) katika Chuo cha Ufundi Stadi cha Makete yenye uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 160.
- 100. *Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwenye vyuo vya ufundi stadi, Serikali itanunua na kuweka vifaa vipya vya kujifunzia katika vyuo vikongwe 29 vya Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini pamoja na kuvifanyia ukarabati. Aidha, itajenga karakana 12 kwenye Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi na Huduma vya Mkoa ya Lindi, Pwani, Manyara, Kihonda, Kipawa na Mwanza. Aidha itakarabati karakana mbili (2) za Useremala na Uchomeleaji Vyuma katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi cha Arusha.

### **Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi**

- 101. *Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka wa fedha 2020/21, Baraza litatekeleza kazi zifuatazo:
- (i) litafuatilia na kutathimini Vyuo 200 vya Elimu ya Ufundi ili kuhakikisha kuwa Mafunzo yanayotolewa yanakidhi viwango vya ubora;
  - (ii) litakagua na kuhakiki Vyuo 60 kwa ajili ya usajili wa Vyuo vitakavyokidhi sifa ya kutoa Mafunzo ya Elimu ya Ufundi, pamoja na kutoa miongozo itakayoviwezesha Vyuo kupata ithibati kamili endapo vitakidhi vigezo vilivyowekwa;
  - (iii) litahakiki na kuidhinisha Mitaala 150 ya Vyuo vya Elimu ya Ufundi nchini ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira; na

- (iv) litaratibu na kuhakiki udahili wa wanafunzi wapatao 150,000 katika programu za Astashahada na Stashahada.

## **Chuo cha Ufundi Arusha**

**102. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Chuo cha Ufundi Arusha kitatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kitadahili wanafunzi 1,390 wa mwaka wa kwanza kwa ngazi za Stashahada na Shahada (NTA level IV-VIII) na wanafunzi 1,000 wa ngazi ya Ufundi Stadi (NVA level I-III);
- (ii) kitajenga bweni la wasichana lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 kwa wakati mmoja na maktaba yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 ili kuongeza udahili na kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji;
- (iii) kitakarabati madarasa, mabweni, barabara za ndani, majengo ya ofisi, mfumo wa maji safi na majitaka, mfumo wa mawasiliano wa ndani na nyumba za makazi kwa lengo la kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji;
- (iv) kitakamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa tatu (3) lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja litakalokuwa na maabara, madarasa na ofisi za walimu kupitia ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa lengo la kuboresha mazingira ya kusomea;
- (v) kitaendeleza Kituo cha Mafunzo ya Nishati Jadidifu cha Kikuletwa ili kiwe Kituo cha Umahiri (Centre of Excellence) kupitia mradi wa

EASTRIP unaofadhiliwa na Benki ya Dunia;

- (vi) kitafanya utafiti juu ya matumizi bora ya maji katika kilimo cha mpunga kwa kushirikiana na shirika la utafiti kutoka Japan (JIRCAS) ili kuwezesha wananchi kuongeza uzalishaji wa zao hilo kwa kutumia maji kidogo; na
- (vii) kitaendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kwa walengwa mbalimbali kuhusu uimara wa udongo, kokoto na lami zinazotumika katika ujenzi wa barabara, kupima ubora wa maji, usanifu wa miradi ya maji na ujenzi wa aina mbalimbali kwa lengo la kuwajengea uwezo wafanyakazi wa taasisi husika.

### **Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**

**103. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere itatekeleza yafuatayo:

- (i) itadahili wanafunzi 9,389 kwa mwaka wa masomo 2020/21;
- (ii) itafanya tafiti 10 zenye lengo la kutafuta ufumbuzi wa matatizo yanayoikabili jamii katika maeneo ya Maendeleo ya uchumi 3, Jinsia na Maendeleo (2), Taaluma za jamii (3) na Maadili na Uongozi (2). Aidha, itaandika maandiko ya miradi ya utafiti mawili (2) kwa ajili ya ufadhili kutoka nje ya Chuo;
- (iii) itafadhili watumishi wanataaluma 10 kwenda masomoni katika ngazi za Uzamivu na Uzamili ili kuongeza idadi ya wahadhiri;
- (iv) kuendelea na ujenzi wa bweni la wanafunzi katika Kampasi ya Karume litakalokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000

kwa wakati mmoja na jengo la Maktaba katika Kampasi ya Kivukoni kwa lengo la kuongeza udahili na kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia. Aidha, itakarabati madarasa na nyumba za watumishi, barabara za ndani ya chuo, umeme pamoja na mifumo ya maji safi na majitaka; na

- (v) itahuisha mitaala 34 ya chuo ili iendane na mahitaji ya soko. Aidha, itaboresha mfumo wa TEHAMA katika kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

### **Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu ya Juu**

**104. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Idara ya Elimu ya Juu itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itaendelea kuratibu maendeleo ya udahili, uandikishaji na utoaji wa mikopo kwa wanafunzi katika Taasisi za Elimu ya Juu;
- (ii) itaendelea kuratibu ufadhili wa masomo wa wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka mashirika na nchi rafiki;
- (iii) itaratibu ufadhili wa wanafunzi 10 raia wa China kusoma Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;
- (iv) itafanya ufuatiliaji wa utendaji wa Vituo vya Umahiri vya Afrika katika Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini (African Centre of Excellence- ACE II) ambavyo vipo katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela;
- (v) itaendelea kuratibu ufadhili wa masomo ya wanataaluma 68

kutoka Vyuo Vikuu vya Umma katika shahada za umahiri kwenye nyanja za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati;

- (vi) itaratibu na kufuatilia utekelezaji wa Mradi wa 'Higher Education for Economic Transformation' (HEET); na
- (vii) itaendelea kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum wa Vyuo Vikuu ili waweze kujifunza kwa ufanisi.

### **Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania**

**105. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/21, Tume itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itakagua Vyuo Vikuu 25 kwa lengo la kuhakiki ubora wake;
- (ii) itafanya tathmini ya programu 200 za masomo mbalimbali katika Vyuo Vikuu nchini na kuzisajili zile zitakazokidhi vigezo;
- (iii) itafanya tathmini na kutambua tuzo 5,000 zilizotolewa katika Vyuo Vikuu nje ya nchi;
- (iv) itaratibu udahili na kuhakiki maombi ya wanafunzi takribani 100,000 wa mwaka wa kwanza watakaomba kudahiliwa katika Vyuo vya Elimu ya Juu katika programu mbalimbali;
- (v) itaandaa miongozo ya ulinganifu (Benchmarks Standards) kwenye programu za masomo ya Uhandisi na Sayansi ya Tiba ya Binadamu;
- (vi) itafanya utafiti ili kuweza kuishauri Serikali kuhusu masuala mbalimbali yenye lengo la kufanya maboresho kwenye mfumo wa utoaji Elimu ya Juu nchini;

- (vii) itakagua Asasi/Kampuni zinazojishughulisha na uratibu wa wanafunzi wanaokwenda kusoma nje ya nchi kwa lengo la kuzitambua na kuzisajili;
- (viii) itaboresha mfumo wa kutumia TEHAMA katika utoaji na ukusanyaji taarifa kutoka vyuo vya Elimu ya Juu nchini ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati kwa ajili ya mipango na maamuzi ya kisera na kiutendaji;
- (ix) itashiriki katika makongamano na mikutano inayohusu uimarishaji na Uthibiti wa Ubora wa Elimu ya Juu katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kimataifa kwa lengo la kuongeza ujuzi na weledi katika kuthibiti ubora wa Elimu ya Juu nchini; na
- (x) itaratibu maonesho ya 15 ya Elimu ya Juu nchini ili kutoa elimu kwa umma kuhusu vyuo na propramu mbalimbali zinazotolewa.

### **Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

**106. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/21, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itatoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji **54,000** wa mwaka wa kwanza yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 199.8** ikilinganishwa na wanafunzi **49,799** waliopata mikopo yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 173.2** katika mwaka 2019/2020. Lengo la utoaji mikopo ni kuwawezesha wanafunzi wengi zaidi wa Kitanzania kupata Elimu ya Juu bila kuathiriwa na hali zao za kiuchumi na kijamii;
- (ii) itatoa mikopo kwa wanafunzi 91,000 wanaoendelea na masomo yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 264.2** ikilinganishwa na wanafunzi 82,320 waliopata mikopo katika mwaka wa fedha 2019/20;

- (iii) itakusanya mikopo iliyoiva kutoka kwa wanufaika yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 190** ili zitumike kutoa mikopo kwa wanafunzi wenye uhitaji na kuwa na sifa ya kupata mikopo;
- (iv) itaendesha programu za elimu ya uombaji mikopo kwa usahihi katika shule 300 za sekondari na vyuo 70 ili kupunguza makosa yanayofanywa na waombaji wa mikopo wakati wa uombaji na hivyo kuwakosesha mikopo; na
- (v) itatoa elimu kwa waajiri na wafanyabiashara katika mikoa 20 kuhusu umuhimu wa urejeshaji wa mikopo kwa wakati ili kuwezesha ukusanyaji wa marejesho ya mikopo.

### **Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

**107. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kudahili wanafunzi 29,056 wa shahada za awali pamoja na kuongeza udahili wa wanafunzi wa kike kutoka 12,129 hadi 12,735 ambapo ufadhili wa masomo utatolewa kwa wanafunzi 50 wa kike wanaosomea masomo ya sayansi;
- (ii) kuongeza idadi ya miradi ya tafiti kutoka 173 hadi 221 kwa kuwafadhili watafiti 40 katika maeneo yanayolenga uchumi wa viwanda na kuzingatia Ajenda ya Utafiti ya Taifa;
- (iii) kuongeza idadi ya machapisho ya CKD katika majarida ya kitaifa na kimataifa kutoka 1,048 hadi 1,103;
- (iv) kuongeza idadi ya majarida ya CKD ya kimataifa kutoka 13 hadi 16 na kuyafanya yafikike kwa njia ya mtandao ifikapo Juni 2021;
- (v) Kugharamia wanataaluma 112 kusoma masomo ya uzamili katika fani mbalimbali; na
- (vi) kukamilisha upanuzi wa Hosteli za Dkt. John Pombe Joseph



Magufuli kwa ghorofa mbili zaidi zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,280 hivyo kufanya Hosteli hizo kuweza kuchukua jumla ya wanafunzi 5,120.

**108. *Mheshimiwa Spika***, Serikali itakamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la Shule Kuu tarajiwa ya Uchumi katika kampasi ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere lenye ghorofa sita (6) ambalo litakuwa na ofisi 50 za wafanyakazi; ofisi za kukaa wanafunzi 60 wa masomo ya uzamili, kumbi za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800, ukumbi wa mikutano wenye uwezo wa kuchukua watu 80 na sehemu ya huduma ya chakula yenye uwezo wa kuhudumia watu 120 kwa wakati mmoja.

**109. *Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha mazingira ya watumishi na wanachuo, Serikali itaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la kituo cha wanafunzi ambapo kukamilika kwa jengo hili kutasaidia kuwa na sehemu za kujisomea, sehemu za kibenki, maduka, *saloon* za kike na kiume, sehemu za vinywaji, kumbi za burudani na ofisi ya Mlezi wa Wanafunzi.

### **Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam**

**110. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kudahili wanafunzi wa mwaka wa kwanza 1,900 kati yao 600 ni wa fani ya Sayansi;
- (ii) kugharamia uendeshaji wa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 3,850 ili kukazia maarifa yatolewayo kwa njia ya nadharia;
- (iii) kuimarisha ufundishaji na utoaji wa huduma kwa kuajiri jumla ya

wafanyakazi 164 kati yao wanataaluma ni 45 na waendeshaji ni 119;

- (iv) kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwa kugharamia ununuzi wa vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi 68 pamoja na vifaa vya utafiti kwa wanataaluma ili kuhakikisha kuwa watu wenye mahitaji maalum wanapata fursa sawa za elimu;
- (v) kuandaa mitaala minne (4) mipya ya Stashahada za Uzamili, Shahada za awali na Uzamivu ili kuongeza fursa za wanufaika na Eimu ya Juu;
- (vi) kufanya tafiti 20 zinazotatua matatizo ya jamii na kutoa huduma tano (5) za ushauri wa kitaalamu katika maeneo ya elimu, sayansi na sayansi za jamii;
- (vii) kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la utawala ili kuongeza ofisi hamsini (50) za wafanyakazi na vyumba vya utafiti na kujenga jengo la maabara za sayansi na vyumba vya kujifunzia ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa vitendo;
- (viii) kuimarisha miundombinu kwa kukarabati mabweni na kumbi za mihadhara, kuimarisha miundombinu ya TEHAMA na ujenzi wa mfumo wa ukusanyaji wa maji taka ili kuhakikisha kuwa miundombinu ya chuo ni rafiki kwa shughuli za ufundishaji na ujifunzaji;
- (ix) kupunguza tatizo la uhaba wa malazi kwa wanafunzi kwa kujenga hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 na kuiwekea samani. Vilevile, itaboresha hosteli za wanafunzi (NSSF Mtoni Kijichi) zenye uwezo wa kuchukua jumla wanafunzi 500; na
- (x) kujenga madarasa katika shule ya Msingi ya Mazoezi

Chang'ombe na Shule ya Sekondari ya Mazoezi Chang'ombe pamoja na maabara nne (4) za sayansi ili kuongeza fursa za kupata elimu.

### **Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa**

**111. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa itatekeleza yafuatayo:

- (i) itaongeza udahili wa wanafunzi wa shahada za awali na uzamili kutoka 6,315 hadi kufikia 6,635;
- (ii) itaanzisha shahada mpya tatu (3) za awali na tatu (3) za umahiri ili kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu;
- (iii) Itaongeza machapisho 20 katika Nyanja za Insia na Sayansi ya Jamii, Elimu na Sayansi;
- (iv) itaratibu makongamano mawili (2) ya kitaaluma na kutekeleza miradi 10 ya utafiti na ushauri ili kuongeza wingi na ubora wa kazi za kitafiti na kiugunduzi;
- (v) itafadhili mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa watumishi 75 katika ngazi za Shahada ya kwanza, Umahiri na Uzamivu ili kuongeza weledi na ufanisi katika utendaji wa kazi;
- (vi) itanunua vifaa vya TEHAMA, vitabu 2,000 pamoja na vifaa vya maabara za Fizikia, Baolojia na Kemia; na
- (vii) itaimarisha mafunzo kwa vitendo kwa kupanua maabara ya Baiolojia yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 120 kwa wakati mmoja kwa ajili ya kuboresha mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji kwa vitendo. Baada ya upanuzi maabara itaweza kuchukua wanafunzi 240 kwa wakati mmoja.

## **Chuo Kikuu Mzumbe**

**112. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu Mzumbe itatekeleza yafuatayo:

- (i) itasajili wanafunzi wapya 5,864 (Astashahada 747, Stashahada 760, Shahada ya kwanza 3,631, Shahada ya Umahiri 716 na Shahada ya Uzamivu 10) kwa lengo la kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu;
- (ii) itaandaa programu 10 mpya za masomo kwa lengo la kuongeza fursa za masomo;
- (iii) itafadhili masomo kwa watumishi 66 wakiwemo Shahada ya Uzamivu 44 na Shahada ya Umahiri 22. Aidha, itawezesha watumishi 40 kuhudhuria warsha, semina na makongamano ndani na nje ya nchi ili kuongeza ujuzi na ufanisi katika kazi; na
- (iv) itachapisha machapisho 35 katika majarida ya Kitaifa na Kimataifa na kuchapisha jarida la "Uongozi" la Chuo Kikuu Mzumbe kwa lengo kuwezesha jamii kupata maarifa. Aidha, itaandaa mapendekezo 15 ya kazi za utafiti na mapendekezo 30 ya kazi za ushauri wa kitaalamu.

**113. *Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, Serikali itaendelea na ujenzi wa madarasa, ofisi, ukumbi, uwekaji wa samani na miundombinu ya TEHAMA katika jengo la Kampasi Kuu (Maekani). Aidha, itajenga bwalo la chakula na kuweka samani katika majengo yaliyopo Kiwanja Na. 300 Kitalu D Tegeta, Kampasi ya Dar es Salaam pamoja na kukarabati na kuweka samani katika jengo la wanafunzi wa Shahada za Uzamivu (PhD).

## **Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA)**

**114. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo itatekeleza yafuatayo:

- (i) itaongeze udahili wa wanafunzi wa mwaka wa kwanza, wakiwemo wanafunzi wa Shahada za Kwanza kutoka 4,526 hadi 4,845, Shahada za Juu (Umahiri na Uzamivu) kutoka 195 hadi kufikia 245;
- (ii) itaanzisha shahada mpya za awali mbili (2) na shahada za uzamili tatu (3) katika fani tatu (3) ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira;
- (iii) itaanzisha tafiti mpya 45 na kuendelea kufanya tafiti zilizopo 103 kwa lengo la kuboresha uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo, misitu na uvuvi ili kuhuisha elimu na uwezo wa wananchi katika kuzalisha mali na malighafi za mazao ya kilimo kwa ajili ya viwanda;
- (iv) itaongeze utoaji wa elimu na ushauri kwa washiriki 2,500 wakiwemo wakulima, maafisa ugani na watafiti kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile vituo atamizi, mashamba darasa, semina, kozi fupi, runinga na redio ili kuongeza uzalishaji na tija na hatimaye kupunguza umaskini kwa wananchi;
- (v) itaboresha na kuongeza mahusiano na taasisi nyingine ndani na nje ya nchi ili kuleta tija katika tafiti na shughuli mbalimbali za maendeleo;
- (vi) itajengea uwezo vitengo vya uzalishaji ili kuongeza mapato ya ndani ya chuo kwa asilimia ishirini; na
- (vii) itaajiri wafanyakazi 238 kwenye maeneo yenye upungufu na kuwaongezea elimu.

- 115. *Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza fursa za udahili ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, Serikali itajenga ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000, pamoja na chanzo kipya cha maji na mfumo mpya wa maji taka na itaboresha miundombinu ya maji iliyopo katika kampasi ya Solomon Mahlangu.
- 116. *Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, Serikali itakarabati vyumba 17 vya madarasa Kampasi kuu na Kampasi ya Solomon Mahlangu, majengo ya ofisi na maabara katika idara za DFRAM na DEC, majengo ya idara ya mimea vipando (Crop Science), mabweni na hosteli tano (5), *Hortculture shed house* (Crop museum) pamoja na kukarabati majengo na kununua samani kampasi ya Tunduru.
- 117. *Mheshimiwa Spika***, Serikali itakarabati miundombinu kampasi ya Katavi, kituo cha mafunzo ya kilimo kwa wakulima kilichopo Mgeta, kiwanda cha samani Vuyisile SMC pamoja na mabweni matano (5), nyumba 30 za wafanyakazi katika Kampasi ya Solomon Mahlangu.
- 118. *Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha mafunzo kwa vitendo na kutoa huduma katika jamii, Serikali itatekeleza yafuatayo:
- (i) itapanua misitu ya mafunzo iliyopo Madaba – Songea kwa kupanda miti hekari 300 pamoja na shamba la mkonge Morogoro kwa kuongeza hekari 200;
  - (ii) itafufua kitengo cha ufugaji wa ng'ombe na nguruwe pamoja na maghala ya kuhifadhia chakula cha mifugo katika shamba la mifugo la Solomon Mahlangu;
  - (iii) itaanzisha malisho ya asili (natural pastures) Kampasi Kuu na

Kampasi ya Solomon Mahlangu; na

- (iv) itafunga mfumo wa kisasa wa umwagiliaji (traveller irrigation gun) kwenye shamba la mafunzo lililopo Kampasi Kuu.

### **Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili**

**119. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili itatekeleza yafuatayo:

- (i) itaongeze udahili wa wanafunzi wa Shahada ya Uzamivu, Shahada ya Uzamili, Shahada ya kwanza na Stashahada kutoka udahili wa sasa wa wanafunzi 4,051 hadi kufikia wanafunzi 4,500;
- (ii) itaongeze udahili wa wanafunzi wa kike kutoka asilimia 29 hadi asilimia 40, ili kuongeza rasilimali watu iliyo na uwiano wa kijinsia;
- (iii) itahakikisha asilimia 40 ya idara zote za kitaaluma zinaanzisha angalau kozi tatu za muda mfupi kwa ajili ya mafunzo ya kuendeleza ueledi na maadili (professionalism and ethics) kwa wafanyakazi wa kada ya afya kote nchini ili kuboresha utendaji katika kutoa huduma za afya;
- (iv) itaongeze matumizi ya TEHAMA katika kujifunzia na kufundishia kutoka asilimia 25 hadi kufikia asilimia 40, ili kuongeza ufanisi wa kufundisha idadi kubwa ya wanafunzi kwa wakati mmoja; na
- (v) itafanya kongamano la tisa (9) la kisayansi (9<sup>th</sup> MUHAS Scientific Conference) na kuboresha semina za kitafiti za ndani ya chuo ili kusambaza matokeo ya tafiti kwa wadau ikiwemo watunga sera za afya.

**120. *Mheshimiwa Spika***, ili kujenga uwezo wa ndani wa kuandaa na kufanya tafiti zenye tija katika jamii pamoja na kutoa huduma za ushauri, Serikali itatekeleza yafuatayo:

- (i) itaimarisha makundi ya kitafiti (Research Clusters) na kutoa mafunzo kwa viongozi wa makundi hayo ili kujenga uwezo wa ndani wa kuandaa na kufanya tafiti zenye tija katika kutatua changamoto za afya;
- (ii) itaanzisha miradi mipya miwili (2) ya tafiti na kutoa huduma tano (5) mpya za ushauri wa kitaalamu pamoja na kuanzisha mahusiano na wenye viwanda watatu (3) ili kuongeza uwezo wa kuzalisha rasilimali watu katika kada ya afya watakaoleta tija katika kuendeleza viwanda; na
- (iii) itaongeza utoaji huduma katika vitengo mbalimbali vya chuo ikiwemo shule ya meno na kuanza mpango wa ujenzi wa Kliniki ya Uporoto (Uporoto Polyclinic), ili kuimarisha mazingira ya kufundishia, kutafiti na kutoa huduma za tiba; na

**121. *Mheshimiwa Spika***, ili kuzalisha rasilimaliwatu wenye utaalamu wa kutafiti, kutibu na kukinga magonjwa ya moyo na mishipa ya damu, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya tafiti kwa kukamilisha kituo cha Umahiri wa magonjwa ya moyo na mishipa ya damu (Center of Excellence in Cardiovascular Sciences) katika kampasi ya Mloganzila.

### **Chuo Kikuu cha Dodoma**

**122. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Dodoma itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kudahili jumla ya wanafunzi 31,604 ambapo Shahada za awali ni



27,379; Astashahada na Stashahada 3,471 na Shahada za Umahiri 754;

- (ii) kufanya mapitio ya kozi 10 katika Ndaki tano (5) ili ziendane na uhitaji wa wataalamu na soko la ajira;
- (iii) kuajiri watumishi 850 ili kuweza kuziba mapengo ya uhaba wa wafanyakazi sambamba na kuendana na ongezeko la wanafunzi;
- (iv) kushiriki katika maonesho ya Nane Nane, Sabasaba na Tume ya Vyuo Vikuu ili kutoa elimu kuhusu huduma zinazotolewa na chuo;
- (v) kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo vifaa vya maabara na vifaa kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji; na
- (vi) kukarabati majengo ya ofisi, hosteli za wanafunzi, madarasa pamoja na nyumba za makazi pamoja na mifumo ya maji na umeme katika majengo hayo.

**123. *Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza ufanisi wa kazi, chuo kitawajengea uwezo watumishi ili kuboresha utendaji kazi kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa jumla ya watumishi 850 kwa mchanganuo ufuatao: Viongozi waandamizi 40, ngazi ya Astashahada, Shahada na Shahada za Umahiri 250, Mafunzo ya ustadi wa kufundisha 450 na watumishi 110 watejengewa uwezo kulingana na uhitaji.

**124. *Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza idadi ya tafiti na Huduma za Ushauri (Consultancy Services) chuo kitatekeleza yafuatayo:

- (i) kitaratibu mashindano ya wanataaluma katika kufanya tafiti ambapo tafiti bora tano (5) zitachapishwa;
- (ii) kitachapisha machapisho 400 ya wanataaluma katika majarida

(peer reviewed journals) ambayo yatatokana na uhamasishwaji kwa wafanyakazi wanataaluma;

- (iii) kitahamasisha wafanyakazi wanataaluma kutumia majarida ya nje na ndani katika kuchapisha tafiti zao;
- (iv) kitawezesha wafanyakazi wanataaluma 50 kushiriki katika makongamano ya kisayansi ya Kitaifa na ya Kimataifa; na
- (v) kitawajengea uwezo wafanyakazi wanataaluma 400 katika eneo la kutoa huduma za ushauri ili kuongeza idadi ya wafanyakazi wenye uwezo wa kuendesha huduma hizi sambamba na kukiwezesha chuo kuongeza idadi ya huduma za ushauri na kupanua wigo wa mapato kupitia huduma hizi.

**125. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia, chuo kitatekeleza yafuatayo:

- (i) kitajenga nyumba sita (6) za wafanyakazi zenye uwezo wa kuchukua familia 33;
- (ii) kitaboresha huduma za Maktaba kwa kununua vitabu 2,000 pamoja na kuboresha miundombinu ya mfumo wa TEHAMA ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;
- (iii) kitaanza awamu ya pili ya ujenzi wa Ndaki mbili (2) ambazo ni; Ndaki ya Sayansi Asilia na Hisabati na Ndaki ya Sayansi za Ardhi na Uhandisi. Majengo haya yatakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 600 yatakapokamilika na kutoa nafasi za maabara za kutosha kujifunzia;
- (iv) kitajenga hosteli za wanafunzi katika Hospitali za Rufaa za Iringa na Singida kwa ajili ya wanafunzi wa Shahada za Udaktari na Ukunga wanaopata mafunzo kwa vitendo. Hosteli hizi zitakuwa

na uwezo wa kuchukua wanafunzi 600 pindi zitakapokamilika. Kukamilika kwa ujenzi huu kutasaidia kupunguza gharama za kupanga majengo ya watu/Taasisi binafsi kwa ajili ya malazi ya wanafunzi hao;

- (v) kitajenga kiwanda cha utengenezaji maji tiba ya hospitali (Intravenous-IV fluids) kwa ajili ya matumizi ya hospitali ya chuo na kuziuzia hospitali nyingine za umma ambazo kwa sasa zinaagiza maji tiba nje ya nchi pamoja na kutumika kama sehemu ya mafunzo;
- (vi) kitakarabati ukumbi wa mihadhara wa Chimwaga kwa kuweka samani mpya na kuboresha miundombinu yake ili kuufanya uwe wa kisasa kwa ajili ya matumizi ya Chuo na Taasisi mbalimbali; na
- (vii) kitanunua magari matano (5) yatakayosaidia katika shughuli za kila siku za uendeshaji za chuo.

### **Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi**

**126. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kudahili wanafunzi wapya 4,415 (Astashahada 1,480, Stashahada 695, Shahada za awali 2,100 na Shahada za Uzamili 140);
- (ii) kuandaa programu nne (4) za mafunzo ili kuongeza idadi ya wanafunzi katika fani za Ushirika na Biashara, Huduma za Kibenki, Usimamizi wa Fedha na Ushirika wa Mazao na Masoko;
- (iii) kitafanya miradi ya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalam pamoja na kuchapa makala mbalimbali kwa kushirikiana na vyuo vingine vya ndani na nje ya nchi kwa lengo la kusambaza elimu

inayokidhi mahitaji ya sasa ya jamii ili kupunguza umaskini;

- (iv) kitatoa na kueneza elimu ya ushirika nje ya Chuo ili kuchochea ari ya maendeleo katika jamii kwa kushirikiana na wadau wengine, hususan Wizara ya Kilimo; Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC); Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO); Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC) na vyama vya ushirika nchini na katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na
- (v) kitaendelea kuwezesha mafunzo ya wafanyakazi 64.

**127. *Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, chuo kitatekeleza yafuatayo:

- (i) kuendelea na ujenzi wa maktaba yenye uwezo wa kuchukua wasomaji 2,500 kwa wakati mmoja ili kuboresha mazingira ya kujifunzia;
- (ii) kitajenga ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 300 kwa wakati mmoja; na
- (iii) kitakarabati kumbi za mihadhara tatu (3), vyumba vya mihadhara 12, vyumba vya semina 9, jengo la maabara ya kompyuta na nyumba 10 za makazi.

### **Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**

**128. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kudahili jumla ya wanafunzi 16,650 (Cheti 3,000, Stashahada 4,000, Shahada ya kwanza 7,000, Shahada ya Uzamili 2,500 na Shahada ya Uzamivu 150);

- (ii) kufanya utafiti katika maeneo ya mazingira, TEHAMA, nishati, kilimo na chakula, uongozi na biashara, maendeleo ya utalii, sheria, uthibiti wa ubora, utawala na maendeleo, watu wenye ulemavu na mahitaji maalumu, maliasili, umaskini, utamaduni, haki za binadamu, maendeleo ya watu na mawasiliano pamoja na tafiti katika lugha na fasihi;
- (iii) kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu katika Nyanja za mazingira, TEHAMA, nishati, kilimo na chakula, uongozi na biashara, maendeleo ya utalii, sheria, uthibiti wa ubora, utawala na maendeleo; na
- (iv) kujenga jengo Makao Makuu ya Nchi Jijini Dodoma na majengo ya ofisi za wafanyakazi katika vituo vya mikoa ya Geita, Simiyu, Manyara, Lindi na Kigoma. Pia utafanyika ujenzi wa ukumbi wa mitihani mkoani Morogoro. Vilevile, katika kipindi hiki Chuo kinatarajia kufanya ukarabati katika majengo ya ofisi za vituo vya Mikoa ya Mwanza, Mbeya, Shinyanga, Kilimanjaro, Tabora na Kagera. Aidha, Chuo kitajenga uzio katika viwanja vya vituo vya Mtwara, Arusha na Rukwa. Pia utafanyika ukarabati wa vituo vya uratibu vya Zanzibar, Mafia na Tunduru.

### **Chuo Kikuu cha Ardhi**

**129. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Ardhi itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kudahili wanafunzi 5,255 wakiwamo ngazi ya shahada ya kwanza 4,955, ngazi ya shahada ya uzamili 215 na ngazi ya Shahada ya Uzamivu 85;
- (ii) kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi 31; wakiwemo 17 katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu na 10 katika ngazi ya

Shahada ya Uzamili na 4 katika ngazi ya Stashahada;

- (iii) kufanya miradi ya tafiti 50 zinazolenga kutatua changamoto za jamii hususan katika maeneo ya matumizi bora ya ardhi, utunzaji wa mazingira, kujikinga na maafa, usimamizi bora wa ardhi, makazi na majenzi. Aidha, Chuo kitaandaa machapisho 150 katika maeneo ya usimamizi wa ardhi na mazingira, makazi na majengo;
- (iv) kutoa mafunzo ya aina tano (5) ya kitaalam kwa jamii (outreach training) kuhusiana na matumizi bora ya ardhi, kujikinga na majanga, kutengeneza bidhaa kwa kutumia mabaki ya mazao ya kilimo, kutunza kumbukumbuku za biashara ndogondogo na utunzaji wa mazingira;
- (v) kutoa huduma za ushauri wa kitaalam kwa jamii kuhusu matumizi bora ya ardhi, upimaji na tathmini, usanifu majengo na ujenzi;
- (vi) kukamilisha ujenzi wa Jengo la Ardhi (Lands Building), ujenzi wa miundombinu ya TEHAMA na kuweka samani katika mabweni ya wanafunzi; na
- (vii) Kuendeleza ujenzi wa mabweni ya wanafunzi yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 592.

### **Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**

**130. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Sayansi, Teknolojia na Ubunifu itaendelea kuibua, kutambua, na kuendeleza ubunifu, ugunduzi na teknolojia zinazozalishwa nchini kupitia Mashindano ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili kuchangia katika kuzalisha ajira mpya. Aidha, itaratibu shughuli za Sayansi

Teknolojia na Ubunifu katika ngazi za mikoa na mamlaka za Serikali za mitaa ili kuwafikia wabunifu katika ngazi zote hususan vijijini.

**131. *Mheshimiwa Spika***, Serikali itaainisha matokeo ya utafiti hususan yale yenye manufaa ya moja kwa moja kwa jamii, pamoja na kubaini uwezo wa vifaa na wataalam katika taasisi za utafiti na Elimu ya Juu ili kuimarisha ushirikiano baina ya Taasisi za utafiti. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza yafuatayo:

- (i) itaendelea kuelimisha umma kuhusu matumizi na manufaa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu pamoja na kusimamia matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi; na
- (ii) itafanya mapitio ya Mwongozo wa Kitaifa wa Kutambua na Kuendeleza Ugunduzi, Ubunifu na Maarifa Asilia ili uendane na wakati na uweze kutumika na wadau wengi.

### **Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia – COSTECH**

**132. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/21, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kubaini na kugharamia miradi mipya 8 ya utafiti yenye kulenga kutatua matatizo ya wananchi katika sekta za Kilimo na Mifugo; Viwanda; Mafuta na Gesi; Uvuvi; Elimu; Afya na Mazingira;
- (ii) kufungasha na kusambaza matokeo ya utafiti kwa wadau ikiwemo viongozi, watunga sera na wananchi, kupitia machapisho, runinga na radio pamoja magazeti ili kuelimisha jamii kuhusu ufumbuzi wa matatizo kutokana na utafiti uliofanyika; na

- (iii) kubiasharisha matokeo matano (5) ya tafiti nchini yanayolenga kutatua matatizo kwa jamii ili kuthibitisha uzalishaji, muendelezo na utumiaji wa matokeo ya utafiti katika mifumo ya kibiashara kwa kutumia viwanda na masoko.

**133. *Mheshimiwa Spika***, Serikali itaendelea kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu pamoja na kuboresha mifumo ya ubunifu kwa kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kugharamia kazi za wabunifu ili kuwajengea uwezo, kuwahamasisha na kuendeleza ujuzi na umahiri wao;
- (ii) kuratibu mashindano ya kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ya mwaka 2021 ili kutambua, kuendeleza na kurasimisha matokeo ya ubunifu kwa ajili ya kuchangia maendeleo ya nchi;
- (iii) kuboresha mifumo ya ubunifu na kuendeleza wabunifu nchini ili kuhamasisha na kuongeza matumizi ya ubunifu katika mifumo rasmi ya uchumi na viwanda kwa maendeleo na ushindani wa kibiashara;
- (iv) kusimamia uanzishwaji wa mifumo na miongozo ya kuzijengea uwezo taasisi zinazofanya tafiti nchini katika kulinda viwango vya utekelezaji wa utafiti kulingana na weledi na ubobezi wa taaluma ili kupata matokeo ya utafiti yanayotatua matatizo ya nchi kijamii na utamaduni, kiuchumi na kisiasa;
- (v) kufanya tathmini na ufuatiliaji wa miradi inayofadhiliwa na Tume ili kuboresha mfumo wa udhibiti na utoaji vibali vya utafiti nchini kwa lengo la kuhakikisha utekelezaji na uendelezaji wa tafiti unafuata sheria na taratibu; na
- (vi) kuchangia shughuli za ubunifu kupitia mradi wa *South African*



*Innovation Support* (SAIS) unaotekelezwa katika nchi tano kusini mwa bara la Afrika ili kuhamasisha ushindani, ujuzi na ubora wa ubunifu wa wabunifu nchini na katika nchi hizo tano za Bara la Afrika.

**134. *Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia COSTECH itaandaa mwongozo wa uhawilishaji wa teknolojia kupitia uwekezaji wa nje, pamoja na uhakiki wa teknolojia zinazoibukia kwa lengo la kurasimisha uratibu na kulinda haki miliki na hati miliki. Aidha, itasimamia na kuhakikisha kuwa elimu ya maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu inatekelezwa kukidhi mipango ya taifa ya maendeleo iliyowekwa (TDV 2025) na ile ya kimataifa (STISA 2063 na Malengo 17 ya Maendeleo endelevu).

### **Tume ya Nguvu za Atomiki**

**135. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki (TAEC) itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kuendelea na ujenzi wa maabara changamano kwa awamu ya pili na maabara za kanda katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Zanzibar, Dodoma na Mbeya ambazo zitaboresha na kusogeza huduma kwa wananchi; na
- (ii) kuanzisha ofisi za Tume katika kanda ya Kati - Dodoma, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini - Mbeya na Kanda ya Kusini -Mtwara ili kusogeza huduma kwa wananchi.

**136. *Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Tume imefanya upembuzi yakinifu wa miradi miwili (2) ambapo utekelezaji wake utasaidia kuhifadhi

mazao yanayoharibika haraka (perishables) kurefushwa muda wa kuhifadhi bila kuharibika. Aidha, itawezesha tafiti za kisayansi kwa wadau katika uzalishaji wa dawa za mazao ya kilimo na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kuagiza madawa ya kutibu saratani kutoka nje ya nchi. Miradi hiyo ni:

- (i) Mradi wa uanzishwaji wa kinu cha kuhifadhi mazao ya kilimo ikiwemo vyakula viharibikavyo kirahisi (perishable) kwa kutumia mionzi (Multipurpose Irradiator Facility); na
- (ii) Mradi wa kinu cha tafiti za kinyuklia (Research Reactor) wa kutengeneza madawa ya kutibu saratani kwa viwanda vya madawa.

Aidha, Serikali itaratibu miradi mipya mitano (5) ya kitaifa na miradi 26 ya kikanda ambayo itagharamiwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (International Atomic Energy Agency (IAEA)).

**137. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuhakikisha afya za wafanyakazi wanaotumia teknolojia ya nyuklia zinakuwa salama, Serikali kupitia Tume itatekeleza yafuatayo:

- (i) itaanzisha kituo cha mafunzo cha usalama na kinga ya mionzi katika ngazi ya diploma, cheti na mafunzo ya muda mfupi ambayo yatalenga kuiweka nchi katika usalama zaidi dhidi ya mionzi na nyuklia kwa ujumla;
- (ii) itaendelea na upimaji wa viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 2,200 wanaofanya kazi kwenye vyanzo vya mionzi Hospitali katika, Viwanda na Migodi ili kuhakikisha afya zao zinakuwa salama; na

- (iii) itaendelea kufanyia matengenezo na kusimika mitambo inayotumia teknolojia ya nyuklia pamoja na kuhakiki ubora wa vifaa/mitambo vinavyotumia teknolojia ya nyuklia katika hospitali, viwanda, migodi na kampuni za ujenzi wa barabara.

**138. *Mheshimiwa Spika***, ili kulinda umma wa Tanzania na mazingira yake yasichafuliwe na mabaki ya vyanzo vya mionzi ambavyo havitumiki tena kutokana na nguvu yake kupungua au teknolojia kubadilika, Serikali itaendelea kukusanya, kusafirisha na kuhifadhi mabaki ya vyanzo vya mionzi yasiyotumika kutoka vituo sita na kuyahifadhi katika jengo maalumu (Central Radioactive Waste Management Facility- CRWMF) lililopo Arusha ambapo ukusanyaji na uhifadhi unafanyika.

**139. *Mheshimiwa Spika***, katika kuwalinda wataanzania na kulinda bidhaa zetu kwenye masoko ya nje, Serikali kupitia Tume itatekeleza yafuatayo:

- (i) itapima kiasi cha mionzi katika sampuli zipatazo 20,000 za vyakula, tumbaku na mbolea zinazotoka na kuingia nchini ili kubaini endapo hazina madhara ya mionzi;
- (ii) itapima mionzi kwenye mazingira katika vituo 50 ili kubaini iwapo kuna uchafuzi wa mazingira utokanao na mionzi; na
- (iii) itasimamia kituo cha kupima mionzi katika hewa ya anga (Radionuclide Monitoring Station-TZPRN64) kilichopo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam chini ya mkataba wa kimataifa wa *Comprehensive Nuclear Test-Ban Treaty (CTBT) for Non-Proliferation Test (NPT) of Nuclear Weapons*.

**140. *Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Tume itafanya tafiti kuhusu matumizi ya teknolojia ya nyuklia na kuchapisha matokeo yake ili kuhamasisha matumizi ya matokeo hayo. Aidha, itaanzisha, itasimamia na kufuatilia utekelezaji wa tafiti na miradi ya kitaifa na kikanda inayotumia sayansi ya nyuklia na teknolojia yake ili kuendelea kuleta faida kwenye sekta mbalimbali ikiwemo Afya, Kilimo, Mifugo na Maji ikiwa pamoja na kujijengea uwezo katika ubunifu na matumizi ya teknolojia hii.

**141. *Mheshimiwa Spika***, katika kubaini hali ya usalama inayoendelea katika migodi na vituo vya mionzi, Serikali kupitia Tume itatekeleza yafuatayo:

- (i) itakagua migodi sita (6) (Geita Gold Mine, Bulyanhulu Gold Mine, North Mara Gold Mine, Buzwagi Gold Mine, Williamson Gold Mine, na Stami Gold Tulawaka;
- (ii) itatathmini maombi 500 ya leseni mbalimbali kwa kuzingatia matakwa ya sheria na kanuni za usalama wa mionzi ili kubaini kama yanakidhi matakwa ya Sheria na Kanuni zake;
- (iii) itakagua vituo 500 vyenye vyanzo vya mionzi ayonisha (Ionizing Radiation) ili kubaini hali ya usalama kwa wagonjwa, wafanyakazi na umma; na
- (iv) itakagua vituo 120 vinavyotoa mionzi isiyo ayonisha (Non-Ionizing Radiation) mfano minara ya simu, redio, runinga na vifaa vingine vya mionzi ili kubaini usalama wa wakazi wa maeneo husika.

## Taasisi Teknolojia Dar es Salaam (DIT)

**142. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Taasisi ya Teknolojia Kampasi Kuu ya Dar es Salaam itatekeleza yafuatayo;

- (i) itadahili wanafunzi wapya 2,400 na kuhudumia wanafunzi 3,300 wanaondelea na masomo na kufanya Taasisi kuwa na jumla ya wanafunzi 5,700;
- (ii) itakamilisha tafiti saba (7) zinazoendelea na kuanza kufanya tafiti mpya tatu (3) na kutekeleza miradi 25 ya huduma za ushauri wa kitaalamu kwa lengo la kutatua changamoto za kijamii. Tafiti hizo ni kuhusu:
  - (a) kutengeneza mtambo maalumu wa kuwezesha mazingira rafiki ya kilimo mjini;
  - (b) kukamilisha utengenezaji wa mfumo wa umwagiliaji kwa kutumia nguvu za jua kwenye kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia maji ya kisima;
  - (c) kutengeneza mfumo wa kuhifadhi, kusambaza na kuchakata taarifa za bioanwai hapa nchini kwa kushirikiana na COSTECH unaofadhiliwa na Shirika la kimataifa la *JRS Biodiversity Foundation* la Marekani;
  - (d) kuboresha teknolojia ya mfumo wa usimamizi wa hospitali na vituo vya afya ambao kwa sasa unatumika katika hospitali ya Amana kwa majaribio;
  - (e) kutengeneza mfumo wa mawasiliano yasiyo tumia nyaya kwenye magari yasiyo na dereva;
  - (f) kukamilisha utengenezaji wa mashine ya kuchakata kahawa kwa kigezo cha rangi utakaosaidia wakulima wa kahawa kuongeza mnyoro wa thamani; na
  - (g) kutengeneza injini itakayotumia mfumo wa gesi asilia.

(i) itaendelea na utekelezaji wa mradi wa 'East Africa for Transformation and Regional Integration Project (EASTRIP)' kama ifuatavyo:

- (a) kujenga mabweni mawili (2) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 na jengo la ghorofa 12 la kituo cha umahiri wa TEHAMA katika Kampasi ya Dar es Salaam;
- (b) kuanza ujenzi wa mabweni mawili (2) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 600 na jengo la ghorofa sita (6) la kituo cha umahiri wa teknolojia ya utengenezaji wa bidhaa za ngozi katika Kampasi ya Mwanza; na
- (c) kuhuisha mitaala ya programu 14 (Stashahada 10, Shahada 3, na Umahiri 1) na kuanzisha mitaala ya programu 8 (Stashahada 6, Shahada 1, na Umahiri 1).

**143. Mheshimiwa Spika,** Taasisi itaanza utekelezaji wa mradi wa maendeleo wa *Tanzania Education Labour Market Survey (TELMS)* awamu ya pili unaofadhiliwa na Serikali ya Italia. Mradi huu una lengo la kuvijengea uwezo vyuo vinne (4) vya ufundi nchini (DIT, KIST, ATC na MUST) ili kuzalisha wataalamu waliobobea katika fani za ufundi na teknolojia ambapo yafuatayo yatatekelezwa:

- (i) kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa majengo ya vituo viwili vya ujasiriamali, ubunifu na usambazaji wa teknolojia (Centres of Entrepreneurship, Innovation and Technology Transfer) katika kampasi za Mwanza na Dar es Salaam;
- (ii) kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa jengo la ghorofa nne la kufundishia katika Kampasi ya Myunga iliyopo mkoani Songwe;
- (iii) kufanya ununuzi ya magari matatu (3) ya mradi;
- (iv) itaendelea kushiriki kwenye zabuni za miradi ya kitaifa minne (4)

kwa lengo la kuijengea Taasisi uwezo wa kifedha na kutatua changamoto za jamii kupitia Kampuni ya Taasisi iitwayo "DIT Company Limited"; na

- (v) itaendelea kushiriki katika kusimamia mchakato wa kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu wa Taasisi na kitaifa.

### **Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya**

**144. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kudahili jumla ya wanafunzi 7,150 (Stashahada 3,327, Shahada ya Kwanza 3,705 na Shahada za Uzamili 118);
- (ii) kununua vifaa vya kisasa vya maabara na karakana kwa lengo la kuboresha utoaji wa mafunzo katika fani za Sayansi na Teknolojia ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia;
- (iii) kufanya tafiti 120 zinazolenga kuongeza ubunifu na kuendelea kutoa ushauri elekezi katika nyanja za sayansi na teknolojia ili kuchochea ukuaji wa uchumi wa viwanda;
- (iv) kuboresha mnyororo wa thamani wa zao la viazi kwa kushirikiana na *Hanze University of Applied Sciences (Netherlands)* na MATI Uyole kwa kujenga uwezo kwa wanataaluma na kutoa mafunzo kwa wakulima;
- (v) kutatua changamoto ya makazi kwa wanafunzi kwa kukamilisha ujenzi wa majengo mawili (2) ya hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja na jengo la madarasa la Ndaki ya Usanifu na Teknolojia ya Majengo lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800 kwa wakati mmoja;
- (vi) kukamilisha ujenzi wa jengo la Maktaba lenye uwezo wa

kuchukua wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, itakarabati madarasa, hosteli na nyumba za watumishi;

- (vii) kuongeza matumizi ya nishati mbadala ili kuwa na vyanzo endelevu vya nishati kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Chuo kwa kufunga taa 30 zinazotumia umeme wa jua na hivyo kupunguza gharama za umeme;
- (viii) kuanzisha Kituo cha Teknolojia Vijijini katika Kampasi ya Rukwa ili kuchochea matumizi ya teknolojia stahiki (appropriate technology) katika maeneo ya vijijini; na
- (ix) kutoa mafunzo ya Stashahada ya Ualimu wa Ufundi kwa wanafunzi 400, Shahada ya Ualimu wa Ufundi kwa wanafunzi 400 na Stashahada ya Uzamili ya Ualimu wa Ufundi wa wanafunzi 50 ili kukidhi mahitaji ya Walimu wa Ufundi katika Shule na Vyuvo vya Ufundi nchini.

### **Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha (NM-AIST)**

**145. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha itatekeleza yafuatayo:

- (i) itadahili jumla ya wanafunzi 125 ambapo wanafunzi 100 ni wa ngazi ya Shahada ya Uzamili na wanafunzi 25 wa ngazi ya Shahada ya Uzamivu;
- (ii) itakamilisha utafiti katika miradi 21 ya kitafiti na ubunifu kwa kufadhili wanafunzi sanjari na kulipa gharama za utafiti kwa wanafunzi na wanataaluma ili kuzalisha bunifu katika maeneo ya



TEHAMA, sumu kuvu, uchakataji wa ngozi, viini lishe kwa watoto wenye udumavu na ugonjwa wa kimeta kwa mifugo na wanyamapori;

- (iii) itaratibu shughuli za utafiti na ubunifu kwa kuzalisha bunifu mbili (2) zitakazofikia katika hatua ya atamizi na hatimaye bidhaa kamili; na
- (iv) kutatua changamoto ya makazi kwa wanafunzi kwa kuanza ujenzi wa bweni litakalokuwa na uwezo wa kuhudumia wanafunzi 500.

### **Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimaliwatu**

**146. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia idara ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimaliwatu itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itaendelea kukamilisha taratibu za ujenzi wa jengo kuu la ofisi za Wizara Mtumba - Dodoma kulingana na miongozo na maelekezo ya Serikali;
- (ii) itakamilisha mpango wa utumiaji wa Mfumo wa mawasiliano wa Kielektroniki (E-office) wa kupokea, kutunza na kusambaza nyaraka za ofisi kwa lengo la kuleta ufanisi, kupunguza gharama na kuongeza kasi ya mawasiliano katika ofisi; na
- (iii) itasimamia na kuhakiki Rasilimaliwatu kwa lengo la kubaini mafanikio na changamoto za kiutendaji na kuzipatia ufumbuzi.

**147. *Mheshimiwa Spika***, katika kuleta ufanisi na weledi kwa watumishi, Serikali itaendelea kufanya mapitio ya Mpango wa Mafunzo wa Wizara pamoja na kuratibu mafunzo ya muda mrefu na mfupi yakiwemo: Mafunzo Elekezi; Maadili katika Utumishi wa Umma; Haki na Wajibu wa

Watu Wenye Ulemavu; UKIMWI na Magonjwa yasiyoambukizwa; na Utumiaji wa Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi (Open Performance Review and Appraisal System – OPRAS). Aidha, itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wanaokaribia kustaafu ili kujiandaa na maisha baada ya kustaafu.

### **Usimamizi wa Rasilimali za Wizara**

**148. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia idara ya Usimamizi wa Rasilimali za Wizara itatekeleza yafuatayo:

- (i) itakagua matumizi ya fedha katika Taasisi za Wizara;
- (ii) itaendelea na ukaguzi wa ukusanyaji wa maduhuli na matumizi katika Taasisi za Wizara;
- (iii) itafanya ukaguzi wa taratibu za ununuzi na usimamizi wa Mikataba inayotekelezwa na Wizara ikiwemo mikataba ya Ujenzi na ukarabati; na
- (iv) itafanya ukaguzi wa matumizi ya fedha za Wizara (Expenditure Management) Makao Makuu ya Wizara.

### **Uendelezaji na Uboreshaji wa Sera, Sheria na Miongozo ya Elimu**

**149. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali itaendelea kuendeleza na kuboresha Sera, Sheria na Miongozo ya Elimu kama ifuatavyo:

- (i) itahuisha Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu - Education Sector Development Plan (ESDP) wa Miaka Mitano 2020/21-2025/26 na Mpango Mkakati – Strategic Plan (SP) wa Wizara 2020/21-2025/26 ili kuweka mwelekeo wa Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika kutekeleza Mipango ya Kitaifa na Kimataifa;

- (ii) itafanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera, Mpango na Mkakati ya Wizara 2016/17 - 2020/21;
- (iii) itaendelea kutoa ushauri wa kisheria kuhusu sera, nyaraka, miongozo na mikakati ya Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa taasisi zilizo chini ya Wizara;
- (iv) itaendelea kutoa ushauri kuhusu mikataba na itifaki za mashirika ya kitaifa, kikanda na kimataifa ambayo nchi inapaswa kuridhia pale inapojitokeza; na
- (v) itakamilisha mapitio ya Sera ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996 ili kuwa na Sera ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu inayoendana na mahitaji ya sasa.

## **USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYO CHINI YA WIZARA**

**150. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Wizara itatekeleza miradi ifuatavyo;

### **Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (Education Programme for Results – EP4R)**

**151. *Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (EP4R) kwa mwaka 2020/21 itatekeleza shughuli zifuatazo:

- (i) Kuboresha Vyuo vya Ualimu vya Mhonda na Dakawa kwa kukarabati na kujenga miundombinu katika vyuo hivyo ili kukidhi mahitaji ya sasa na kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji;
- (ii) kukamilisha ujenzi wa Hosteli, Bwalo la chakula na mifumo ya maji katika Chuo Kikuu cha Mzumbe ili kuwezesha upatikanaji wa malazi na kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji;

- (iii) Kukarabati Nyumba za Wakufunzi katika Vyuo vya Ualimu;
- (iv) kuendelea kutoa motisha kwa Halmashauri 184 kutokana na utekelezaji wa vigezo vilivyokubalika kati ya Serikali na wafadhili;
- (v) kuwezesha ukaguzi wa nje wa Programu na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mradi; na
- (vi) itaendelea kuratibu ujenzi wa ofisi 55 za Uthibiti Ubora wa Shule ngazi ya wilaya;

### **Mradi wa Elimu na Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi (Education and Skills for Productive Jobs - ESPJ)**

**152. *Mheshimiwa Spika*,** Mradi wa Elimu na Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi unatakelezwa kwa utaratibu wa Lipa Kulingana na Matokeo - *Payment for Results* (P4R). Katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Mradi wa ESPJ itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kuwezesha Karakana na Maabara za Wabunifu kwa kuzipatia vifaa vya kisasa ili kuboresha mazingira ya uendelezaji ubunifu na ufundishaji na ujifunzaji kwa vitendo;
- (ii) kuendelea na utekelezaji wa Mfuko wa Kukuza Stadi za Kazi kwa kutoa fedha za kuwezesha taasisi za mafunzo ya ufundi kununua vifaa na kuboresha mitaala kupitia maandiko ya kiushindani ili kuendana na mahitaji ya kijamii;
- (iii) kuboresha miundombinu ya Taasisi zinazotoa mafunzo ya ufundi ikiwemo VETA kwa ujenzi na ukarabati;
- (iv) kujengea uwezo Wizara na Taasisi kwa kununua vifaa na kutoa mafunzo ili kuwawezesha kusimamia ubora wa elimu ya ufundi na stadi za kazi;
- (v) kutoa ufadhili kwa Vijana ili kuwawezesha kupata ujuzi kupitia

Mwongozo wa Mamlaka ya Elimu Tanzania;

- (vi) kuwezesha ujenzi wa Maktaba mpya 5 katika mikoa ya Singida, Shinyanga, Simiyu, Dodoma na katika Chuo cha Maktaba - Bagamoyo. Aidha, Ukarabati wa Maktaba 9 za mikoa utafanyika; na
- (vii) kuimarisha Vyuo vya VETA na Elimu ya Ufundi kwa kufanya mafunzo kwa njia ya Uanagenzi (Apprenticeship).

### **Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Ufundi, Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu**

**153. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia mradi wa kuimarisha Elimu ya Ufundi, Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kuwezesha uendeshaji na maendeleo ya Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi;
- (ii) kuwezesha wanafunzi wa vyuo vya ufundi stadi kupata ujuzi wa kujiari na kuajiriwa; na
- (iii) kuanzisha vituo vya mafunzo ya ufundi stadi.

### **Mradi wa Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MEM) – Kuimarisha Mafunzo ya Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu - KKK**

**154. *Mheshimiwa Spika***, Serikali imesaini mkataba wa makubaliano na wadau wa Maendeleo - GPE tarehe 15 Januari, 2020 kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya pili ya Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi. Programu hii inalenga kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa watoto wenye umri

wa miaka 5-13 walio ndani na nje ya mfumo rasmi. Mpango huu unafadhiliwa na Mfuko wa Ushirika wa Kimataifa wa Elimu (*Global Partnership for Education-GPE Fund*). Katika mwaka 2020/2021, itatekeleza kazi zafuatazo:

- (i) kuwezesha Vituo vya Walimu (TRC) kutekeleza Mpango wa mafunzo endelevu kazini (CPD);
- (ii) kuandaa mwongozo kwa ajili ya Waratibu wa Vituo vya Walimu (TRC) ili kuendana na Mpango wa mafunzo endelevu kazini (CPD);
- (iii) kuwezesha mafunzo ya Waratibu wa TRC na Maafisa Elimu kata 966;
- (iv) kuwezesha Tathmini na Ufuatiliaji wa Mradi;
- (v) kuandaa moduli za mafunzo endelevu kazini kwa walimu wa shule za Msingi kuhusu mtaala mpya, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na upimaji endelevu;
- (vi) kuandaa moduli za mafunzo endelevu kazini kwa wawezeshaji wa MEMKWA kuhusu mtaala mpya, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na upimaji endelevu;
- (vii) kuwezesha uandaaji, uchapaji na usambazaji wa vitabu vya wanafunzi wa Darasa la VI na VII pamoja na kiongozi cha mwalimu kwa masomo yote;
- (viii) kuandaa miongozo na kuboresha mihtasari kwa ajili ya Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Watoto Walioikosa (MEMKWA) na kufanya upimaji;
- (ix) kuwezesha mafunzo kazini kwa walimu wenye mahitaji maalum kuhusu mtaala, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na upimaji endelevu; na

- (x) kuwezesha mafunzo kwa Wawezeshaji wa MEMKWA wenye mahitaji maalum ngazi ya Mikoa na Halmashauri.

### **Mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu (TESP)**

**155. *Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Mradi wa TESP itatekeleza shughuli zifuatazo:

- (i) kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo vifaa vya maabara ya Sayansi, TEHAMA, vitabu vya kiada vya shule za Msingi na Sekondari pamoja na vitabu vya kiada na ziada kwa Vyuo vya Ualimu 35 vya Serikali;
- (ii) kuwezesha Vyuo vya Ualimu 35 vya Serikali kuunganishwa katika Mkongo wa Taifa;
- (iii) kukarabati Maabara za Sayansi nne (4), za TEHAMA tano (5) na Maktaba sita (6) katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali; na
- (iv) kuwezesha mapitio ya mtaala wa Elimu ya Ualimu, uchapaji na usambazaji na miongozo kwa ajili ya uendeshaji wa mafunzo kazini kwa masomo 21 na moduli 6 za mkakati jumuishi. Aidha, itawezesha uandaaji, usambazaji, ufuatiliaji na tathmini wa Kiunzi cha Ujuzi wa Mwalimu na Mkufunzi.

**156. *Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha utendaji kazi wa watumishi, Serikali kupitia mradi wa TESP itatoa mafunzo kazini katika maeneo yafuatayo:-

- (i) utawala na matumizi ya TEHAMA kwa watumishi 1,300 kutoka Vyuo vya Ualimu;
- (ii) usimamizi wa fedha za miradi kwa watumishi 50 wa makao makuu ya Wizara;

- (iii) matumizi ya TEHAMA kwa watumishi 210 wa vyuo vya ualimu wakiwemo Wakutubi na Makatibu muhtasi;
- (iv) usimamizi na ufuatiliaji kwa Bodi za Vyuo vya Ualimu 35 vya Serikali;
- (v) matumizi ya vifaa visaidizi na TEHAMA kwa Walimu na Wakufunzi 300 wenye mahitaji maalumu;
- (vi) matumizi ya Lugha ya Alama kwa walimu wa shule za Msingi 350 na Sekondari 150; na
- (vii) mbinu za ufundishaji kwa Wakufunzi 570 wakiwemo wa masomo ya Sayansi, Hisabati, Biashara, Kilimo, *Development Studies*, Elimu ya Michezo, Uraia na Sanaa.

### **Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu (UTC)**

**157. *Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2020/21, Serikali kupitia Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu (UTC), itatekeleza shughuli zifuatazo:

- (i) Ujenzi wa kumbi za Mihadhara, ununuzi wa vifaa vya Maktaba na ukarabati wa jengo la utawala katika Kampasi ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima Morogoro; na
- (ii) Kuendelea na Ujenzi na Ukarabati wa vyuo vya Ualimu vinne (4) vya Shinyanga, Mpuguso, Ndala na Kitangali.

### **Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni**

**158. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia mradi wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni itatekeleza yafuatayo:

- (i) kufuatilia na kutathmini ujenzi wa miundombinu ya vyoo na maji awamu ya pili katika Shule za Msingi 946 kwa kushirikiana na Wizara zinazotekeleza Programu Endelevu ya Usambazaji wa Maji



Vijijini na Usafi wa Mazingira ili kubaini mafanikio, changamoto na kutoa ushauri stahiki;

- (ii) kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya maji na vyoo vya mfano katika Vyuo vya Ualimu vitano (5) vya Katoke, Nachingwea, Kinampanda, Shinyanga na Murutunguru ili kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu;
- (iii) kutoa elimu elekezi kuhusu utumiaji wa Mwongozo wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira shuleni kwa Maafisa Elimu na Wathibiti Ubora wa Shule ili waweze kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni; na
- (iv) kununua magari matatu (3) ili kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa programu katika Mikoa na Halmashauri nchini.

### **Mradi wa Kuimarisha Ubora Elimu ya Sekondari - SEQUIP**

**159. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia mradi wa Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kuandaa moduli na Mwongozo wa Elimu Jumuishi pamoja na kutoa mafunzo ya elimu jumuishi kwa walimu wa Shule za Sekondari za Serikali ili kuwajengea uwezo katika kazi zao na kupata uelewa zaidi kuhusu elimu jumuishi;
- (ii) kuandaa na kutekeleza mkakati wa upatikanaji wa walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati ili kupunguza changamoto za upatikanaji wa walimu na kuongeza ufaulu wa wanafunzi;
- (iii) kuandaa mwongozo kwa ajili ya kufanya tathmini ya ujifunzaji kwa Elimu ya Sekondari;

- (iv) kuandaa mwongozo wa ufundishaji wa TEHAMA na kutoa mafunzo kwa walimu 1,000 kutoka shule za Sekondari 500 kuhusu moduli za TEHAMA; na
- (v) kuainisha na kuboresha vituo vya kutolea Elimu nje ya mfumo rasmi ili kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu.

**Mradi wa Kujenga Ujuzi Afrika Mashariki - *East Africa for Transformation and Regional Integration Project (EASTRIP)***

**160. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Mradi wa Kujenga Ujuzi Afrika Mashariki - EASTRIP itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itawajengea uwezo wanataaluma 100 pamoja na kuandaa na kutoa ithibati ya mitaala ya Umahiri ya Elimu ya Ufundi (Competence Based Curricular); na
- (ii) itajenga uwezo kwa vyuo vya ufundi kwa kutoa mafunzo ya kufundisha elimu ya ufundi ya ujuzi (Competecec Based Training) kwa wanataaluma 400 na kuanzisha *National TVET Resource Centre*.

**TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)**

**161. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO itatekeleza yafuatayo:

- (i) Itafanya tathmini ya mikataba ya UNESCO iliyoridhiwa na Serikali;
- (ii) itasimamia utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali iliyopitishwa katika mpango wa UNESCO wa mwaka 2020/22;
- (iii) itashirikiana na wadau katika kutumia fursa mbalimbali

zinazotokana na uanachama wa Serikali katika shirika la UNESCO;

- (iv) itachangia upatikanaji wa Elimu bora kwa wote kwa kujenga utamaduni endelevu wa kujifunza;
- (v) itatoa mafunzo ya uelewa kwa masuala ya UKIMWI na rushwa katika mazingira ya kazi; na
- (vi) itaimarisha mazingira ya utendaji kazi katika kwa kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi na upatikanaji vitendea kazi.

#### **D. SHUKRANI**

**162. *Mheshimiwa Spika***, napenda kutambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu katika kutekeleza na kufanikisha majukumu ya Wizara yangu. Kipekee kabisa namshukuru Mheshimiwa William Tate Olenasha (Mb), Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kusimamia Wizara hii. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Dkt. Leonard Douglas Akwilapo, Naibu Makatibu Wakuu; Profesa James Epiphan Mdoe na Dkt. Ave Maria Semakafu, Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi, Wakuu wa Idara na Vitengo, na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano wao wa karibu katika kusimamia na kutekeleza majukumu ya kila siku ya Wizara.

**163. *Mheshimiwa Spika***, napenda kuwashukuru viongozi wa vyama vya wafanyakazi, Watumishi wa Wizara na Taasisi zake, Walimu, Wanafunzi na Wadau wa Elimu, kwa ushirikiano wao. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wamiliki wa Shule, Vyuho na Taasisi Binafsi ambao wamekuwa wakishirikiana na Serikali katika utoaji wa elimu hapa nchini.

**164. *Mheshimiwa Spika***, napenda kuwashukuru Washirika mbalimbali wa Maendeleo na Wadau wa Elimu wote ambao wamechangia kufanikisha Mipango ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Naomba kuwatambua baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za: Algeria, Austria, Brazil, Canada, China, Cuba, Finland, Hungary, India, Indonesia, Italia, Israel, Japan, Korea ya Kusini, Malta, Marekani, Malaysia, Misri, Morocco, Netherland, New Zealand, Norway, Palestine, Romania, Saudi Arabia, Sweden, Thailand, Ufaransa, Urusi, Uswisi, Uingereza, Uholanzi, Ujerumani na Venezuela. Aidha, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika.

**165. *Mheshimiwa Spika***, napenda pia kuyashukuru mashirika yaliyochangia kufanikisha programu za Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo ni pamoja na; Benki ya Dunia, *Department for International Development (DfID)*, *Swedish International Development Agency (SIDA)*, Umoja wa Nchi za Ulaya, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Jumuiya ya Madola, *Global Partnership in Education (GPE)*, *United Nations International Children's Emergency Fund (UNICEF)*, *United Nations Development Programme (UNDP)*, *United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization (UNESCO)*, USAID, *Inter University Council for East Africa (IUCEA)*, *Human Development Innovation Fund (HDIF)*, *Deutscher Akademischer Austauschdienst (DAAD)*, *British Council*, *Campaign for Female Education (CAMFED)*, *Commonwealth Secretariat*, *Aga Khan Education Services*, *Japan International Cooperation Agency (JICA)*, *Karibu Tanzania Organization (KTO)*, *Korea International Cooperation Agency (KOICA)*, *WaterAid*, *Plan International*, *Tanzania Education Network/Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET)*, *Christian Social Services Commission (CSSC)* na Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA).

## **E. MAOMBI YA FEDHA WA MWAKA 2020/21**

**166. Mheshimiwa Spika,** ili kuwezesha utekelezaji wa malengo kwa mwaka wa fedha 2020/21, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,348,563,375,000.00** kwa mchanganuo ufuatao:

- (i) **Shilingi 87,361,755,810.00** zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya idara na vitengo vilivyoko Makao Makuu ya Wizara. Kati ya fedha hizo **Shilingi 61,802,934,325.00** ni Mishahara na **Shilingi 25,558,821,485.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo;
- (ii) **Shilingi 403,687,395,190.00** zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wakala na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Kati ya fedha hizo **Shilingi 356,908,438,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 46,778,957,190.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na
- (iii) **Shilingi 857,514,224,000.00** zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 606,715,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 250,799,224,000.00** fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**167. Mheshimiwa Spika,** naliomba pia Bunge lako tukufu liidhinishhe jumla ya **Shilingi 2,239,181,000.00** kwa ajili ya Fungu 18 Tume ya Taifa ya UNESCO. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 706,888,000.00** ni kwa ajiri ya Mishahara na **Shilingi 1,532,293,000.00**

ya Kawaida (Mishahara ni **Shilingi 706,888,000.00** na Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 1,532,293,000.00**).

**168. Mheshimiwa Spika,** napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

**169. Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni <http://www.moe.go.tz>.

**170. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.



Mitambo ya kujifunzia Chuo Cha ufundi Arusha (ATC)



Usambazaji wa vitabu vya kiada na ziada shule za msingi na sekondari.  
Wanafunzi ya shule ya msingi Bunge wakitumia vitabu vilivyotolea katika Shule hiyo





**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Mji wa Serikali - Mtumba

Mtaa wa Afya

S. L. P. 10,

40479 Dodoma

Simu: 0262 963 533

Tovuti: [www.moe.go.tz](http://www.moe.go.tz) | Barua pepe: [info@moe.go.tz](mailto:info@moe.go.tz)